Ujumbe wa Waangalizi
wa Uchaguzi wa Umoja wa Ulaya

# Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

## Ripoti Kamili
**Uchaguzi Mkuu**
**2015**

# Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

## RIPOTI KAMILI

**UCHAGUZI MKUU**
**25 OKTOBA 2015**

## UJUMBE WA WAANGALIZI
## WA UCHAGUZI WA UMOJA WA ULAYA

*Jumbe za Uangalizi wa Uchaguzi za Umaoja wa Ulaya ziko huru na taasisi za Umoja wa Ulaya. Tamko hili limeandaliwa na Ujumbe wa Waangalizi wa Uchaguzi wa Umoja wa Ulaya kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na linawasilisha yalioyobainiwa na ujumbe huo kuhusu uchaguzi mkuu wa tarehe 25 Oktoba. Taasisi za Umoja wa Ulaya hazitoi uhakika wa usahihi wa data zilizomo kwenye tamko hili, na haziwajibiki kwa namna ambavyo zinaweza kutumika*

**FAHIRISI**


I. MUHTASARI WA UTENDAJI ..... 5

II. UTANGULIZI ..... 11

III. HISTORIA YA KISIASA ..... 12

IV. MFUMO WA KISHERIA ..... 13

- A. Kanuni na Ahadi za Kimataifa na Kikanda ..... 13
- B. Utungaji Sheria za Kitaifa za Uchaguzi ..... 13
- C. Mfumo wa Uchaguzi ..... 14

V. UTENDAJI WA UCHAGUZI ..... 14

- A. Muundo na Mpangilio ..... 14
- B. Utendaji wa Uchaguzi ..... 15
- C. Uwekaji Mipaka ya Majimbo ..... 17
- D. Elimu kwa Wapipga Kura. ..... 18

VI. DAFTARI LA WAPIGA KURA ..... 19

- A. Haki ya KupigaKura. ..... 19
- B. Uandikishaji Wapiga Kura ..... 19

VII. USAJILI WA VYAMA VYA SIASA NA WAGOMBEA ..... 21

- A. Usajili wa Vyama vya Siasa ..... 21
- B. Usajili wa Wagombea ..... 22

VIII. KAMPENI ZA UCHAGUZI NA MAZINGIRA KABLA YA UCHAGUZI ..... 23

- A. Kampeni za Uchaguzi ..... 23
- B. Matumizi ya Rasilimali za Dola ..... 24
- C. Fedha za Kampeni ..... 24

IX. WAANGALIZI WA UCHAGUZI WA KITAIFA NA KIMATAIFA ..... 25

X. VYOMBO VYA HABARI NA UCHAGUZI ..... 26

- A. Mazingira kwa vyombo vya habari ..... 26
- B. Mfumo wa Kisheria ..... 28
- C. Utangazaji wa Uchaguzi na Uangalizi wa Vyombo vya Habari wa EU EOM ..... 29

XI. USHIRIKI WA WANAWAKE, VIKUNDI VYA WACHACHE NA WATU WENYE ULEMAVU ..... 31

- A. Ushiriki wa Wanawake ..... 31
- B. Ushiriki wa Vikundi vya Wachache ..... 32
- C. Watu wenye Ulemavu ..... 32

XII. UTENDAJI WA HAKI KIUCHAGUZI ..... 32

A. Makosa ya Kiuchaguzi .......... 32
B. Kamati za Maadili .......... 33
C. Malalamiko na Rufaa .......... 33
D. Malalamiko ya Kichaguzi .......... 35
XIII. JAMHURI YA MUUNGANO TANZANIA - SIKU YA UPIGAJI KURA NA KIPINDI .......... 35
A. Upigaji Kura na Kufunga Vituo .......... 35
B. Kuhesabu na Kujumlisha Matokeo .......... 36
C. Matangazo ya Matokeo ya Uchaguzi wa Muungano .......... 38
D. Hali Baada ya Uchaguzi .......... 39
XIV. ZANZIBAR - SIKU YA KUPIGA KURA NA KIPINDI BAADA .......... 40
A. Upigaji Kura na Kufunga Vituo .......... 40
B. Kuhesabu na Kujumlisha Kura .......... 41
C. Kubatilishwa Uchaguzi na Matkmio Baada .......... 42
XV. MAPENDEKEZO .......... 46
Kiambatisho I: Orodha ya Mapendekezo
Kiambatisho II: Matokeo ya Uangalizi wa Vyombo vya Habari wa EU EOM

## I. Muhtasari wa Utendaji

- Tarehe 25 Oktoba 2015, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilifanya uchaguzi wake wa tano tangu kurejeshwa kwa demokrasia ya vyama vingi mwaka 1 992. Kufuatia mualiko toka kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi Zanzibar, Umoja wa Ulaya ulituma Ujumbe wa Waangalizi wa Uchaguzi (EU EOM) ambao ulikuwepo nchini toka tarehe 11 Septemba hadi tarehe 8 Desemba 2015. Ujumbe huo uliongozwa na Muangalizi Mkuu, Judith Sargentini, Mbunge wa Bunge la Ulaya (MEP). Kwa ujumla, EU EOM ilituma waangalizi 141 nchini kote, toka nchi 28 wanachama wa EU, pamoja na Norway, Uswisi na Canada. Wawakilishi toka Bunge la Ulaya, wakiongozwa na Inés Ayala Sender MEP, pia walijiunga na ujumbe kufanya uangalizi siku ya uchaguzi. Jukumu la EU EOM ilikuwa kufanya tathmini ya kina ya mchakato wa uchaguzi, kutokana na uangaizi wake wenyewe, kulingana na ahadi za kimataifa na za kikanda kwa chaguzi za kidemokrasia na sharia za Tanzania.
- Kulikuwa na ushindani mkubwa katika uchaguzi wa 2015 ndani ya Muungano na Zanzibar. Kutokukamilika kwa mchakato wa urekebishwaji wa katiba, kulipelekea kwa vyama vikuu vya upinzani, Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na Civic United Front (CUF), kuunda umoja wa kiuchaguzi, uliojulikana kama Umoja wa Katiba ya Wananchi (Ukawa), (Umoja wa Watetezi wa Katiba ya Wananchi). Katika kumchagua mgombea wake wa urais, Chama Cha Mapinduzi (CCM) kiliingia kwenye mchakato wa uteuzi gawanyishi wa ndani, ambapo waziri wa ujenzi anayeheshimiwa John P. Magufuli alichaguliwa. Kutolewa kwa mgombea aliyeongoza na Waziri Mkuu wa zamani toka CCM Edward N. Lowassa, katika hatua ya mwanzo, kulipelekea kujiunga kwake na Ukawa na uteuzi wake mara moja kama mgombea urais wa ukawa, akigombea rasmi kama mgombea wa CHADEMA. Pamoja na CCM na CHADEMA, vyama vingine sita vya siasa vilikuwa na wagombea wa urais wa jamhuri. Huko Zanzibar, vyama vya siasa 14 viliteua wagombea urais, wakiwemo Rais aliyekuwa madarakani Ali Mohamed Shein wa CCM na Makamu wa Kwanza wa Rais aliyekuwa madarakani Seif Sharif Hamad (Maalim Seif) wa CUF. Kulikuwa na wagombea 1,218 waliyogombea viti 264 vya kuchaguliwa moja kwa moja vya Bunge, pamoja na wagombea 10,879 waliyogombea viti vya Udiwani. Huko Zanzibar, kulikuwa na wagombea 180 kwa ajili ya majimbo 54 ya Baraza la Wawakilishi, pamoja na wagombea 353 kwa ajili ya Halmashauri 111 za Mitaa.
- Tanzania imeridhia hati zote za haki za binadamu za kimataifa na za kikanda zinazohusiana na chaguzi za kidemokrasia. Mfumo wa kisheria ndani ya Muungano na Zanzibar unaruhusu kwa kiasi uendeshwaji wa chaguzi za kidemokrasia kulingana na ahadi za kimataifa na za kikanda zilizoridhiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata hivyo, kuna baadhi ya mapungufu ya kikatiba kuhusu haki za kisiasa na haki ya kujumuika, na, huko Zanzibar, kuhusu haki ya kujiandikisha kama mpiga kura, ambayo hayajafanyiwa kazi toka uchaguzi uliyopita na ambayo hayaendani na kanuni za kimataifa za chaguziza kidemokrasia. Mapungufu hayo ni pamoja na kukatazwa kikatiba kwa wagombea binafsi katika ngazi zote za uchaguzi, ambayo ina kiuka haki ya kushiriki kwa uhuru katika utawala wa nchi, haki yu kujumuika, ambayo inajumlisha haki ya kutojumuika (na chama cha siasa), kutokuweza kupinga matokeo ya uchaguzi wa rais, kutokuwepo kwa njia ya utatuzi wa uteuzi wa ugombea urais uliyokataliwa kinyume cha sheria, kutokuwepo kwa uwezo kisheria kuunda na kusajili umoja wa vyama vya siasa, na, kwa Zanzibar, masharti magumu ya ukazi kwa uandikishwaji mpiga kura.
- Hakuna masharti magumu sana kujiandikisha kama mpiga kura kwa chaguzi za Muungano. Hata hivyo, kwa chaguzi za Zanzibar, sharti la kuwa na kitambulisho cha Zanzibar, pamoja na sharti la ukazi wa miezi 36, na mamlaka tete husika waliopewa *masheha* katika uhakiki wa ukazi katika jimbo husika, yanaonekana kupita kiasi. NEC iliendesha uandikishwaji mpya wa wapiga kura kwa kutumia teknolojia ya bayometriki kwa uchaguzi wa Muungano wa 2015. Jumla ya wapiga kura 22,751,292 waliandikishwa. Kwa uchaguzi wa Zanzibar, ZEC iliendesha zoezi la kusasisha la daftari la kudumu la wapiga kura ambalo lilihusisha wapiga kura 503,860 walioandikishwa. Madaftari yote mawili ya wapiga kura yalitolewa siku

10 kabla ya siku ya uchaguzi, ikiwa ni kabla ya muda wa mwisho kisheria. Kutolewa kwa madaftari hayo mapema zaidi, kungeruhusu uhakiki sahihi na kuongeza imani juu ya madaftari hayo, na kuviwezesha vyama vya siasa kuwa na uelewa zaidi kuhusu wapiga kura wao kwa sababu za kampeni, hasa kwa kuzingatia mabailiko ya hivu karibuni katika mipaka ya majimbo.

- Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) pamoja na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) zilionyesha kujiandaa vya kutosha kwa utendaji wa mchakato wa uchaguzi na uwezo wa kuendesha operesheni muhimu kama vile uchapishwaji wa karatasi za kupigia kura na usambazaji wa nyenzo za uchaguzi. Pamoja na kutokuwa na muundo wa kudumu kwenye ngazi za chini, EUEOM imeona utendaji wake kuwa wenye mpangilio na ulioandaliwa vizuri. Katika utekelezaji wa hatua tofauti za mchakato wa uchaguzi, NEC na ZEC hawakuonyesha uwazi kamili kuhusu taratibu zao za kufanya maamuzi, na fursa ya kukagua shughuli zao haikutolewa wakati wote. Japokuwa NEC iliendelea kutoa taarifa kuhusu maandalizi ya uchaguzi kupitia mikutano ya mara kwa mara na waandishi wa habari, hatua hizi hazikutosheleza kujenga imani miongoni mwa vyama vya siasa kuhusu uwazi wa NEC. Huko Zanzibar, vyama vya siasa kutokupewa taarifa kuhusu daftari la wapiga kura pamoja na mipaka ya majimbo pia iliathiri imani ya vyama vya siasa juu ya ZEC na mchakato wa uchaguzi.
- NEC na ZEC waliendesha zoezi la uwekaji mipaka wa majimbo muda mfupi kabla ya uchaguzi wa 2015. Mipaka mipya haizingatii kanuni ya usawa wa idadi ya wapiga kura katika majimbo, hivyo kushindwa kuhakiki ubora wa upigaji kura. Baadhi ya maeneo yenye watu wengi yana uwakilishi pungufu kwa maana ya viti yakilinganishwa na majimbo yenye idadi ndogo zaidi ya watu. Huko Zanzibar kuchelewa kwa mchakato pamoja na kutokuwepo kwa usahihi wa mipaka mipya, kuliathiri uelewa wa vyama vya siasa juu ya wapiga kura wao kwa ajili ya kampeni, na pia kuathiri wapiga kura katika kutambua majimbo yao.
- NEC ilikuwa na jukumu la kuratibu na kusimamia shughuli zilizoendeshwa na asasi za kiraia pamoja na vikundi vya kijamii ambavyo vilipewa ruhusa kuendesha shughuli za elimu kwa wapiga kura. Pamoja na kushirikiana na vituo 49 vya redio vya maeneo husika ambavyo vilirusha matangazo yenye maelezo juu ya elimu kwa wapiga kura, NEC ilitumia pia mitandao ya kijamii na kuchapisha vitabu vya muongozo kwa ajili ya wapiga kura, vyama vya siasa na pia kijitabu juu ya maswali ya mara kwa mara. Hata hivyo, Waangalizi wa EU waliripoti kwa kiasi kikubwa kutokuwepo kwa shughuli za elimu kwa wapiga kura katika mikoa mingi, hususan maeneo ya vijijini na miongoni mwa jamii za wafugaji kama vile Wamasai. Kutokuwepo kwa elimu kwa wapiga kura isiyofungumana na chama chochote cha siasa, wapiga kura walitegemea vyama vya siasa kwa taarifa za msingi za wapiga kura, hivyo kupunguza fursa ya wapiga kura kufanya maamuzi sahihi. Huko Zanzibar, elimu kwa wapiga kura iliendeshwa kwa matangazo ya mara kwa mara ya ZEC ambayo yalirushwa na vituo vya televisheni na redia vya Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) pamoja na vituo vya redio vya maeneo husika. Japokuwa ZEC ilizipa asasi za kiraia kazi ya kuendesha elimu kwa wapiga kura, shughuli hizo hazikuonekana.
- EU EOM ilifanya unagalizi wa matukio 139 ya kampeni. Katika matukio hayo, wagombea na pamoja na vyama, walifanya kampeni kwa ari kubwa, na kwa kiasi kikubwa waliheshimu taratibu za kampeni, ikiwa ni pamoja na kuepuka matumizi ya lugha chochezi na kuzingatia muda uliyopangwa kwa ajili ya kampeni. Kampeni za uchaguzi zilikuwa kwa kiasi kikubwa tulivu na za amani. Pamoja na hali chanya kwa kiasi kikubwa ya ushindani wa kiuchaguzi Tanzania Bara, mabishano kati ya mashabiki wa vyama vinavyopingana katika baadhi ya maeneo, viliishia kwa vurugu. Japokuwa athari za matukio kama hayo zilikuwa ndogo na katika maeneo husika tu, yaliathiri ubora wa kampeni. Vyama vya siasa pamoja na wagombea waliweza kufanya kampeni kwa uhuru katika maeneo yote ya Tanzania Bara. CCM iliendelea kunufaika na historia yake kama chama tawala. Utumiaji na kunufaika kwa chama hicho kutokana na rasilimali ambazo zamani zilikuwa za dola, kama vile viwanja vya michezo vya umma, ambavyo EUEOM ilishuhudia katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Katavi na Kigoma, vilikipa faida juu ya vyama vingine, na kuchangia kutokuwepo na usawa katika uwanja wa kiuchaguzi. Uzinduzi wa baadhi ya miradi mikubwa

katika wiki za mwisho za kampeni pia uliongeza hali ya kutokutofautisha kati ya dola na chama tawala, na kusisitiza faida ya CCM kikampeni.

- Huko Zanzibar, hali ya mvutano iliyokuwepo kati ya CCM na CUF ilipelekea kampeni kali zaidi na gawanyishi kuliko ilivyoonekana Tanzania Bara. Matamshi makali ya baadhi ya viongozi wa vyama hivyo yalichangia hali ya kutokuwa na uvumilivu ya kampeni, na pia kuongeza hali ya mvutano miongoni mwa jamii. Baadhi ya vyama vya siasa havikuwa na imani juu ya utendaji wa Polisi katika kampeni, na matukio machache ya kutishiwa kwa wapiga kura yaliyochochewa na vyombo vya usalama vilisajiliwa na EUEOM. Hata hivyo, pamoja na matukio haya, na ukali wa ushindani, kampeni huko Zanzibar zilikuwa kwa kiasi za amani.

- Japokuwa uhuru wa kuongea unahakikiwa na Katiba, baadhi ya sheria, ambazo mbili za hivi karibuni ni Sheria ya Takwimu pamoja na Sheria ya Makosa ya Kimtandao, zina vipengele ambavyo vinaweza kutumika kuiwekea mipaka haki hiyo kwa njia za udhalimu, uwezo wa kupata habari na kuwekea mipaka utendaji wa vyombo vya habari. Japokuwa uhuru wa kuongea uliheshimiwa kwa kiasi kikubwa katika juma zilizotangulia kampeni na waandishi wa habari waliweza kufanya kazi kwa kiasi kikubwa katika mazingira ya uhuru, Sheria ya Makosa ya Kimtandao ilionekana kwa wasemaji wa vyombo vya habari kusababisha kujidhibiti usemaji wao wenyewe kupitia. Muda mfupi baada ya uchaguzi, sheria hiyo ilitumiwa pia dhidi ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), ambapo kundi la waangalizi wa ndani, Tanzania Civil Society Consortium on Election Observation (TACCEO), lilikuwa linakusanya na kutathmini taarifa toka kwa waangalizi wao wa uchaguzi, na pia dhidi ya CHADEMA, kuhusiana na shughuli zao za kukusanya na kutathmini taarifa za waangalizi pamoja na fomu za fomu za matokeo ya uchaguzi. Pia, mnamo tarehe 11 Novemba, Tume ya Utangazaji Zanzibar ilisimamisha kibali cha utangazaji cha kituo cha redio kilichopo Visiwani humo, Swahiba FM kwa miezi miwili kwa sababu ya kituo hicho kurusha moja kwa moja mkutano na waandishi wa habari wa mgombea urais wa CUF.

- Vyombo vya habari vya dola vilishindwa kutoa utangazaji sawa na wa haki wa kampeni. Vituo vya televisheni na redio vya Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) pamoja na vituo vya televisheni na redio vya Shirika la Utangazaji Zanzibar vilitoa kwa kiasi kikubwa muda zaidi wa hewani kwa CCM kuliko vyama vingine vya siaisa kwa pamoja. Magazeti ya dola ya *Zanzibar Leo* pamoja na *Daily News* pia yalionyesha upendeleo kwa CCM. Katika matokeo chanya, baadhi ya vyombo vya habari vinavyomilikiwa na watu binafsi vilionyesha kwa kiasi kikubwa uwiano katika utangazaji wa kampeni, hususan TV Azam 2, Radio One na ITV, pamoja na magazeti ya kila siku, *Mwananchi* na *Nipashe.*

- Kwa mara ya kwanza, CCM ilimteua mwanamke kwa nafasi ya makamu wa rais, amabye hapo baadaye alichaguliwa pamoja na mgombea urais wa CCM. Kulikuwa na mwanamke mmoja, aliyeteuliwa na ACT, miongoni mwa wagombea nane wa urais wa Muungano. Japokuwa Katiba zote mbili zinatoa nafasi za viti maalumu kwa ajili ya wanawake ndani ya Bunge pamoja na Baraza la Wawakilishi, wanawake walikuwa na uwakilisho mdogo katika kugombania viti vya kuchaguliwa moja kwa moja ndani ya vyombo hivyo viwili. Kwa upande wa Bunge, wanawake 26 katia ya wagombea 233 walichaguliwa: 18 toka CCM, saba toka CHADEMA na mmoja toka CUF. Waangalizi wa EU waliripoti uwepo mkubwa wa wanawake kwenye mikutano ya kampeni, hasa ile ya CCM, hata hivyo, kukiwa na uwepo mdogo wa wanawake kama wagombea na wazungumzaji kwenye mikutano hiyo. Katika vituo vya kupiga kura vilivyoangaliwa, asilimia 40 ya maafisa wasimamizi na asilimia 51 ya wasaidizi walikuwa wanawake. CCM iliteua asilimia kubwa zaidi ya wanawake kama wakala wa chama wakiwa ni asilimia 31 ya idadi ya jumla, ikifuatiwa na CHADEMA wkiwa na asilimia 16, ACT asilimia 12 na CUF asilimia tisa.

- Katika maimbo yaliyo mengi, Kamati za Maadili ziliundwa na kuonekana na vyama vya siasa kuwa mfumo wenye kufaa katika kutatua migogoro midogo midogo. Hata hivyo, kufaa kwao kama mfumo wa utatuzi wa migogoro wa haraka mara nyingi ulihojiwa na, kwenye baadhi ya maeneo nchini, migogoro iliyohusika na kampeni ilitatuliwa baina ya pande husika pamoja na maafisa uchaguzi pasipo haja ya

kamati hizo kuundwa, au kupitia usuluhishi wa mamlaka zingine kama vile wakuu wa wilaya. Wakati tamko hili lilipoandikwa, kulikuwa na maombi ya uchaguzi 51 yaliowasilishwa Mahakama Kuu ya Muungano.

- Kwa uchaguzi wa Muungano, zoezi la upigaji kura lilionekana na waangalizi wa EU kuwa chanya. Wawakilishi wa vyama vya siasa walikuwepo kwenye takriban vituo vyote vya kupiga kura vilivyoangaliwa. Taratibu za upigaji kura zilifuatwa wakati wote kwenye vituo vya kupiga kura vilivyotembelewa, na kuhakiki usalama wa wa kutosha kuhakiki uhalali wa kura na uwazi wa mchakato. Zoezi la kuhesabu lilianza mara moja baada ya kufunga na liliendeshwa mbele ya mawakala wa vyama vya siasa ambao walipokea nakala za fomu za matokeo. Kulikuwa hata hivyo, na upungufu wa viwango vya uwazi na uaminifu ya mchakato wa ujumlishaji ukilinganisha na ule wa upigaji kura. NEC haikuweza kuhakiki utekelezaji endelevu wa taratibu za ujumlishaji kote mikoani, zenye muongozo unaoeleweka wa jinsi ya kufanya ujumlishaji na jinsi ya kukabiliana na hitilafu za kihesabu kutofikishwa wakati wote kwa wasimamizi wa majimbo. Waangalizi wa EU waliona zoezi la ujumlishaji kwa ujumla kuwa zuri sana au zuri katika asilimia 64 tu ya vituo vilivyoangaliwa. Waangalizi wa kitaifa walikuwepo kwenye asilimia 41 tu ya vituo vilivyotembelewa. Mawakala wa vyama vya siasa wa CCM na CHADEMA walikuwepo kwenye asilimia 80 ya vituo vilivyoangaliwa na mara nyingi waliweza kuhakiki data kabla fomu kufanyiwa kazi kwa njia ya elektroniki.

- Mara tu baada ya siku ya uchaguzi, kuingiliwa kwa ofisi za CHADEMA pamoja na kundi la waangalizi wa kitaifa TACCEO/Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) na polisi, ambapo tathmini ya data za uchaguzi ikiwemo matokeo ilikuwa ikifanyika, na hatimaye kukamatwa kwa wahusika na kuchukuliwa kwa vifaa na nyaraka chini ya kifungo cha 16 cha Sheria ya Makosa ya Mtandao, kulizua maswali juu ya matumizi na utekelezaji wa sheria hiyo. Sheria ya Makosa ya Kimtandao ya 2015 ilikosolewa kwa kiasi kikubwa na vyama vya siasa pamoja na asasi za kiraia kwa kutozingatia kanuni za kimataifa za uhuru wa kuongea, pamoja na mashaka makubwa juu ya utekelezaji wake, hususan kuhusu adhabu zisizo na uwiano na mamlaka makubwa mno waliyopewa polisi kuendesha operesheni za upekuzi na ukamataji. Wakuu wa Balozi za Umoja wa Ulaya, Uswisi, Canada, Norway na Marekani walitoa Tamko la Pamoja la Ndani, tarehe 9 Novemba, ambalo lilielezea mashaka kuhusu matumizi ya Sheria ya Makosa ya Mtandao kwa namna ambayao inaingilia huru za msingi, na kupunguza uwezo wa asasi za kiraia na waangalizi wa ndani kuchukuwa hatua.

- Huko Zanzibar, takriban vituo vyote vya kupiga kura vilivyoangaliwa vilifunguliwa kwa wakati na taratibu za ufunguzi zilifuatwa kwa kiasi kikubwa. Uendeshaji wa upigaji kura ulionekeana kwenda vyema kwenye vituo vya kupiga kura vilivyoangaliwa. Kwa kiasi kikubwa, upigaji kura uliendeswha katika mazingira tulivu, kukiwa na matukio machache ya shughuli za kampeni karibu na vituo vya kupiga kura. Mawakala wa vyama vya siasa walikuwepo kwenye takriban vituo vyote vya kupiga kura vilivyoangaliwa. Kwenye vituo vyote vilivyotembelewa, zoezi la kuhesabu lilianza mara moja baada ya kufunga. Kwenye vituo vya ujumlishaji vilivyoangaliwa na EUEOM, mawakala wa vyama vya siasa wa CCM, CUF, CHADEMA na Alliance for Democratic Change (ADC) walikuwepo wakati wa ukusanyaji wa matokeo. Waangalizi wa kitaifa hawakuwepo. Wasimamizi waliorodhesha matokeo ya uchaguzi na kukabidhi cheti cha uchaguzi kwa wagombea wote waliyochaguliwa kwenye Baraza la Wawakilishi. Wakati wa ujumlisha mkuu wa matokeo ya urais Zanzibar, maafisa wa ZEC na mwakilishi wa kila chama cha siasa kilichokuwa, kwa siku mbili za awali, ambapo baada ya hapo waangalizi hawakuwa tena na fursa ya kuangalia hadi hapo mwenyekiti wa ZEC alipofanya uamuzi kufuta uchaguzi mnamo tarehe 28 Oktoba kinashindania, walikuwepo. Mchakato mkuu wa uorodhoshwaji wa ZEC, ulikuwa wazi kwa kiasi kikubwa.

- Kufuatia mwenyekiti wa ZEC kutangaza kuwa matokeo ya uchaguzi Zanzibar yalikuwa yamefutwa, EU EOM na jumbe za kimataifa za uangalizi za Umoja wa Afrika (AU), Jumuiya ya Ustawi ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) pamoja na Jumuiya ya Madola walitoa tamko la pamoja, ambalo lilielezea mashaka

makubwa juu ya uamuzi wa kufuta matokeo ya uchaguzi Zanzibar. Jumbe hizo ziliiomba ZEC kueleza ni katika vituo gani hasa vya kupiga kura kulikuwa na hitilafu na pia kuisihi ZEC kutenda kwa uwazi kabisa kuhusu uamuzi wake wa kufuta uchaguzi.

- Mara tu baada ya kutangazwa kufutwa kwa matokeo, kulizuka mjadala miongoni mwa asasi za kiraia pamoja na wanasheria kuhusu uhalali wa uamuzi huo na kuheshimiwa kwa taratibu za maamuzi za ZEC. Hata hivyo, tarehe 1 Novemba, ZEC ilifanya kikao na makamishna wote na kuamua, kwa kurejea, kupitisha uamuzi huo wa kufutwa kwa uchaguzi ambao baada ya hapo ulichapishwa kwenye Gazeti la Serikali tarehe 11 Novemba. Iwapo uamuzi huo ulikuwa umepata uhalali kiutaratibu, mamlaka ya kufuta uchaguzi mzima au mchakato mzima wa uchaguzi yalibakia kuwa tete, kwa vile hakuna kipengele cha kisheria kinachoruhusu jambo hili dhairi.

- Tarehe 9 Novemba, CCM na CUF walianza mazungumzo ambayo ilikuwa hatua ya kwanza ya mtiririko wa mikutano tisa baina ya wagombea wawili wakuu wa urais, Ali Mohamed Shein wa CCM (Rais wa Zanzibar) na Seif Sharif Hamad wa CUF (Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar). Mazungumzo yalilenga uhalali kisheria wa uamuzi wa ZEC. Ombi kutoka CUF kumleta mwenyekiti wa ZEC kwenye mikutano lilikataliwa na CCM kwa misingi kuwa hawakuwa na mamlaka ya kumuamrisha mwenyekiti huyo aje. Baada ya mikutano kadhaa, vya vyote viwili vilishikilia misimamo yao ya awali: CCM ikiunga mkono wito wa ZEC wa kurudia uchaguzi, huku CUF ikiwa na msimamo ya kuwa kufutwa kwa matokeo ya uchaguzi kulikuwa kinyume cha sheria na kukataa pendekezo lolote la kurudia uchaguzi, na kudai kurejea zoezi la ujumlishaji na hatimaye kutangazwa kwa matokeo ya urais. EU EOM iliona kuwa matokeo ya mazungumzo katia ya CCM na CUF hayakutolewa kwa umma na kulikuwa pia na jitihada za makusudi kuuzuia umma kupata taarifa hizo. Hali hii ya umma kutokupata taarifa, pamoja na uwepo dhahiri wa jeshi Visiwani humo, kulipelekea sehemu za jamii kuamini kuwa jeshi lilikuwa limechukuwa uendeshaji wa shughuli za serikali hadi hapo suluhisho la kisiasa litakapopatikana.

- EU EOM iliendelea kuwepo nchini hadi tarehe 8 Desemba, ikiendelea kuwa na uwepo huko Zanzibar na pia kufanya mikutano ya mara kwa mara na wadau wakuu Visiwani humo. Pamoja na maombi kadhaa, EU EOM haikufanikiwa kufanya mkutano na mwenyekiti au makamu wa mwenyekiti wa ZEC. Toka uamuzi wa kufuta uchaguzi ufanywe, mwenyekiti wa ZEC hakuweza kupatikana na ZEC, kama taasisi yenye jukumu la utendaji na usimamizi wa mchakato wa uchaguzi, ilitokomea. Hapakuwa na taarifa za ziada kwa umma toka ZEC kuwataarifu wapiga kura kuhusu mchakato wa uchaguzi au kufafanua au kutoa ushahidi wa madai ya hitilafu ambazo zilipelekea kufutwa kwa uchaguzi. EU EOM iliona kuwa ZEC ilionyesha dhahiri kutokuwajibika. Hii ilizidi kudhihirishwa na ukweli kuwa pamoja na kuwa taasisi yenye jukumu la mchakato wa uchaguzi, ZEC haikuhusishwa kwenye mikutano baina ya vyama viwili vikuu vya siasa, ambapo suluhisho zilijadiliwa.

- EU EOM iliona kuwa hadi kuondoka kwake nchini tarehe 8 Desemba, ZEC haikuonyesha uwazi katika uamuzi wake wa kufuta uchaguzi na pia haikuipa EU EOM au mdau mwingine yeyote wa uchaguzi ushahidi wa hitilafu ambazo zilihalalisha kufutwa kwa uchaguzi. Tarehe 8 Desemba, kabla ya kuhamia kwake Ulaya kwa muda, EU EOM ilitoa taarifa kupitia vyombo vya habari ikieleza ya kuwa EU inaendelea kuungano mkono mchakato wa uchaguzi Zanzibar na ujumbe ungerejea tena baada ya makubaliano ya kuanza tena kwa mchakato wa uchaguzi kufikiwa kulingana na uchaguzi shirikishi, wenye uwazi, unaofanywa kwa wakati na wa kuaminika.

- Pamoja ya kuwa mikutano baina ya uongozi wa CCM na CUF huko Zanzibar iliendelea hadi tarehe Januari 2016, hakuna makubaliano yaliyofikiwa kuhusu mgogoro wa uchaguzi Zanzibar. Tarehe 22 Januari, kabla ya uamuzi wowote kusitisha rasmi mikutano kati ya pande hizo mbili, mwenyekiti wa ZEC alitangaza tarehe 20 Machi 2016 kuwa tarehe ya kurudiwa kwa uchaguzi mkuu Zanzibar. Tarehe 28 Januari, CUF ilitangaza rasmi kuwa haitoshiriki marudio ya uchaguzi. Kufuatia matukio haya, tarehe 29 Januari, wakuu wa balozi za Umoja wa Ulaya, nchi wanachama wa Umoja wa Ulaya, Norway, Uswisi,

Canada na Marekani walitoa tamko la pamoja la ndani, ambalo lilisisitiza maoni yao kuwa mgogoro wa kisiasa huko Zanzibar ungeweza kutatuliwa vyema zaidi kupitia suluhisho lililojadiliwa kwa pamoja, na kumsihi Rais Magufuli kuonyesha uongozi, ili kuhakiki matokeo ya amani na uhalali wa mchakato wa uchaguzi.

- Marudio ya uchaguzi Zanzibar yalifanyika tarehe 20 Machi. Vyama tisa vya siasa kati ya 14 vilivyoshiriki uchaguzi wa awali mwezi Oktoba, ikiwemo CUF, vilisusia uchaguzi huo. Pamoja na vyama kuindakia ZEC na kuitaarifu kutokushiriki kwao, ZEC haikuondoa majina ya wagombea waliyosusa wala vyama vyao kwenye karatasi za kupiga kura, wakidai uamuzi unazingatia taratibu. Vyama vya siasa vilivyoshiriki uchaguzi huo wa marudio havikuruhusiwa kufanya kampeni yoyote kabla ya uchaguzi huo. EU EOM haikufanya uangalizi wa uchaguzi wa tarehe 20 Machi kwa kuwa iliona mazingira na muktadha ambapo marudio hayo yalifanyika, hayakuendana na uchauzi shirikishi, halisi na wa kuaminika.

Maboresho ya maswala mengi ya mchakato wa uchaguzi, ikiwa ni pamoja na kupitia upya mifumo ya kisheria ya Muungano nay a Zanzibar, yanahitajika ili kuhakiki haki za msingi za watu na makundi, kama ilivyoainishwa kwenye kanuni za kimataifa na za kikanda za chaguzi za kidemokrasia. Kwa mtazamo huo, mapendekezo muhimu yafuatayo yanawasilishwa ili kufikiriwa na kufanyiwa kazi na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali ya Zanzibar, Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Tume ya Uchaguzi Zanzibar, vyama vya siasa, asasi za kiraia na jumuia ya kimataifa. Mengi ya mapendekezo haya yalikuwemo kwenye Ripoti Kamili ya EU EOM la 2010, na bado ni halali. Majadiliano kuhusu utekelezaji wa mapendekezo muhimu yafuatayo yafikiriwe mapema iwezekanavyo ili kufanyiwa kazi mapungufu yaliyobainika kwenye mchakato wa uchaguzi wa 2015, kwa wakati.Orodha kamili ya mapendekezo inapatikana kwenye Kiambatisho I cha tamko hili.

1. Haki ya kugombea kwenye uchaguzi isiwe kwa wagombea waliyoteuliwa na vyama pekee. Kwa mtazamo huo, hukumu ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (African Court on Human and Peoples' Rights) itekelezwe. Wagombea binafsi wawe na haki ya kugombea kwenye uchaguzi wowote wa Muungano au wa Zanzibar, kama ilivyoainishwa kwenye Makubaliano ya Kimataifa Kuhusu Haki za Kiraia na Kisiasa (International Covenant on Civil and Political Rights) pamoja na Hati ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (African Charter of Human and Peoples' Rights). Utekelewaji wa haki ya wagombea binafsi hauathiri mfumo wa uchaguzi wa Wa-Kwanza-Kupita (First-Past-the-Post) unaotumika kwenye Muungano na pia Zanzibar.

2. Haki ya vyama vya siasa kuunda na kusajili umoja wa kiuchaguzi na kuwa na wagombea wa pamoja inapaswa kuwekwa bayana kisheria, hususan kwa uchaguzi wa urais wa Muungano, ambapo wagombea wawili wanateuliwa kwa tiketi moja kwa nafasi za rais na makamu wa rais.

3. Katiba zote mbili, ya Muungano na ya Zanzibar, kwa sasa hazitoi haki ya kupinga matokeo ya uchaguzi wa rais. Haki ya kulalama matokeo ya uchaguzi wa rais inapaswa kuwepo kisheria kulingana na kanuni za kimataifa za uendeshaji uchaguzi wa kidemokrasia.

4. Matumizi ya baadhi ya vipengele vya Sheria ya Makosa ya Kimtandao yanaweza kupunguza uhuru wa kuongea na kupelekea watu kukamatwa kiholela. Taratibu za matumizi zinapaswa kuwepo ili kuhakiki matumizi sahihi na yanayotabirika ya Sheria hiyo. Watu wanaoshtakiwa kwa makosa chini ya Sheria hii wasikataliwe haki ya kujitetea mahakamani kwani kifungu cha 38 cha Sheria hiyo kinasema kuwa usikilizaji wa utekelezaji utakuwa ni wa upande mmoja na wa faragha.

5. Jitihadi za dhati zinapaswa kufanywa ili kupunguza kuhusika kwa taasisi za utendaji za kiserikali katika uandaaji na utekelezaji wa mchakato wa uchaguzi. Uundwaji wa muundo wa kudumu wa NEC katika ngazi ya mkoa uangaliwe, pamoja na muundo huru usiyo wa kudumu katika ngazi ya jimbo kipindi cha uchaguzi, hivyo kuachana na kutegemea miundo ya kiutendaji ya mitaa. Uteuzi wa

makamishna wa NEC uangaliwe upya ili kuongeza imani juu ya uhuru wa NEC miongoni mwa wadau wote.

6. Kuhusu mchakato wa uandikishwaji wa wapiga kura Zanzibar, sharti la kuwa na kitambulisho cha Zanzibar, pamoja na sharti la ukazi la miezi 36, linapaswa kuangaliwa upya kwa kuzingatia tofauti ya kutendewa baina ya raia wa Tanzania walioandikishwa Bara na wale walioandikishwa Zanzibar. Mamlaka hiari ya *masheha* katika kuhakiki wa ukazi pia yanapaswa kuangaliwa upya ili kuongeza imani juu ya mchakato. Daftari la wapiga kura liwe shirikishi na masharti ya ukazi yafupishwe.
7. Ili kuwataarifu wananchi kwa wakati na kwa ufanisi kuhusu mchakato wa upigaji kura pamoja na chaguzi zao za kiuchaguzi, tume za uchaguzi zifikirie kuchukuwa hatua za kuboresha maandalizi, upangaji wa bajeti pamoja na utekelezaji wa shughuli za elimu kwa wapiga kura. Shughuli zilenge ushirikishi, zikiwa na taarifa mahsusi kwa makundi maalum kama vile vijana na wapiga kura wa mara ya kwanza, wanawake, na watu wenye ulemavu.
8. Maelekezo dhahiri kuhusu ujumlishaji, urushaji na utangazaji wa tarartibu za matokeo yatolewe, hivyo kuepuka tafsiri za hiari za wasimamizi. Mafunzo kwa maafisa wote wa uchaguzi kuhusu taratibu za kuhesabu na kuorodhesha, hususan kujazwa kwa fomu kadhaa na hasa fomu za matokeo, yanaweza kuimarishwa. Maelekezo na vitabu vya taratibu vya kutosha viweze kuwafikia watendaji na wadau wa uchaguzi kabla ya siku ya uchaguzi.
9. Mahakama ziwe na nafasi dhahiri ya usimamizi juu ya utendaji na maamuzi ya tume za uchaguzi. Maamuzi ya NEC na ZEC yawe wazi kuhojiwa mahakamani kwa njia ya uangalizi wa kimahakama mara moja baada ya kipindi cha uteuzi wa wagombea, na pia kipindi cha mchakato mzima. Wanaolalama wasilazmike kusubiri hadi kutangazwa kwa matokeo ili kutafuta msaada wa kupata haki.
10. Mashirika ya utangazaji ya kitaifa, TBC pamoja na ZBC yabadilishwa kuwa mashirika ya utangazaji kwa huduma ya jamii na yenye uhuru kamili toka serikali, wa kiuhariri na kifedha.
11. Muda wa hewani unaotolewa bure kwa ajili ya urushaji matangazo ya kisiasa ya wagombea utolewe kwa njia za haki, kwa misingi ya vigezo wazi na visivyo na upendeleo. Masharti kuhusu muda wa hewani unaotolewa bure yanaweza kuelezewa kikamilifu.
12. Taasisi zinazosimamia vyombo vya habari zifikirie kurekebisha Kanuni ya Huduma za Utangazaji (Maudhui) (Urushaji Matangazo ya Kiuchaguzi ya Vyama vya Siasa) *[Broadcasting Services (Content) (The Political Party Elections Broadcasts) Code]* ili kutoa masharti nafuu zaidi, hususan kwa vyombo vya habari vinavyomilikiwa na watu binafsi. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) iiangalie upya kanuni hiyo kwa namna shirikishi na kwa kuzingatia maoni ya wadau wa vyombo vya habari ambao waliyajaribu masharti yake kwa mara ya kwanza wakati wa uchaguzi huu.

## II. Utangulizi

Kufuatia mualiko toka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi Zanzibar, Ujumbe wa Waangalizi wa Uchaguzi wa Umoja wa Ulaya (EU EOM) ulikuwepo nchini toka tarehe 11 Septemba hadi tarehe 8 Desemba 2015. Ujumbe uliongozwa na Muangalizi Mkuu Judith Sargentini, Mbunge wa Bunge la Ulaya (MEP). Kwa ujumla, EU EOM ilituma nchini kote, waangalizi 141 kutoka nchi Wanachama 28 za EU, pamoja na kutoka Norway, Uswisi na Canada, ili kutathmini mchakato mzima wa uchaguzi kulingana na ahadi za kimataifa na za kikanda juu ya chaguzi za kidemokrasia, pamoja na sheria za Tanzania. Wawakilishi kutoka Bunge la Ulaya, wakiongozwa na Inés Ayala Sender (MEP), pia walijiunga na Ujumbe ili kufanya uangalizi siku ya uchaguzi.

EU EOM iko huru katika matokeo na hitimisho zake na inazingatia Tamko la Kanuni za Uangalizi wa Kimataifa wa Uchaguzi lililoadhimishwa huko Umoja wa Mataifa mwezi Oktoba 2015. Tamko hili la EU EOM linatoa tathmini ya kina kuhusu yaliyobainiwa na Ujumbe katika hatua mbali mbali za mchakato wa uchaguzi, na linahusisha pia mtiririko wa mapendekezo kwa ajili ya uboreshaji wa mchakato kwa chaguzi zijazo, kwa kuzingatia matokeo ya uangalizi huu.

EU EOM inapenda kutoa shukrani zake kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Tume ya Uchaguzi Zanzibar, vyama vya siasa, asasi za kiraia, vyombo vya habari, pamoja na wananchi wa Tanzania kwa ushirikiano wao na msaada wao wakati wa uangalizi. EU EOM inashukuru pia Ubalozi wa Umoja wa Ulaya Tanzania, pamoja na Balozi za Nchi Wanachama wa EU nchini kwa ushirikiano wao kipindi chote.

## III. Historia ya Kisiasa

Tarehe 25 Oktoba 2015, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilifanya uchaguzi wake wa tano wa vyama vingi toka kufutwa kwa mfumo wa chama kimoja mwaka 1992. Tanzania ni taifa lililo na serikali mbili: Serikali ya Muungano, ambayo inatawala Tanzania Bara na kushughulikia Maswala ya Muungano, kama ilivyoainishwa kwenye Katiba, pamoja na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Uchaguzi wa rais, Bunge pamoja na Halmashauri za Mitaa ulifanyika kwa wakati mmoja kwa Muungano na Zanzibar, ambako kuna rais wake, bunge (Baraza la Wawakilishi) na Halmashauri za Mitaa. Rais wa Muungano, Jakaya Kikwete, alimaliza kipindi chake cha pili na cha mwisho madarakani.

Uchaguzi wa 2015 ulikuwa na ushindani mkali kwa upande wa Muungano na pia Zanzibar. Mchakato wa mabadiliko ya katiba ambao haukukamilika, na ambao vya vya upinzani viliona kuwa ulishawishiwa na chama tawala,Chama cha Mapinduzi (CCM), ilipelekea vyama vikuu vya upinzani, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), pamoja na Chama cha Wananchi (CUF), kuunda kwa mara ya kwanza umoja wa kiuchaguzi, uliyojulikana kama Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA). Vyama vya NCCR-Mageuzi pamoja na NLD pia vilishiriki kwenye umoja huo wa UKAWA.

Katika kumteua mgombea wake wa urais, CCM iliingia kwenye mchakato wa uteuzi wa ndani gawanyishi, ambapo waziri anayeheshimika wa ujenzi John P. Magufuli alichaguliwa. Kuenguliwa kwa mgombea aliyeonekana kuongoza na waziri mkuu wa zamani toka CCM Edward N. Lowassa, katika hatua za mwanzo, kulipelekea Lowassa kujiunga na UKAWA na uteuzi wake wa haraka kama mgombea urais wa UKAWA, akigombea rasmi kama mgombea wa CHADEMA. Uamuzi wa Lowassa ulipelekea pia kuhama kwa wana CCM wengine kwenda UKAWA, ikiwa ni pamoja na waziri mkuu mwingine wa zamani na wanasiasa wengine waandamizi. Pamoja na CCM na CHADEMA, vyama vingine sita vya siasa vilisimamisha wagombea wa urais wa jamhuri.

Kwa uchaguzi wa Bunge, CCM ilikuwa chama pekee kugombania viti vyote. Vyama vya UKAWA vilikubali kuteua mgombea mmoja kwa kila jimbo la ubunge, lakini tofauti baina ya wanachama wa umoja huo zilipelekea wagombea wao kushindana kwa baadhi ya viti.

Huko Zanzibar, wahusika wawili wakuu wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (GNU), Rais Ali Mohamed Shein wa CCM na Makamu wa Kwanza wa Rais Seif Sharif Hamad (Maalim Seif) wa CUF, pamoja na wogombea wengine 12 waligombea urais.

Tarehe 29 Oktoba, NEC ilitangaza matokeo ya uchaguzi wa rais ya Muungano, ambapo Magufuli alipata asilimia 58.46 ya kura na Lowassa asilimia 39.97. Lowassa pamoja na UKAWA waliyakataa matokeo rasmi, wakidai kulikuwa na hitilafu kubwa na na hila katika uchaguzi, pamoja na kuingiliwa kwa mifumo ya kitaalamu ya NEC, na watendaji wanaohusika na serikali. Hata hivyo, kutokuwepo kwa njia za kisheria kupinga matokeo hayo, na huku NEC ikitupilia mbali malalamiko ya UKAWA, Magufuli alithibitishwa kuwa

mshindi wa urais tarehe 30 Oktoba na kuapishwa tarehe 5 Novemba. Hadi tamko hili lilivyoandikwa, mgogoro wa kisiasa uliyosababishwa na kufutwa kwa uchaguzi Zanzibar kupitia Tume ya Uchaguzi Zanzibar tarehe 28 Oktoba, ulikuwa bado haujatatuliwa na Rais Shein ameendelea kubaki madarakani. Hata hivyo, uhalali wake wa kubaki madarakani umeendelea kupingwa na CUF pamoja wadau wa sheria.

## IV. Mfumo wa Kisheria

### *A. Kanuni na Ahadi za Kimataifa na Kikanda*

Tanzania imeridhia hati zote kuu za kimataifa na za kikanda za haki za binadamu zinazohusiana na chaguzi za kidemokrasia. Hii ni pamoja na Agano la Kimataifa Juu ya Haki za Kiraia na za Kisiasa la 1966 (1966 International Covenant on Civil and Political Rights - ICCPR), Mapatano ya Kukomesha Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake ya 9179 (1979 Convention on the Elimination of All Forms of Discrimination against Women - CEDAW) pamoja na Itifaki Mbadala ya Mapatano hayo, Mapatano ya Kukomesha Aina Zote za Ubaguzi wa Rangi ya 1966 (1966 International Convention on the Elimination of All Forms of Racial Discrimination - ICERD), Mapatano Kuhusu Haki za Watu Wenye Ulemavu ya 2006 (2006 Convention on the Rights of Persons with Disabilities - CRPD) pamoja na Mapatano ya Haki za Kisiasa za Wanawake ya 1952 (1952 Convention of the Political Rights of Women - CPRW). Kama mwanachama wa Umoja wa Mataifa (UN), Umoja wa Afrika (AU), Jumuiya ya Madola, ), Jumuiya ya Ustawi ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) pamoja na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Tanzania inawajibika kuzingatia Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa la 1948 (1948 UN Universal Declaration of Human Rights), Hati ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ya 1981 (1981 African Charter of Human and Peoples' Rights (ACHPR), Tamko la Umoja wa Afrika la Kanuni Zinazosimamia Chaguzi za Kidemokrasia Afrika la 2002 (2002 AU Declaration of Principles Governing Democratic Elections in Africa), Kanuni na Miongozo ya SADC Inayosimamia Chaguzi za Kidemokrasia iliyoridhiwa mwaka 2015 pamoja na Itifaki ya Utawala Bora ya EAC.

### *B. Utungaji Sheria za Kitaifa za Uchaguzi*

Mfumo wa kisheria uliyosimamia uchaguzi mkuu wa 2015 kwenye Jamhuri ya Muungano pamoja na Zanzibar kwa kiasi kikubwa haujabadilika toka uchaguzi mkuu uliyopita. Uchaguzi wa rais na wabunge wa Muungano unasimamiwa na hati kadhaa ikiwa ni pamoja na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977, Sheria ya Uchaguzi ya Taifa ya 1985, Sheria ya (Uchaguzi) ya Halmashauri za Mitaa ya 1979, Sheria ya Vyama vya Siasa ya 1992 pamoja na Sheria ya Matumizi ya Fedha Katika Uchaguzi ya 2010. Maelezo husika kuhusu makosa ya kiuchaguzi yanapatikana pia kwenye Kanuni ya Adhabu. NEC ilitoa taratibu kadhaa kwa ajili ya mchakato wa uchaguzi wa 2015 ambazo zilihusisha Kanuni za Kitaifa za Uchaguzi (Uchaguzi wa Rais na Wabunge), Kanuni za Halmashauri za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani), Kanuni za Maadilii za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, pamoja na Miongozo kwa Waangalizi wa Ndani na wa Kimataifa.

Mfumo wa kisheria Zanzibar unahusisha Katiba ya Zanzibar ya 1984, Sheria ya Uchaguzi Namba 11 ya 1984, Sheria ya Vyama vya Siasa Namba 5 ya 1992, Sheria ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar Namba 7 ya 2005, Sheria ya Uandikishwaji Ukazi wa Wazanzibari Namba 7 ya 2005 pamoja na Sheria ya Uzanzibari Namba 5 ya 1985. Kanuni za ZEC ni pamoja na Kanuni za ZEC za 2015, Kanuni za ZEC za Ukaguzi wa Daftari la Wapiga Kura za 2010, Miongozo na Kanuni za Maadili kwa Vyama vya Siasa kwa Uchaguzi wa 2015, na Miongozo Kanuni za za Maadili kwa Waangalizi wa Ndani na wa Kimataifa ya 2015.

Mfumo wa kisheria ndani ya Muungano pamoja na Zanzibar unaruhusu kwa kiasi cha kukubalika msingi wa uendeshwaji wa uchaguzi wa kidemokrasia kulingana na ahadi za kimataifa na za kikanda zilizoridhiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katiba zote mbili pamoja na sharia husika za kiuchaguzi zinahakiki haki za kisiasa na uhuru wa msingi pamoja na haki ya kupata kutendewa haki pamoja na suluhisho za kisheria kulingana na ahadi za kimataifa na za kikanda. Hata hivyo, kuna baadhi ya vikwazo vya kikatiba juu ya haki za

kisiasa pamoja na uhuru wa kujumuika, na, huko Zanzibar, kuhusu haki ya kuandikishwa kama mpiga kura, ambavyo havijafanyiwa kazi toka uchaguzi uliyopita na ambavyo haviendani na kanuni za kimataifa za chaguzi za kidemokrasia. Hivi ni pamoja na kutoruhusiwa kwa wagombea binafsi katika ngazi zote za uchaguzi ambayo ni kinyume na haki ya kushiriki kwa uhuru katika utawala wan chi, uhuru wa kujumuika, ikiwa ni pamoja na uhuru wa kutojumuika (na chama cha siasa), kutokuweza kupinga matokeo ya urais, kutokuwepo kwa njia ya utatuzi kwa uteuzi wa mgombea urais uliyokataliwa kinyume cha sheria, kutokuwepo na mifumo ya kisheria ya kuunda na kusajili umoja wa vyama vya siasa, na, kwa Zanzibar, masharti magumu ya ukazi kwa ajili ya uandikishaji mpiga kura. Pia, haki ya kukata rufaa kwa wakati dhidi ya maamuzi ya NEC au ZEC ya kukataa uteuzi wa mgombea ubunge haihakikiwi kwa kuwa rufaa za kukataliwa kwa uteuzi zinaweza tu kw=uwasilishwa baada ya kutangazwa matokeo. Tofauti kati ya mfumo wa kisheria wa Tanzania na ahadi zake za kimataifa zinaweza tu kufanyiwa kazi kupiti kurekebishwa kwa Katiba zote mbili, ya Jamhuri ya Muungano pamoja na ya Zanzibar.

### *C. Mfumo wa Uchaguzi*

Kwa uchaguzi wa rais wa Muungano, vyama vya siasa vinapaswa kuwasilisha wagombea wawili kwa wakati mmoja, mmoja kwa nafasi ya rais na mwingine kwa nafasi ya makamu wa rais. Kidesturi, ikiwa mgombea urais anatokea Bara ya Jamhuri ya Muungano, mgombea mwenza anatokea Zanzibar, na kinyume chake. Serikali ya Umoja wa Kitaifa, kulingana na mabadiliko ya Katiba ya Zanzibar ya Agosti 2010, iliundwa baada ya uchaguzi mkuu wa Oktoba 2010, huku chama kilichoshika nafasi ya pili kikimteua makamu wa kwanza wa rais kuongoza pamoja na rais aliyechaguliwa. Mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, ambao umeainishwa kwenye Katiba ya Zanzibar, utaendelea kuwepo baada ya uchaguzi wa 2015.

Marais wote wawili, wa Jamhuri ya Muungano na wa Zanzibar, wanachaguliwa kwa muda wa miaka mitano katika uchaguzi wa duru moja kwa kupata idadi kubwa zaidi ya kura zilizopigwa. Katiba inamruhusu rais kukaa madarakani kwa duru si zaidi ya mbili. Mfumo wa wa-kwanza-kupita pia unatumika katika uchaguzi wa Bunge la Muungano pamoja na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

Bunge lina viti 264 vya kuchaguliwa moja kwa moja (214 kwa Bara na 50 kwa Zanzibar), ikiwo ni ongezeko la majimbo 26 toka uchaguzi wa 2010. Rais wa Jamhuri pia anateua wabunge 10 na wabunge wawili kutokana na nyadhifa zao *(ex officio)*. Viti vingine vitano vinapewa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Hatimaye, Bunge pia lina viti vya kutochaguliwa moja kwa moja ambavyo vinavyohifadhiwa kwa ajili ya wanawake, na ambavyo ni sawa na asilimia 40 ya jumla ya viti vya Bunge vya kuchaguliwa moja kwa moja pamoja na vya kuteuliwa, toka mwaka 2010. Viti hivi vilivyohifadhiwa vinagawiwa kwa mfumo wa uwiano wa uwakilishi kulingana na asilimia ya kura ilizozipata kila chama katika uchaguzi wa Bunge. Orodha ya wagombea wanawake kwa viti hivi ndani ya Bunge pamoja na Baraza la Wawakilishi, hazikutolewa kwa umma na NEC au ZEC kabla ya uchaguzi.

Pamoja na uchaguzi wa rais na wabunge wa Muungano, wapiga kura wa Zanzibar walifanya uchaguwa rais wa Zanzibar, viti 54 vya kuchaguliwa moja kwa moja vya Baraza la Wawakilishi, pamoja na Madiwani 111. Jumla ya viti 22, ikiwa pia ni asilimia 40, vinahifadhiwa kwa ajili ya wanawake kwa njia uwakilishi wa uwiano kwenye Baraza la Wawakilishi. Rais wa Zanzibar anateua wajumbe 10 wa Baraza la Wawakilishi, ambapo wawili kati yao wanateuliwa na rais kwa mashauriano na kiongozi wa upinzani.

## V. Utendaji wa Uchaguzi

### *A. Muundo na Mpangilio*

***Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC)***

Katiba inaunda Tume ya Tafa ya Uchaguzi (NEC), ikiwa na makamishna saba waliyoteuliwa na rais wa Muungano kwa kipindi cha miaka mitano. Mwenyekiti pamoja makamu wa mwenyekiti shurti wawe majaji

ama wa Mahakama ya Rufaa au Mahakama Kuu. Ikiwa mwenyekiti anatokea Bara, makamu wake atatokea Zanzibar, na kinyume chake. Mwenyekiti wa sasa aliteuliwa mwaka 2011 naye ni jaji mstaafu wa Mahakama ya Rufaa. Kwa makamishna wengine watano, mmoja anachaguliwa toka Tanganyika Law Society, na makamishna wengine wane wanapaswa kuwa na uzoefu wa uendeshaji na usimamizi wa uchaguzi au sifa zingine ambazo rais anaona ni muhimu katika utekelezaji wa kazi zao husika. Rais anaweza kumuondoa kamishna kwa kushindwa kufanya kazi zake kwa sababu ya ugonjwa, kwenda kinyume na miiko ya kazi au kupoteza sifa muhimu. NEC hutoa kanuni, miongozo na taarifa na maamuzi yake hufanywa kwa kura ya waliyo wengi, pamoja na akidi ya wajumbe wane akiwemo mwenyekiti.

Akiwa ameteuliwa na rais miongoni mwa watumishi waandamizi wa umma na kwa kupendekezwa na Tume, Afisa Mtendaji Mkuu wa NEC ndiye mkurugenzi wa uchaguzi ambaye pia nia katibu wa Tume. Sekretarieti, iliyo na idara kadhaa maalumu, inaundwa kenye ngazi ya kitaifa tu na hufanya kazi katika ngazi za chini nyakati za uchaguzi kupitia uteuzi wa maafisa wa serikali.

Katiba inaipa NEC uhuru kama taasisi.[1] Hata hivyo, kwenye ngazi za chini NEC inaendelea kuwa tegemezi kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa miundombinu pamoja na wafanyakazi wake na pia katika kutengewa bajeti. Tume inateua maafisa uchaguzi kadhaa kimkoa miongoni mwa watendaji wa mikoa ama wilaya pamoja na maafisa wa serikali za mitaa ambao wako chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. NEC pia inategemea wakurugenzi wa majiji na miji, na wakurugenzi watendaji wa wilaya kufanya kazi za wasimamizi. Utegemezi huu, ambao ulishaonwa na EU EOM 2010, unaathiri mtazamo wa wadau kuhusu kutokuwa na upendeleo au kufungamana na upande wowote kwa Tume. NEC iliajiri waratibu 30 wa uchaguzi, wasimamizi wakuu 972 pamoja na wasimamizi 7914 katika kipindi cha uchaguzi.

***Tume ya Uchaguzi Zanzibar***

Katiba inaitaka ZEC kuwa tume huru isiyoingiliwa na serikali wala vyama vya siasa. Mamlaka ya ZEC ni pamoja na usimamizi wa jumla wa uchaguzi wa rais, Baraza la Wawakilishi na Halmashauri za Mitaa Zanzibar. Wajumbe saba wa ZEC wanateuliwa na rais wa Zanzibar. Mwenyekiti wa ZEC anateuliwa na rais, wajumbe wawili wanateuliwa kwa mapendekezo ya kiongozi wa shughuli za serikali, wakati wajumbe wengine wawili wanateuliwa kwa mapendekezo ya mkuu wa upinzani kwenye Baraza la Wawakilishi. Mmoja kati ya wanaoteuliwa na rais shurti awe jaji wa Mahakama Kuu, na uteuzi mmoja ni kwa busara ya rais. Rais anaweza tu kumuondoa mjumbe wa ZEC kwa mjumbe huyo kushindwa kufanya kazi zake. Rais anamteua mkurugenzi wa uchaguzi wa ZEC kutokana na mapendekezo ya ZEC. Kwa wadau, mifumo hii ya uteuzi inaonekana kushindwa kuhakiki uhuru wa ZEC kulingana na misingi ya kikatiba na kanuni za kimataifa.[2]

Tume ya sasa yenye wajumbe saba iliteuliwa na rais wa Zanzibar mwaka 2013 na haikuwa na wanawake. Makamishna wote, ikiwa ni pamoja na mwenyekiti, walikuwa ni wapya isipokuwa wajumbe wawili waliyopendekezwa na upinzania. Zanzibar iliongeza idadi ya wilaya za kiutendaji toka kumi hadi kumi na moja, hivyo kwa uchaguzi wa 2015, ZEC ilikuwa na ofisi za wilaya za kudumu kumi na moja - saba zikiwa Unguja nan ne Pemba.

*B. Utendaji wa Uchaguzi*

Uendeshaji wa uchaguzi wa rais, Bunge na Halmashauri za Mitaa Tanzania Bara ni jukumu la NEC. Kwa Zanzibar, NEC na ZEC zinasimamia, kila mmoja kwa upande wake, chaguzi za Muungano na zile za Zanzibar. ZEC inajukumu la kuendesha chaguzi tatu za Zanzibarv – urais, Baraza la Wawakilishi na Halmashauri za

[1] Ibara ya 25 ya ICCPR, Tume ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa, Maoni ya Jumla Na. 25, aya 20: "Mamlaka huru ya uchaguzi iundwe kusimamia mchakato wa uchaguzi ili kuhakiki kuwa unaendeshwa kwa haki, bila upendeleo na kulingana na sheria zilizopo ambazo zinaendana na Agano."

[2] Ibara ya 25 ya ICCPR, Tume ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa, Maoni ya Jumla Na. 25, aya 20: "Mamlaka huru ya uchaguzi iundwe kusimamia mchakato wa uchaguzi ili kuhakiki kuwa unaendeshwa kwa haki, bila upendeleo na kulingana na sheria zilizopo ambazo zinaendana na Agano."

Mitaa – wakati NEC inawajibika kwa chaguzii mbili za Muungano visiwani – urais na Bunge la Muungano. Pamoja na kuwa siku ya kupiga kura tume zote mbili ziliendesha shughuli zake kwenye vituo hivyo hivyo, vitendea kazi na rasilimali watu zilikuwa tofauti.

Tume ya Taifa Uchaguzi (NEC) na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) zote zilionyesha viwango vya kuridhisha vya utayari wa kuendesha chaguzi na uwezo kwenye maeneo makuu ya utendaji kama vile kuchapisha karatasi za kupigia kura na usambazaji wa vifaa vya kupigia kura. Pamoja na kutokuwepo kwa mfumo wa kudumu wa NEC kwenye ngazi za chini, tathmini ya EU EOM juu ya utendaji wake ilikuwa ni kwamba utendaji huo ulikuwa ni wa mpangilio na wenye maandalizi ya kutosha. Waangalizi wa EU waliripoti kuwa, kwenye mikoa mingi Tanzania Bara, kulifanyika mikutano kati ya wasimamizi wa uchaguzi na vyama vya siasa mara kwa mara. Ndani ya ZEC, hakukuwa na mawasiliano ya kutosha kati ya ZEC na watendaji wa wilaya, hasa kwa Pemba, ambao mara nyingi walikuwa hawana maelezo kuhusu hali ya maandalizi ya uchaguzi. Tanzania Bara, mawasiliano kati ya NEC na watendaji wake wa ngazi za chini yalionekana kuwa bora zaidi. Huko Zanzibar, uratibu baina ya watendaji wa ZEC na NEC ulionekana kuwa mdogo, lakini pande zote mbili ziliheshimu ratiba zao.

Vyama vya siasa vilikuwa na mitazamo tofauti juu ya uhuru na uwazi wa NEC na ZEC. Wakati wawakilishi wa CCM waliamini utendaji na uwezo wa vyombo vya usimamizi wa uchaguzi, vyama vya upinzani vilishuku kutofungamana kwa wasimamizi wa uchaguzi kwa sababu ya mchakato wa uteuzi wao.[3] Wasiwasi ulielezwa juu ya tuhuma za kuwepo kwa upendeleo kwa wasimamizi wa uchaguzi kwenye baadhi ya wilaya Tanzania Bara, hasa pale ambapo malalamiko hayakupatiwa suluhisho. Baadhi ya watendaji wa ngazi za juu wa NEC walibadilishwa karibu na siku ya kupiga kura, wakiwemo aliyekuwa mkurugenzi wa uchaguzi na wakurugenzi wa idara za sheria, elimu ya wapiga kura, maelezo na utawala.[4] Mabadiliko haya pamoja na uteuzi wa mkamishna wawili mwezi mmoja tu kabla ya siku ya kupiga kura yalileta wasiwasi kwa wajadilianaji. Katika kipindi kuelekea siku ya uchaguzi, NEC mara kadhaa ilikana tuhuma kuwa Usalama wa Taifa (TISS) ilikuwa imeweka watu wake kwenye kituo cha NEC. Pamoja na maombi ya mara kwa mara, ombi la kutembelea kituo hicho halikukubaliwa. Huko Zanzibar, wawakilishi wa CCM walifurahia utendaji wa kitaalamu wa ZEC hadi muda mfupi baada ya siku ya uchaguzi, huku wawakilishi wa CUF wakiona kuwa ZEC haikuwa huru na ilikuwa ikiipendelea CCM.

Katika hatua zote za mchakato wa uchaguzi, NEC na ZEC hazikutoa uwazi kamili juu ya maamuzi yao, na uwezo wa wadau kufuatilia muenendo wa shughuli za tume haukuwepo wakati wote. Kwa upande wa uchaguzi wa Muungano, karatasi za uchaguzi, zilizochapishwa Afrika Kusini, ziliwasili tarehe 12 Oktoba. Usambazaji ulianza siku iliyofuata kwenda maeneo yote nchini. Kwa mujibu wa vyama vya siasa, havikukaribishwa kuhudhuria kuona kuwasili kwa nyaraka hizo nyeti. NEC ilisita kutoa taarifa hizi kwa sababu za usalama. Lakini, wadau wote, ikiwa ni pamoja na EU EOM, walialikwa kushuhudia kuwasili kwa karatasi za kupigia kura za uchaguzi wa Zanzibar.

Matatizo yaliyojitokeza katika kukamilisha madaftari ya wapiga kura na kuchorwa upya mipaka upande wa Tanzania Bara na Zanzibar, pamoja na maelezo ya Mfumo wa Kusimamia Matokeo (RMS), kwa uchaguzi wa Muungano, hayakuelezewa kikamilifu kwa vyama na kwa wananchi. Pamoja na kuwa NEC ilitoa maelezo ya RMS kwa vyama vya siasa, haikuweza kuondoa wasiwasi ulioelezwa na baadhi ya vyama vya siasa juu ya maswala ya kiufundi na programu za kompyuta zilizotumika kurusha matokeo. Vyama vya UKAWA havikuridhika na maelezo waliyopewa juu ya RMS, na waliomba kufanyike uhakiki wa kiufundi wa programu

[3] Ibara 2, Kifungu 4 (e) cha Tamko la Umoja wa Afrika Juu ya Kanuni Zinazosimamia Chaguzi za Kidemokrasia Afrika, 2002: "Chaguzi za kidemokrasia zifanywe […] na taasisi za kiuchaguzi zisizofungamana na upande wowote, shirikishi, zenye uwezo kiutendaji na zinazowajibika, zenye wafanyakazi waliyopata mafunzo stahili, zikiwa na utaratibu wa ugavi na usafirishaji wa kutosha." Kanuni na Miongozo ya SADC Inayosimamia Chaguzi za Kidemokrasia za 2015, Fungu 5.1.3: "Weka Taasisi za Uangalizi wa Uchaguzi zisizofungamana na upande wowote, zenye weledi, zilizo huru, shirikishi, zenye uwezo kiutendaji na zinazowajibika, zikiwa na makamishna mashuhuri, wasiyofungamana na chama chochote, na wafanyakazi wa uwezo kiutendaji".

[4] EU EOM haikupewa maelezo ya yababu za mabadiliko haya.

ya RMS pamoja na taarifa za matumizi ya programu hiyo kwenye chaguzi nyingine. NEC ilikataa kufanya uhakiki wa kiufundi. NEC ilitoa taarifa za maendeleo ya maandalizi ya uchaguzi kupitia taarifa za mara kwa mara kwa vyombo vya habari. Hata hivyo, hatua hizo hazikutosha kujenga imani miongoni mwa vyama vya siasa juu ya uwazi wa NEC.

Uhaba wa taarifa zilizotolewa kwa vyama vya siasa juu ya daftari la wapiga kura na mipaka ya majimbo pia iliathiri imani juu ya ZEC na mchakato wa uchaguzi katika kipindi kuelekea siku ya kupiga kura. ZEC ilifanya mkutano na wadau wote tarehe 11 Oktoba kuwataarifu juu ya maandalizi ya uchaguzi. Maswala kadhaa yalielezwa na vyama vya siasa, ikiwa ni pamoja na taarifa zilizochelewa na ambazo hazikueleweka kirahisi za mipaka ya majimbo ya Baraza la wawakilishi, ukusanyaji wa kadi za uandikishaji wapiga kura, usalama wa nyaraka nyeti za uchaguzi, uhakiki wa utambulisho wa wapiga kura kwenye vituo vya kupigia kura, upigaji kura wa wafanyakazi wa vyombo vya usalama na ratiba ya utangazaji wa matokeo ya uchaguzi wa rais. ZEC ilichelewa sana kutoa nakala za ramani za majimbo, jambo ambalo liliathiri uwezo wa vyama vya siasa kutambua wapiga kura wao kwa madhumuni ya kufanya kampeni, haswa kuwa kuzingatia mabadiliko ya mipaka ya majimbo na watendaji wa mitaa *(shehia).*

*C. Uwekaji Mipaka ya Majimbo*

Zoezi la kuchora upya mipaka ya majimbo lililofanyika na NEC na ZEC muda mfupi kabla ya uchaguzi wa 2105 halikuzingatia msingi wa usawa wa mgawanyiko wa wapiga kura katika majimbo, na hivyo kushindwa kuhakikisha usawa wa kura zilizopigwa.[5]

NEC ilitangaza kuanza zoezi la kuchora upya mipaka ya majimbo tarehe 28 Aprili 2015, miezi sita kabla ya siku ya uchaguzi.[6] Katika kuchora mipaka, NEC inapaswa kuhakiki idadi ya wapiga kura halali katika majimbo inakaribia kulingana kwa kuangalia vigezo vya idadi ya watu, mifumo ya mawasiliano, hali ya kiuchumi ya jimbo na eneo lake. Jumla, halmashauri za mitaa 37 ziliomba kupewa hadhi ya jimbo na maombi 41 ya majimbo mapya yalipopkelewa. Baada ya tathmini ya NEC, maombi 36 yalikidhi vigezo, na kati ya hayo 21 yaliendana na vigezo vya mipaka kiutawala na 15 yalikidhi vigezo vya idadi ya watu.[7] Mabadiliko yaliyofanyika kwenye mipaka, kwenye idadi ya majimbo na/au wabunge wanaowakilisha majimbo hayo, yalipitishwa kwa uchaguzi mkuu wa 2015.

Baadhi ya maeneo yenye idadi kubwa ya watu yana uwakilishi mdogo Bungeni kulingana na majimbo mengine yenye watu wachache zaidi. Kuna majimbo ambapo uzito wa kura ni mara 15 zaidi ya jimbo linguine. Hili limejitokeza Madaba mkoani Ruvuma, iliyo na wapiga kura walioandikishwa 27,502 ikilinganishwa na wapiga kura 417,612 walioandikishwa Temeke mkoani Dar es Salaam. Kuna si chini ya majimbo 10 ambayo yana wapiga kura wasiyofika 50,000 walioandikishwa na majimbo saba yenye zaidi ya wapiga kura 200,000 walioandikishwa. Wastani wa taifa wa idadi ya wapiga kura kwa jimbo kwenye uchaguzi mkuu ilikuwa 85,853. Kamati ya Uangalizi wa Uchaguzi Tanzania (Tanzania Election Monitoring Committee - TEMCO), kwenye taarifa yake ya awali juu ya uchaguzi wa 2015, ilisema kuwa zoezi la uchoraji mipaka ya majimbo "lilifanyika ipasavyo, kwa kutumia taratibu zilizo wazi, zinazoeleweka na kuendana na taratibu, kama inavyoainishwawa kisheria." Matokeo ya utafiti wa TEMCO haukuona ishara zozote za hila katika upangaji wa mipaka ya majimbo ungeweza kusababisha kuchezewa kwa matokeo ya uchaguzi.

[5] Kifungu 25 cha Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Raia na Siasa (ICCPR), Tume ya Haki za Binadamy ya Umoja wa Mataifa, Maelezo na. 25, ibara 21: "… ndani ya fumo wa uchaguzi wa kila nchi, kura mpiga kura mmoja iwe sawa na kura ya mwingine. Uchoraji wa mipaka na njia inayotumika kugawa kura isilete athari kwa mgawanyiko wa wapiga kura na isibague dhidi ya kundi lolote."

[6] Ripoti yamwisho iliyotolewa Julai 2015 iliorodhesha majimbo mapya. Kwenye uchaguzi wa 2010, NEC ilishaongeza idadi ya majimbo kutoka 232 hadi 239.

[7] Ripoti iliyotolewa na NEC inaongelea majimbo mapya 26, hivyomkuongeza idadi kufikia 265. Tume baadae ikaongelea jumla ya majimbo 264. Mikoa iliyokuwa na majimbo mapya ni: Morogoro, Dodoma, Tanga, Geita na Arusha ikiwa na jimbo moja jipya kila mkoa; Dar es Salaam, Shinyanag, Ruvuma, Njombe, Mbeya na Katavi ikiwa na majimbo mapya mawili kila mkoa na Mara, Mtwara na Tabora ikiwa na majimbo mapya matatu kila mkoa.

Tarehe 7 Agosti, ZEC ilitangaza ongezeko la majimbo Zanzibar kutoka 50 hadi 54 kwa Baraza la Wawakilishi. Mchakato wa kupanga majimbo ulikamilika wiki chache tu kabla ya siku ya uchaguzi. Ripoti ya ZEC ya upangaji mipaka ya majimbo haikutangazwa kabla ya uchaguzi. Zaidi ya hilo, waziri mwenye dhamana ya serikali za mitaa kabla ya hapo aliongeza idadi ya *shehia* na kupunguza idadi ya kata mwezi Mei 2015.[8] Mchakato huo ambao haukuwa wazi na uliochelewa, pamoja na kutokujulikana kwa uhakika mipaka mipya, iliathiri vyama vya siasa kwenye ufahamu wa wapiga kura wao kwa ajili ya kufanya kampeni, na iliathiri pia ufahamu wa wapiga kura juu ya majimbo yao.

Daftari lililoboreshwa la wapiga kura la Zanzibar lilikuwa na wapiga kura 358,773 kwa Unguja na 145,087 kwa Pemba. Majimbo 18 ya Pemba yalikuwa na wastani ya wapiga kura 8,060. Kwa Unguja, kila kiti kati ya viti vyote 36 kiliwakilisha wastani ya wapiga kura 9,966. Ingawaje zoezi la uwekaji mipaka majimbo la 2015 lilizaa majimbo mapya manne Unguja, wapiga kura wa Pemba walibaki kuwa uwakilishi wa ziada kwa viti viwili kwenye Baraza la Wawakilishi. Tofauti zaidi zilionekana kwenye usawa wa kura Unguja. Jimbo lililokuwa na idadi kubwa kabisa ya wapiga kura lilikuwa ni jimbo la Uzini likiwa na wapiga kura 15,069, wakati jimbo lenye idadi ndogo kabisa lilikuwa Fuoni lililokuwa na wapiga kura 1,923 tu. Hii ilimaanisha kuwa kura moja Fuoni ilikuwa na uzito mara 7.8 zaidi ya kura ya Uzini.[9]

Suluhisho la NEC kwa ongezeko la majimbo ya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar kutoka 50 hadi 54 ilikuwa kugawa majimbo manne ya Bunge la Muungano kati ya majimbo nane ya Baraza la Wawakilishi. Mbali na majimbo hayo nane, majimbo 46 yaliyobaki ya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar yanafanana kabisa na yale ya Bunge la Muungano. Hii inaleta kutolingana kwa kura za viti vya Bunge la Muungano. Kwenye jimbo la Fuoni, wapiga kura 1,923 walioandikishwa walimchagua mbunge mmoja wa Bunge la Muungano, wakati Bububu, wapiga kura 22,947 walioandikishwa pia walimchagua mbunge mmoja.

Kwenye ngazi ya Muungano, Zanzibar kihistoria imekuwa na uwakilishi mkubwa zaidi kuolingana na idadi ya watu. Wakati wapiga kura wa Zanzibar ni asili mia mbili tu ya idadi ya wapiga kura wa Jamhuri ya Muungano, wapiga kura wa Zanzibar walichagua wabunge 50 wa Bunge la Muungano. Wabunge wengine watano wa Bunge la Muungano waliotoka Zanzibar ni wabunge wanaoteuliwa na Baraza la Wawakilishi.

### *D. Elimu kwa Wapipga Kura.*

NEC ilipewa jukumu la kuratibu na kusimamia shughuli zilizotekelezwa na asasi za kiraia na makundi ya kijamii 447 yaliyopewa ruhusa kutoa elimu kwa wapiga kura. Pamoja na kushirikiana na vituo 49 vya redio vilivyokuwa vikitangaza ujumbe wa elimu kwa wapiga kura, NEC pia ilitumia mitandao ya kijamii na kusambaza vitabu vya muongozo kwa wapiga kura, vyama vya siasa na kitabu cha maswali yanayoulizwa mara kwa mara. Hata hivyo, shughuli hizi, pamoja na shughuli zilizoendeshwa na asasi za kiraia, hazikutosha kabisa kukidhi mahitaji kwani wapiga kura hawakuwa na taarifa za kutosha kuhusu taratibu za kupiga kura zao, usiri wa kura, umuhimu wa uchaguzi na taasisi za kidemokrasia na pia hawakuwa na uelewa wa msingi wa sera za vyama vya siasa. Vipindi vya redio ndiyo vilikuwa vyanzo vikuu vya maelezo kwa wapiga kura.

Waangalizi wa EU waliripoti hali ya kutokuwa na shughuli za elimu kwa wapiga kura kwa ujumla kwenye mikoa mingi, haswa maeneo ya vijijini na miongoni mwa jamii za wafugaji kama Wamasai. Mashirika yasiyo ya kiserikali machache yaliendesha miradi midogo katika jamii iliyolenga wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Zaidi, NEC ilitegemea msaada wa Mradi wa Uwezeshaji wa Kidemokrasia (Democratic Empowerment Project - DEP) unaoendeshwa na UNDP kufanya shughuli za elimu kwa wapiga kura. Kampeni ya elimu kwa wapiga kura iliyopanga kutumia vyombo aina mbali mbali vya habari iliyonuia

---

[8] Kila jimbo lina shehia kadhaa. Idadi ya shehia iliongezeka kutoka 345 hadi 388 na idadi ya kata ilipungua kutoka 141 hadi 111. Masheha 43 wa shehia mpya hawakuteuliwa kabla ya uchaguzi.

[9] Kulikuwa na mifano mingine ya tofauti kubwa kama vile Tunguu ikiwa na wapiga kura 14,326 na Mwera ikiwa na wapiga kura 5,419.

uchaguzi shirikishi na wa amani, na kulenga wakazi wa maeneo ya vijivni, wanawake, vijana, wapiga kura wa mara ya kwanza na watu wenye ulemavu, ilipangwa kuzinduliwa siku kumi kabla ya siku ya kupiga kura. Hata hivyo, shughuli hizo hazikuonekana. Bila ya kuwa na elimu kwa wapiga kura isiyofungamana na vyama, wapiga kura walilazimika kupata taarifa zao kutoka kwa vyama vya siasa.

Upande wa Zanzibar, ZEC ilizipa asasi za kiraia 14 jukumu la kutoa elimu kwa wapiga kura, lakini shughuli zilichelewa sana kuanza na zilibanwa na uhaba wa fedha. Hivyo elimu kwa wapiga kura ilitolewa zaidi kupitia matangazo ya mara kwa mara ya ZEC yaliyokuwa yakitolewa kupitia vituo vya televisheni na redio vya Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) na kwenye kwenye vituo vya redio vya jamii. Vipeperushi na picha za kubandikwa ukutani za elimu kwa wapiga kura kutoka ZEC zilisambazwa kwa asasi za kiraia zilizopewa dhamana ya kutoa elimu kwa wapiga kura, na kwa madereva wa mabasi kuoneshwa kwenye magari yao na kwenye vituo vya mabasi. Zaidi, tume ilipanga kuandaa maigizo, tamasha na michezo ikilenga kuelimisha wapiga kura. Japokuwa ZEC ilizipa kazi kwa asasi za kiraia, kama vile Kituo cha Huduma za Sheria cha Zanzibar, kuendesha shughuli za elimu kwa wapiga kura, shughuli hizo hazikuoneka. Tamasha la Kimataifa la Filamu la Zanzibar (ZIFF) na asasi za kiraia zilizokuwa zikifanya kazi ndani ya Mradi wa Kuwezesha Mchakato wa Amani wa Uchaguzi (PROPEL) zilizungusha filamu iliyoongelea uchaguzi wa amani mara kumi.

## VI. Daftari la Wapiga Kura

### *A. Haki ya KupigaKura.*

Halkukuwa na masharti magumu kwa kujiandikisha kuwa mpiga kura kwa uchaguzi wa Muungano. Mfumo wa kisheria unaendana na misingi ya kimataifa ya haki ya kupiga kura kwa wote na ushirikishi. [10] Vigezo vya kustahili vilikuwa ni pamoja na kuwa na uraia wa Tanzania na kuwa na umri si chini ya miaka 18 ifikapo tarehe ya kupiga kura. NEC inaandikisha wapiga kura kwa uchaguzi wa Muungano, ikiwa ni pamoja na mtu yeyote aliye Zanzibar ambaye anastahili kupiga kura kwenye uchaguzi wa rais wa Muungano tu.

Daftari tofauti la wapiga kura linatumika kwa uchaguzi wa Zanzibar. Wazanzibari wenye umri zaidi ya miaka 18 wana haki ya kujiandikisha. Mtu lazima awe na makazi ya kudumu na awe ameishi katika jimbo kwa muda wa miezi 36 mfululizo kabla ya siku ya kupiga kura. Kitambulisho pia kinahitajika kupewa au kukuongeza muda wa kadi ya kupiga kura. Sharti la ukazi ili kuandikishwa kuwa mpiga kura, pamoja na mamlaka yaliyolalamikiwa waliyopewa *masheha* kuhakiki ukazi wa mpiga kura kwa miezi 36 jimboni, linaonekana kuwa gumu mno na linaleta uwezekano wa kukosa haki kwa wapiga kura wa Kizanziabri wanaostahili kupiga kura. [11]

Hakuna mfumo wowote wa kushirikisha Watanzania walio nje ya nchi, walio rumande au wafungwa wanaotumikia kifungo cha chini ya miezi sita ambao wana haki ya kupiga kura.

### *B. Uandikishaji Wapiga Kura*

***Jamuri ya Muungano wa Tanzania***

Mapungufu kwenye mfumo wa teknolojia ya OMR (Optical Mark Recognition) iliyotumika kwenye uchaguzi uliopita yalipelekea kutumika kwa mfumo mpya wa uandikishaji wa wapiga kura unaotumia alama za kimwili, yaani BVR (Biometric Voter Registration) kwa uchaguzi wa 2015. Serikali iliidhinisha bajeti kwa hili Januari 2015, baada ya kipindi cha majaribio cha uandikishaji kilichifanyika Desemba 2014 kwenye majmbo matatu kwenye mikoa ya Dar es Salaam, Katavi na Morogoro. Kati ya Februari na Agosti 2015, NEC

[10] Kifungu 25 cha ICCPR, Tume ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa, Maelezo Na. 25. Ibara ya 4: "Nchi lazima zishukue hatua za makusudi kuhakikisha kuwa watu wanaostahili kupiga kura wanaweza kutumia haki yao hiyo"

[11] Kifungu 25 cha ICCPR, Tume ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa, Maelezo Na. 25. Ibara ya 4: "Nchi lazima zishukue hatua za makusudi kuhakikisha kuwa watu wanaostahili kupiga kura wanaweza kutumia haki yao hiyo. Pale ambapo uandikishaji wa wapiga kura unahitajika, zoezi hilo lirahisishwe na kusiwekwe vizingiti vya kujiandikisha. Kama kuna sharti la ukaaji, basi liwe na mantiki…"

ilifanikiwa kuandikisha wapiga kura 23,782,558, ikiwa ni 99.6% ya idadi ya wapiga kura halali iliyotabiriwa na NEC pamoja na Baraza la Taifa la Takwimu. Umoja wa Ulaya ulituma Tume ya Watalamu wa Uchaguzi (EEM) nchini Tanzania, kati ya tarehe 8 Mei na 24 Julai 2015, kutathmini mchakato wa BVR. EEM iliona kuwa misingi ya haki ya kupiga kura kwa wote na fursa kuandikishwa kwa kutumia BVR ilitolewa na kulikua na ushiriki wa idadi kubwa ya wananchi. Daftari la wapiga kura la NEC Zanzibar ambalo linajumuisha majina ya wasio wakazi wa Zanzibar waliyo na haki ya kupiga kura kwenye uchaguzi wa rais wa Muungano tu, lilikuwa na wapiga kura 48,182, ambao kati yao, 28,132 walikuwa Unguja na 20,050 walikuwa Pemba.

Zoezi lililofanyika wakati huo huo la uchoraji mipaka ya kata mpya 622, lililofanywa na ofisi ya Waziri Mkuu, lilileta changamoto kwa NEC wakati wa zoezi la uandikishaji wapiga kura kwa BVR. NEC ililazimika kupitia upya taarifa za uandikishaji wakati zoezi la BVR likiendelea, hivyo kuchelewesha mchakato wa uandikishaji na kuhitaji upatikanaji wa ramani mpya zilizoendana na mabadiliko ya mipaka ya kata. Takwimu za BVR za 2015 huenda zikawa takwimu kamilifu zaidi ambazo zimewahi kupatikana nchini Tanzania. Hata hivyo, NEC haikusimamia ipasavyo mategemeo ya mwenendo wa uandikishaji miongoni mwa waandikishwa. Foleni ndefu, uhaba na ugavi usio na usawa wa rasilimali, kutokuwa na uwazi kwenye zoezi la uchoraji mipaka mipya, na kutokuwepo kwa kampeni za uelimishaji wananchi vyote viliathiri mtazamo wa watu juu ya uwezo wa NEC kuendesha uandikishaji shirkishi na wa kuaminika.

Daftari kamili la wapiga kura kwa uchaguzi wa Muungano lilitolewa siku 10 kabla ya siku ya kupiga kura, siku mbili kabla ya siku ya mwisho kwa mujibu wa sheria. Jumla ya wapiga kura 22,751,292 waliandikishwa. Kati ya hao, majina 1,031,266 yaliondolewa kwenye daftari la muda kukiwa na majina 181,452 yakionekana kuandikishwa zaidi ya mara moja. Kwa matukio kama hayo, NEC ilibakiza jina la mwisho lilioandikishwa. Yaliyobaki 845,944 yaliokosewa yalitokana na uandikishwaji uliofanyika katika kipindi cha mafunzo yaliotolewa kwa waendesha mashine za uandikishaji. Zaidi ya hayo, majina 3,870 yalibainika kuwa ni ya wageni. Zoezi la uandikishaji wa BVR liliweza kuandikisha asilimia 96 ya wapiga kura halali waliyokadiriwa kuwepo. Wasiwasi juu ya daftari la wapiga kura ambalo lingetumika ilipelekea NEC kutoa miongozo iliyolenga kushughulikia mazingira mengine ambayo yangemwezesha mpiga kura kupiga kura yake, ikiwa ni pamoja na masharti yaliyokuwepo tayari yaliyotaka jina la mpiga kura kuwepo kwenye orodha ya wapiga kura na mpiga kura kuwa na kadi ya mpiga kura mkononi. Masharti ya ziada yalionekana kuwa ya maana na ambayo yasiyo na ubaguzi.

Vyama vya siasa vilipatiwa nakala ya daftari kwa nia ya kompyuta. Ingawaje sheria haihitaji orodha ya wapiga kura kutolewa mapema zaidi, upatikananji mapema zaidi wa daftari ungeweza kuongeza imani ya wadau juu ya uhalali wa daftari la wapiga kura na kuboresha mipango ya kampeni za vyama vya siasa kutokana na kuwaelewa vizuri zaidi wapiga kura wao, haswa ikizingatiwa mabadiliko yaliyofanyika ya majimbo na mipaka.

***Zanzibar***

ZEC ilifanya zoezi la kutengeneza upya daftari la kudumu la wapiga kura kwa ajili ya uchaguzi wa mwaka 2015. Daftari lililopatikana lilikuwa na wapiga kura 503,860 waliondaikishwa, kati yao 269,073 wakiwa wanawake na 235,060 wanaume. Kulingnishwa na daftari la mwaka 2010, hii ilikua ni ongezeko la asilimia au wapiga kura 96,478. ZEC ilitangaza orodha ya wapiga kura 7,751 waliofutwa kutoka kwenye daftari. Mengi ya majina yaliyoondolewa yalikuwa ya waliyofariki pamoja na majina yaliyoandikishwa mara mbili. Fursa kwa wapioga kura halali kuhakiki maelezo yao kwenye daftari ilikuwa ndogo, kwani wapiga kura hao walipewa siku mbili tu kujiandikisha kwenye vituo walivyopangiwa kwenye maeneo ya makazi yao. Tathmini ya EU EEM ya mchakato wa uandikishaji wa mwaka 2015 ilikuwa kwamba ulikuwa na vikwazo mno kutokana na sharti la kuwa na kitambulisho cha Zanzibar ili kuandikishwa, pamaoja na mamlaka yaliyoleta mvutano ya

*Masheha* ya kutoa vitambulisho.[12]

ZEC ilivipa fursa vyama vya siasa kupata daftari tarehe 7 Oktoba. Kama ilivyokuwa upande wa Muungano, kutolewa mapema zaidi kwa daftari kungeongeza imani ya wadau juu ya mchakato wa uchaguzi na hasa juu ya uhalali wa daftari la wapiga kura.

ZEC ilitoa vitambulisho vya kupiga kura baada ya kufanya zoezi la uhakiki, tofauti na NEC, iliyochapisha na kutoa kadi ya kupiga kura mara baada ya kuandikishwa. Utoaji wa kadi za kupipga kura uliendelea kwenye ofisi za wilaya hadi siku ya uchaguzi. ZEC pia ilisambaza kadi zilizotolewa mwaka 2010 na 2013. Hata hivyo kuilikuwa na utata kwa wapiga kura juu ya sehemu ya kwenda kuchukua kadi zao za kupigia kura. Kadi za kupigia kura ambazo zingekuwa hazijachujkuliwa na wenyewe kutoka ofisi za wilaya zilitakiwa kurudishwa ofisi kuu ya ZEC kufikia tarehe 19 Oktoba. Kabala ya hapo wapiga kura kadhaa hawakuweza kupokea kadi zao walipofika kwenye ofisi za wilaya na kuonyesha stakabadhi za kulipia kadi ya kupigia kura. ZEC ilitangaza kupitia redio kuwa wapiga kura wangeweza kupokea kadi zao hadi tarehe 24 Oktoba kutoka ofisi ya ZEC. Kwa mujibu wa ZEC, takriban wapiga kura 8,000 walikua hawajachukuwa kadi zao kabla ya siku ya kupiga kura.

EU EOM ilijionea yenyewe kuwa sharti la kuonyesha kitambulisho cha Zanzibar au stakabadhi ya kuandikishwa ili kupokea kadi ya kupigia kura halikwua linafuatwa kila wakati na maafisa wa ZEC. Tarehe 9 Oktoba, kwenye ofisi ya ZEC Magharibi B kisiwani Unguja, waangalizi wa EU waliona mabasi matano, yalioandaliwa na kamati ya masheha, yakiwafikisha vijana ofisini hapo kupokea kadi zao za kupigia kura. Kati yao, hakuna aliyeonyesha kitambulisho cha Zanzibar wala stakabadhi ya uandikishaji kupiga kura, masharti rasmi ya kupokea kadi. EU EOM iliona kuwa kadi zilitolewa kwa mtu kutaja jina lake tu, kinyume na taratibu ilivyoonekana awali kwenye ofisi hiyo hiyo ya ZEC. Watu waliyopokea kadi zao walitaja namba zao za simu kwa wasimamizi na majina yao yakawekewa alama kwenye orodha.

## VII. Usajili wa Vyama vya Siasa na Wagombea

### *A. Usajili wa Vyama vya Siasa*

Masharti ya kusajili vyama vya siasa ni ya kueleweka na yanaenda na makubaliano ya kimataifa juu ya uhuru wa kujumuika. Hata hivyo, haki ya vyama kuunda muungano haijatajwa kwenye sheria. Kiutendaji, vyama viliweza kupendekeza mgombea mmoja kwa uchaguzi na kuzungumzia umoja kwenye mikutano ya kampeni, lakini jina la umoja huo halikuweza kuwekwa kwenye karatasi za kupigia kura.

Sheria ya vyama vya siasa inabainisha masharti na taratibu za kuandikisha vyama vya siasa. Vyama vinavyoendekeza maswala ya kidini, kikabila au kimkoa, vinavyo pendekeza kuvunjwa Muungano au vinavyotumia vurugu kuendeleza sera zake vinazuiwa kusajiliwa. Zaidi, sheria inamtaja Msajili wa Vyama vya Siasa, anayeteuliwa na rais, kuwajibika kwenye swala la usajili wa vyama vya siasa. Uamuzi wa msajili juu ya kufutwa uandikishwaji wa chama unaweza kukatiwa rufaa mahakamani.

Vyama vitatu viliomba usajili kwa ajili ya uahcaguzi wa mwaka 2015 na ni kimoja tu kilipata usajili kamili, chama cha Alliance for Cange and Transparency (ACT au ACT-WAZALENDO). Vingine viwili havikukidhi vigezo vya kusajiliwa. Kwa kesi zote mbili hizo, Msajili wa Vyama vya Siasa alivipatia vyama hivyo maelekezo juu ya mapungufu yaliyokuwepo. Kutakana na hilo, tarehe 9 Novemba 2015, Msajili wa vyama vya siasa alitoa usajili wa muda kwa chama cha Tanzania Patriotic Front (TPF-Mashujaa), ambacho kilikuwa cha kwanza kuomba usajili baada ya uchaguzi.

[12] Kifungu 25 cha ICCPR, Tume ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa, Maelezo Na. 25. Ibara ya 4: “Nchi lzima zishukue hatua za makusudi kuhakikisha kuwa watu wanaostahili kupiga kura wanaweza kutumia haki yao hiyo. Pale ambapo uandikishaji wa wapiga kura unahitajika, zoezi hilo lirahisishwe na kusiwekwe vizingiti vya kujiandikisha. Kama kuna sharti la ukaaji, basi liwe na mantiki…”

*B. Usajili wa Wagombea*

Masharti ya kugombea nafasi ya urais, ubunge na udiwani, kama yalivyoelezwa kwenye Katiba za Muungano na Zanzibar na sheria zake za uchaguzi, ni za kueleweka na za wastani, isipokuwa kipengele cha Katiba kinachozuia wagombea binafsi. Sharti linalohitaji mgombea kuwa mwanachama na kupendekezwa na chama cha siasa kinanyima haki na fursa kwa watu kugombea nafasi na kupunguza idadi ya wagombea wapiga kura wanaoweza kuwachagua. [13] Ingawaje sheria haizungumzii moja kwa moja kuungana kwa vyama, vyama vya siasa vinaweza kushirikiana katika kupendekeza wagombea na kutoa msaada kwa wagombea hao.

Majina ya wagombea wa nafasi ya urais wa Muungano na Zanzibar yanawasilishwa kwa NEC na ZEC, ambapo majina ya wagombea ubunge wa Muungano na Baraza la Wawakilishi Zanzibar na udiwani yanashughulikiwa na wasimamizi wa uchaguzi kwenye ngazi ya jimbo na wasimamizi wasaidizi wa kata. Wagombea hawaruhusiwi kugombea, kwa wakati mmoja, nafasi ya rais na ubunge. Lakini hakuna kizuizi kwa mgombea kugombea ubunge na udiwani.

Mara baada ya kuwasilisha majina ya wagombea, vyama vya siasa vinatakiwa kulipa dhamana kwa kila mgombea. Kiwango kwa nafasi za urais na ubunge wa Muungano ni TZS milioni moja (Euro 400) kwa urais na TZS 50,000 (Euro20) kwa ubunge. Amana pia inahiutajika kwa wagombea urais na uwakilishi wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, ambayo ni mara mbili ya kiwango cha amana za Muungano, TZS milioni mbili (Euro 800) kwa urais na TZS 100,000 (Euro 40) kwa Baraza la Wawakilishi. Baada ya kupendekeza majina, Sheria ya Gharama za Uchaguzi inavitaka vyama vya siasa kueleza fedha zote ambazo vimepokea kwa matumizi ya uchaguzi, kwa mchakato wa kupendekeza majina au kwa kampeni za uchaguzi, iwe ni zawadi, mkopo, karadha, amana au michango. Chama chcochote au mgombea yeyote anayeshindwa kutoa maelezo haya haruhusiwi kugombea kwenye uchaguzi.

Wagombea nane, pamoja na wagombea wenza, walipendekezwa kugombea nafasi ya urais wa Muungano. Pamoja na wagombea wa CCM na Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA), iliyoundwa na Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Chama cha Wananchi (CUF), NCCR-Mageuzi na NLD, vyama vingine sita viligombea urais wa Muungano.

Mgombea wa ACT na Mgombea wa nafasi ya makamu wa rais wa CCM ndiyo walikuwa wagombea pekee wanawake. Mapendekezo kutoka vyama viwili, TADEA na CCK, yalikataliwa kwa kutokidhi masharti kitaratibu. Kulikuwa na wagombea 1,218 waliogombea viti 264 vya majimbo kwenye Bunge la Muungano, na wagombea 10,879 wa udiwani.

Pingamizi au malalamiko juu ya mapendekezo ya majina ya wagombea wa nafasi za Bunge la Muungano au Baraza la Wawakilishi yanawasilishwa kwa msimamizi wa uchaguzi husika, ambaye maamuzi yake yanaweza kukatiwa rufaa kwa NEC na ZEC. Njia pekee kwa mapendekezo ya kugombea ubunge yanayokataliwa kukatiwa rufaa ni kuwasilisha lalamiko baada ya matokeo kutangazwa rasmi, hivyo kunyima haki ya kupata suluhisho la wakati kwa mlalamikaji. Hata hivyo, kuna njia inayoweza kutumika kupinga uamuzi huu mapema zaidi kwa kuomba mahakama kuupitia upya na hii ni kwa mujibu wa katiba za pande zote mbili. Hata hivyo, mahakama inaweza kufuta kesi kwa sababu za kiutaratibu na kuagiza kesi kufunguliwa mahakamani baada ya kutangazwa matokeo. NEC ilipokea rufaa 56 dhidi ya maamuzi ya wasimamizi wa uchaguzi za pingamizi na malalamiko juu ya mapendekezo ya majina ya wagombea, na rufaa 233 zilizohusu mapendekezo ya majina ya wagombea udiwani. Pingamizi na malalamiko mengi yalikuwa ni ya kukiukwa taratibu. Takriban asilimia 50 ya maamuzi yalipitishwa na asilimia 50 yalipinduliwa na NEC.

---

[13] Kifungu 25 cha ICCPR, Tume ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa, Maelezo Na. 25. Ibara ya 15: "utekelezaji wa haki na fursa ya kugombea nafasi kwenye uchaguzi unahakikisha kuwa watu wenye haki ya kupiga kura wanapata chaguo huru la wagombea. Watu amabo vinginevyo wasngestahili kugombea nafasi kwenye uchaguzi hawatanyimwa kwa kuwa na vigezo vya ubaguzi kama vile elimu, makaazi au familia, au kwa sababu za mfungamano wa kisiasa"

Kwa nafasi ya urais Zanzibar, vyama 14, ikiwa ni pamoja na CCM na CUF vilipendekeza wagombea. Rais wa wakati huo wa Zanzibar, Ali Mohamed Shein wa CCM aligombea muhula wa pili. Kulikuwa na wagombea 180 wa majimbo 54 ya Baraza la Wawakilishi, na wagombea 353 kwa halmashauri 111. ZEC ilipokea malalamiko 6 juu ya mapendekezo ya majina ya wagombea na kupindua uamuzi kwenye kesi moja ya kupendekeza mgombea wa halmashauri.

## VIII. Kampeni za Uchaguzi na Mazingira Kabla ya Uchaguzi

### *A. Kampeni za Uchaguzi*

Kampeni za uchaguziTanzania Bara zilianza tarehe 22 Agosti na Zanzibar zilianza tarehe 7 Septemba. Kampeni, pande zote mbili Bara na Zanzibar, zilionekana kuwa kali. Upande wa Bara, CCM na UKAWA wote waliandaa kampeni za kitaifa, mara nyingi kukiwa na mikutano kadhaa kila siku, na kuvutia maelfu ya watu kwenye karibu mikutano yote. ACT kilikua chama pekee kingine kilichofanya kampeni kitaifa, ingawa kilivuta makundi madogo zaidi.

EU EOM iliangalia mikutano ya kampeni 139 nchini, ambayo 53 ilikuwa ni ya CCM, 67 ya CHADEMA, CUF, NCCR, NLD na/au UKAWA, 14 ilikuwa ya ACT na 5 ya vyama vingine vidogo zaidi. Kwenye mikutano ya kampeni iliyoangaliwa, wagombea na vyama vilifanya kampeni kwa nguvu, na kwa ujumla kutii masharti ya kampeni, ikiwa ni pamoja na kutotumia lugha za uchochezi na kufuata masaa yaliyopangwa kwa kampeni. Kampeni za uchaguzi kwa kiasi kikubwa zilikuwa tulivu na za amani, na ratiba ya mikutano ya kampeni za urais na makamu rais ilikubalika kwa maridhiano na kupitiwa na vyama vyote. Kwenye tukio moja tu, Kyengege mkoani Singida, EU EOM iliona upendeleo ukionyeshwa kwa CCM kwenye kupanga ratiba ya mikiutano ya kampeni.

Matukio machache yaliyotokea, ikiwa ni pamoja na kutekwa mgombea ubunge wa CHADEMA Mtwara tarehe 5 Oktoba, kupigwa kwa wanachama wa CCM waliyohamia CHADEMA Sumbawanga tarehe 8 Oktoba na kuvamiwa wafuasi wa CHADEMA waliyokuwa njiani kuelekea mkutano wa kampeni ya upinzania tarehe 10 Oktoba kwenye eneo hilo, pamoja na kupigana Tabora tarehe 10 Oktoba kati ya wafuasi wa CUF na CCM, yalikuwa na athari ndogo kwa mazingira ya uchaguzi. Vyama vya siasa na wagombea waliweza kufanya kampeni kwa uhuru maeneo yote ya Tanzania Bara, na vyama vingi vililipongeza jeshi la polisi kwa utendaji kazi wake wakati wa mikutano ya kampeni, lakini kulikuwa na matukio kadhaa ya wagombea wa CHADEMA na CUF na wanaharakati kukamatwa kwa makosa ya vurugu, kwenye maeneo kadhaa pamoja na Dodoma, Iringa, Morogoro, Katavi na Mara. [14] Bukoba, mkoani Kagera, wanachama na wafuasi wa CUF walikamatwa na kushtakiwa na polisi kwa kuhusika na uharibifu wa makanisa. CUF ilituhumu kuwa kukamatwa huko kulitokana na sababu za kisiasa, lakini polisi walikanusha kuwasaka watu kutokana na mfungamano wao kisiasa.

Jumbe za kampeni nyingi zililenga haja ya kuwa na mabadiliko, na kulikuwa na machache sana ya kutofautisha vyama kwenye sera, isipokuwa maswala ya elimu, ambako UKAWA waliahidi elimu bure kuanzia msingi hadi chuo kikuu, wakati CCM waliahidi elimu bure hadi sekondari tu. Kwenye mikutano mingi, CCM ilijiweka mbali na historia yake kama chama tawala, wakati UKAWA ilijinadi kuwa njia bora ya kuondoa utawala uliyokuwepo muda mrefu.

Kukiwa na matumaini makubwa kwa mdahalo kati ya wagombea wakuu, CCM na UKAWA wote walikataa kushiriki kwenye mdahalo wa ana kwa ana, na mdahalo wa urais, uliyofanyika tarehe 18 Oktoba, ulikuwa na washriki wa vyama vidogo tu.

Kulinganisha na upande wa bara, kampeni za Zanzibar zilikuwa za nguvu zaidi, kukiwa na mvutano kati ya vyama viwili vya Serikali ya Umoja, CCM na CUF. Maneno makali yaliyotumika na baadhi ya viongozi wa

[14] Angalia Kifungu XII. Utendaji wa Haki Kiuchaguzi: A. Makosa ya Kiuchaguzi, ukurasa 32.

vyama wakati wa kampeni wakati mwingine yalikuwa yanaelekea kuwa ya kibaguzi, yaliongeza mvutano katika jamii na yangeweza kuchukuliwa kuwa ni ya uchochezi. Kwa mfano, ADC kwenye mkutano wa kampeni tarehe 5 Oktoba, kisiwani Pemba ilisema kuwa CUF haiwezi kuaminika na kukipigia kura chama hicho inaweza kuleta mfarakano Zanzibar kama ule wa Somalia. Kwenye mkutano wa kampeni wa CCM Chake Chake Pemba tarehe 11 Oktoba, makamu wa pili wa rais wa Zanzibar aliwataja viongozi wa CUF kuwa waongo na kuwa watu wanaofanana na wachawi. Zaidi aliituhumu CUF kuiba fedha za maendeleo ya majimbo.

Viziwani Zanzibar, baadi ya vyama vilikuwa havina imani na muennendo wa polisi kwenye kampeni, na matukio mahcache ya vitisho kwa wapiga kura vilivyo fanywa na vyombo vya usalama viliorodheshwa na EU EOM, pamoja na kilichoonekana kuwa jaribio la wazi la vyombo vya usalama la kuwatisha wafuasi wa upinzani jioni ya tarehe 1 Oktoba pale Sarayevo, Unguja, wakati maafisa wa usalama, waliokuwa hawako kwenye sare, walienda eneo la mkutano wa kampeni ya upinzani uliyokuwa ukifanyika mapema siku hyo, na kuharibu mali za watu waliyoonekana kuwa wafuasi wa upinzani, jambo lililopelekea kuongezeka kwa mvutano na kutumiwa mabomu ya machozi na silaha za moto. Hata hivyo, pamoja na matukio hayo, na ukali wa ushindani, kampeni za Zanzibar kwa jumla zilikuwa za amani.

Kwenye siku za mwisho za kampeni, ugomvi wa maneno kati ya upinzani na serikali juu ya uhalali na kufaa kwa maneno ya kuwashawishi wapiga kura kubaki maeneo ya vituo vya kupigia kura ili “kulinda kura” baada ya kupiga kura ilichangia kuwa na hali ya wasiwasi wa usalama katika kipindi kuelekea uchaguzi, pande zote mbili za Tanzania bara na Zanzibar, ingawaje kulikuwa na athari ndogo siku ya uchaguzi.

*B. Matumizi ya Rasilimali za Dola*

Pamoja na kwamba kujitokeza kwa umoja wa upinzani kuliongeza ushindani wa kampeni za uchaguzi, CCM iliendelea kunufaika kutokana na nafasi yake kihistoria kama chama tawala, na kilendelea kuwa chama chenye mpangilio bora na chenye uwezo mkubwa kifedha. Matumizi na chama hicho ya rasilimali ambazo zamani zilikuwa ni za dola, kama vile viwanja vya umma na viwanja vya michezo, jambo ambalo EU EOM iliona kwenye mikoa ya Arusha, Dodoma, Katavi na Kigoma, yalikipa nafasi zaidi ya vyama vingine, na yalichangia kutokuwepo na usawa katika mazingira ya kampeni. Wakati mwingine hii ilimaanisha kuwa vyama vingine vilijikuta vinaishia maeneo yasiyo bora, kwa mfano Arusha ambapo mikutano ya CHADEMA ilikuwa ikifanyika kwenye uwanja wenye matope nje ya mji.

Watumishi wa umma wakati mwingine walionekana kuhudhuria mikutano ya kampeni wakiwa katika nyadhifa zao, ikiwemo kwenye mikoa ya Mwanza na Zanzibar, na kulikuwa na taarifa za kutumika magari ya ofisi kwa shughuli za vyama kwenye mikoa kadhaa. Uzinduzi wa baadhi ya miradi mikubwa, ikiwemo uzinduzi wa mradi wa bomba la gesi Mtwara, tarehe 10 Oktoba, ufunguzi wa tawi la benki kuu Dodoma tarehe 15 Oktoba, kuwekwa jiwe la msingi la bandari mpya Bagamoyo tarehe 16 Oktoba na uzinduzi wa uwanja wa michezo Dar es Salaam tarehe 17 Oktoba, vyote katika wiki za mwisho za kampeni, zilizidi kupunguza kutofautisha kati ya serikali na chama tawala, na kuongeza nguvu kwenye kampeni za CCM. Hata hivyo, matumizi ya rasilimali za dola yalitajwa mara chache sana na vyama vya siasa na yalipata kufuatiliwa kwa kiasi kidogo tu na vyombo vya habari na waangalizi wengine.

Rais Kikwete aliingilia moja kwa moja kampeni siku ya kumbukumbu ya Nyerere tarehe 14 Oktoba alipokosoa ushawishi wa upinzani kwa watu kubaki maeneo ya kupigia kura, na kuchangia vita ya maneno kati ya serikali na upinzani.

*C. Fedha za Kampeni*

Sheria ya Gharama za Uchaguzi ya 2010, inayotumika kwa uchaguzi mkuu wa Muungano, inasimamia gharama za mchakato wa kuchagua wagombea ndani ya chama na kampeni. Waziri mkuu, kupitia taarifa ya serikali na. 325, iliyotolewa mwezi Agosti, alitaja kima cha gharama za uchaguzi kuendana na ukubwa wa

majimbo, aina ya uchaguzi, idadi ya watu na mfumo wa mawasiliano uliyokuwepo. Viwango hivi vimeongezwa kwa takriban asilimia 10 kutoka viwango vilivyokuwepo kwenye chaguzi zilizopita. Kwa chaguzi za Muungano mwaka 2015, kiwango cha juu kilichopangwa kwa gharama za kampeni za urais kwa kila chama kilikuwa ni TZS bilioni 17 (Euro milioni 7).

Michango kwa vyama vya siasa inaweza kupokelewa kutoka kwa mtu au taasisi yoyote ndani au nje ya nchi ya Tanzania, lakini michango kutoka nje ya nchi hairuhusiwi kupokelewa kwa siku 90 kuelekea siku ya kupiga kura. Vyama vyote vinavyogombea viliwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa viwango vilivyoukusudiwa kutumika kama gharama za uchaguzi. Katika kipindi kisichozidi siku 60 baada ya siku ya kupiga kura, kila mgombea anatakiwa kuwasilisha kwa chama chake ripoti iliyohakikiwa ya fedha alizotumia. Chama lazima, katika kipindi kisichozidi siku 180, kiwasilishe kwa Msajili wa Vyama vya Siasa taarifa ya matumizi pamoja na ushahidi wa malipo. Kama taasisi yenye wajibu wa usimamizi wa matumizi ya vyama vya siasa wakati wa uchaguzi, Msajili wa Vyama vya Siasa ana mamlaka ya ukaguzi na kudai maelezo, na anaratibu kazi zake na taasisi kadhaa za serikali ikiwa ni pamoja na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu wa Serikali (CAG), Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na zinginezo. Wakati wa kuandika ripoti hii, vyama vya siasa vilikuwa bado havijawasilisha taarifa za matumizi yao kwa Msajili wa Vyama vya Siasa.

Hakuna ruzuku inayotolewa maalum kwa kuendesha kampeni za vyama. Vyama vyote vilivyo na wabunge kwenye Bunge la Muungano na wawakilishi kwenye Baraza la Wawakilishi Zanzibar vinapatiwa ruzuku kuendesha shughuli za vyama hivyo kuendana na idadi ya viti vilvyokuwa navyo. Pamoja na kuwa vyama vyote vilivyo na viti Bungeni vilikiri kuwa kampeni zao ziliendeshwa na sehemu ya ruzuku hii, viwango na ushindani wa uchaguzi wa 2015, na takwimu zilizotajwa na baadhi ya vyama, inaashiria kulikuwa na kiwango kikubwa cha fedha kimepatikana kutoka vianzo vingine. Wagombea wengi wa upinzani walitegemea rasilimali zao binafsi. CHADEMA, NCCR-Mageuzi na ACT-WAZALENDO waliripoti kuwa walitumia kiasi kikubwa sana kuliko walivyotarajia, na walifanya shughuli kadhaa za kuchangisha fedha ili kufidia gharama za kampeni ya urais. Wagombea wa ubunge wanatarajiwa kujitegemea. CHADEMA pia ilikiri kupokea michango mikubwa kutoka watu binafsi, lakini haikutaja viwango. CCM haikutoa maelezo yoyote juu ya bajeti yake ya kampeni wala vyanzo vya fedha, ingawa kutokana na viwango vya utangazaji wake, ilielekea kuwa chama chenye rasilimali kubwa na kilichokuwa na gharama kubwa zaidi.

## IX. Waangalizi wa Uchaguzi wa Kitaifa na Kimataifa

Makundi makuu yaliyofanya uangalizi wa uchaguzi yalikuwa Kamati ya Uangalizi wa Uchaguzi Tanzania (TEMCO) na TACCEO.[15] Umoja wa Uangalizi wa Ufuatiliaji wa Uchaguzi Tanzania (CEMOT) iliziunganizha TEMCO na TACCEO. TEMCO na TACCEO kwa pamoja zilituma waangalizi 350 wa muda mrefu, na takriban 2,100 wa muda mfupi. TACCEO na TEMCO pia walituma waangalizi wa muda mrefu Zanzibar, pamoja na Chama cha Uongozi cha Kiislamu (MLO) kilichokuwa na waangalizi wa muda mrefu huko Visiwani. Chini ya CEMOT, walikuwa na muangalizi angalau moja wa muda mrefu kila wilaya. Taasisi mbili hizo ziliendesha mafunzo kwa waangalizi wao kila mmoja kivyake, zilitoa maoni yao kutokana na mbinu mbili tofauti na kutoa tamko mbili tofauti. CEMOT ilianzisha kituo cha uangalizi wa uchaguzi ambako takwimu za uchaguzi zilikusanywa na kuchambuliwa. Kituo kilikuwa na wawakilishi kutoka NEC, ZEC na ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Jeshi la Polisi.

Tamko la awali la TEMCO lilibainisha mapungufu ya kisheria kwenye mfumo wa uchaguzi, ikiwa ni pamoja

[15] Tanzania Civil Society Consortium of Election Observation (TACCEO) ni umoja usiyo wa kiserikali, usiyo wa kichama na usiyofanya shughuli zake kwa faida za kifedha unaohusisha asasi 17 za kiraia. Umoja huu uliundwa kabla ya uchaguzi wa 2010. Kituo cha Haki Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) ndiyo kinachoratibu waangalizi wa TACCEO wengi wao wakiwa na sifa za kisheria. Tanzania Election Monitoring Committee (TEMCO), ilyoundwa 1995, inafanya kazi pamoja na zaidi ya taasisi 172, zikiwemo za dinizenye miundo ngazi za wananchi nchini. Mradi wa kichuo Research and Education for Democracy in Tanzania (REDET) ndiye wakala mkuu wa waangalizi wa TEMCO. Shughuli za TEMCO zinafadhiliwa na USAID, Ubalozi wa Uholanzi, Ubalozi wa Canada pamoja na Open Society Initiative for East Africa.

na uteuzi wa makamishna wa NEC, wakihoji uwezo wao wakutekeleza majukumu bila upendeleo. Kutokuwepo na mfumo wa NEC nje ya makao makuu, uwezo wa kutegemea wasimamizi walioteuliwa kwa shughuli maalumu kutekeleza majukumu bila upendeleo, kutokuwepo na ruhusa kisheria kwa wagombea binafsi, kunyimwa raia walionje ya nchi kupiga kura na kugombea nafasi, mapungufu ya mifumo ya kuhakikisha Sheria ya Gharama za Uchaguzi inafuatwa pia ziliongelewa. TEMCO/CEMOT ilifanya uangalizi kwenye vituo 6,579 vya kupigia kura. Matukio ya majina ya wapiga kura kutokuwepo kwenye daftari la wapiga kura yalionekana kwenye asilimia 18 ya vituo vilivyotembelewa. Mapendekezo makuu ya TEMCO yalilenga uhitaji wa marekebisho makubwa ya mfumo wa uchaguzi kuruhusu wagombea binafsi, kupinga matokeo ya uchaguzi wa rais, vifungu vya sheria kuruhusu vyama kuunda ushirikiano na umoja, raia waliyo nje ya nchi kupiga kura.

CEMOT ilitathmini kuwa, kwa ujumla, uchaguzi ulikuwa huru na kuwa matokeo yaliendana na matakwa ya wananchi. Kwa maoni yake, pamoja na kuwepo kwa mapungufu hapa na pale, uchaguzi kwa kiasi kikubwa, ulifuata sheria. Mapendekezo yalikuwa ni pamoja na haja ya na NEC kuwa na uwazi zaidi, ushirikishwa zaidi wa wadau, kuboresha mikakati ya mawasiliano na kuboresha mfumo wa maelezo kwa jamii juu ya mchakato wa uchaguzi.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), taasisi kuu ndani ya TACCEO, ilitamka kwenye taarifa ya awali kuwa shughulia za elimu ya uraia na wapiga kura hazikutolewa kwa wapiga kura, kwamaba kulikuwa na haja ya marekebisho ya mfumo wa kupiga kura ili kuongeza uwazi kwenye mchakato wa uchaguzi na kuwa na ratiba ya wazi ya utangazaji wa matokeo. Ripoti ilizungumzia tuhuma za rushwa wakati wa shughuli za kugombea kupendekezwa ndani ya vyama pamoja na, nyakati nyingine, matumizi mabaya ya rasilimali za umma kama vile magari ya serikali kwenye kampeni za urais. Zaidi, LHRC iliona kuwa kuongezeka kwa uwepo wa polisi na magari ya kuzuia vurugu katika kipindi cha uchaguzi kulileta hali ya hofu na vitisho ambavyo viliathiri ushiriki huru wa wapiga kura kwenye mchakato wa uchaguzi.

LHRC ilitoa ripoti ya hali baada ya uchaguzi kutokana na kuvamiwa na polisi kwenye kituo chao cha uangalizi wa uchaguzi tarehe 29 Oktoba.[16] Kituo kilishtakiwa, chini ya kifungu cha 16 cha Sheria ya Makosa ya Mtandao, kutangaza na kutangaza taarifa zisizo za kweli, za udanganyifu, za kupotosha na/au zisizokamili. LHRC iliiomba NEC kutangaza kwa umma uhalali na haki za kundi hilo la uangalizi.

Kwa mujibu wa NEC, takriban waangalizi 600 wa kimataifa walitumwa kwa ajili ya uchaguzi mkuu, zikiwemo tume za kibalozi kutoka Marekani na Uingereza. Tume za kimataifa za uangalizi zilizokuwepo nchini kwa uchaguzi wa 2015 ni pamoja na ile ya Umoja wa Afrika iliyoongozwa na Armando Guebuza, Rais Mstaafu wa Msumbiji; ya SADC ilyoongozwa na Oldemiro Baloi, Waziri wa Mambo ya Nje wa Msumbiji; Kundi la Waangalizi wa Nchi za Jumia ya Madola (COG) lililoongozwa na Goodluck Jonathan, Rais Mstaafu wa Nigeria, na ile ya Jumuia ya Africa Mashariki (EAC), iliyoongozwa na Makamu wa Rais Mstaafu wa Kenya, Moody Awori.

## X. Vyombo vya Habari na Uchaguzi

### *A. Mazingira kwa vyombo vya habari*

Tanzania ina vyombo vya habari vingi na vyenye muamko. Redio bado ndiyo chanzo kikuu cha upatikananji taarifa kitaifa, ikifuatiwa na televisheni na magazeti. Takriban mtu mmoja kati ya watano pia anatumia mtandao, zaidi kupitia simu za mkononi.

Tanzania Bara kuna vituo 84 vya redio na 26 vya televisheni vinavyotoa matangazo kitaifa, kimkoa na

[16] TACCEO na LHRC walitoa tamko juu ya kukamatwa kwa waangalizi wa uchaguzi, kunyang'anywa vifaa vya uangalizi wa uchaguzi kutoka kwenye kituo, Novemba 2015.

kiwilaya zikiwemo redio za jamii zilizoandikishwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Mawasiliano (TCRA). Vyombo vinavyowafikia watu wengi zaidi kitaifa ni vituo vya televisheni na redio za Taifa (TBC) na vituo tisa vya televisheni na redio binafsi. Mfumo wa usambazaji magazeti nje ya mijini ni duni. Magazeti ya kila siku ya Kiswahili yenye wasomaji wengi ni magazeti binafsi ya Mwananchi na Nipashe, yakikisiwa kuuza nakala 40,000 kila moja, na gazeti la Kitaifa la Daily News linalochapishwa kwa Kiingereza.

Visiwani Zanzibar, wapiga kura wanafikiwa na vyombo vichache zaidi vya habari. Vyombo vya Kitaifa, hususan vituo vya televisheni na redio vya Zanzibar Broadcasting Corporation (ZBC) ndivyo vyenye nafasi kubwa zaidi kwani hakuna kituo binafsi cha televisheni. Gazeti la kitaifa la Zanzibar Leo ndiyo gazeti pekee linalochapishwa Zanzibar. Hata hivyo, vituo vya televisheni binafsi vinavyo rusha matangazo kutoka Tanzania Bara vinapatikana pamoja na vituo kadhaa binafsi vya redio vilivyopo Zanzibar. Lakini, habari zinazotolewa na vituo hivyo juu ya maendeleo ya kisiaza Zanzibar ni chache sana.

Vyombo vya utangazaji vya Taifa vya TBC na ZBC, pamoja na kuwa vilikusudiwa kuwa vyombo vya umma kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano ya Tanzania, 2003, havina uhuru wa uhariri kutoka serikali zake husika kinyume na kanuni za kimataifa juu ya uhuru wa vyombo vya habari.[17] Rais ndiye anayemteua mkurugenzi mkuu wa shrika la utangazaji la Taifa, na Waziri mwenye dhamana ya habari anateua wanabodi wote isipokuwa mmoja, anayeteuliwa na wafanyakazi wa TBC na ZBC. Vituo vyote viwili vinaonekana kuwa chini ya serikali. Wingi wa maoni nchini unabanwa, kwa kiasi fulani, kwa kampuni chache kushikilia vyombo vikuu vya habari, na, mbaya Zaidi, baadhi ya hizi kampuni kuwa na mahusiano na vyama vya siasa, hususan chama tawala. Mapato yatokanayo na matangazo ya biashara hayatoshi kuendesha sekta ya habari moja kwa moja, jambo linaloleta uwezekano mkubwa kwa vyombo vya habari kuachia uhuru wa uhariri ili kujipatia faida za kifedha. Washirki wa mazungumzo wa vyombo vya habari kutoka EU EOM wamekiri kuwepo kwa kiwango kikubwa cha kujidhibiti miongoni mwa waandishi wa habari nchini Tanzania, hususan kwenye vyombo vya habari vya taifa na kwenye vile vyombo vinavyo fungamana na vyama vya siasa. [18]

Pamoja na uhuru wa kujieleza kuwa kwenye Katiba, kuna sheria kadhaa zinazobana haki hii ya msingi na zinapelekea waandishi kujidhibiti. Sheria ya Usalama wa Taifa ya 1970 inazuia upatikanaji wa taarifa ambazo zimeamuliwa kuwa ni siri, ikiwa haina ufafanuzi dhahiri wa jinsi maamuzi hayo yanavyofikiwa. Sheria ya Magazeti ya 1976, inayoongoza sekta ya uchapishaji magazeti, inasema kukashifu ni kosa la jinai. Sheria ya Utumishi wa Umma ya 2002 inazuia utoaji wa taarifa kwa watumishi wa umma kwenda kwa wasiostahili. Sheria zingine, ikiwemo ya Sheria ya Utangazaji ya 1993, Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya 1995 na Sheria za Ajira na Uhamiaji zinavipengele ambavyo vinaweza kutumika kubana uhuru wa kujieleza na upatikananji wa taarifa kiholela, na hivyo kubana ufanisi wa vyombo vya habari.

Sheria mbili za hivi karibuni zinazogusa uhuru wa kujieleza na vyombo vya habari ni Sheria ya Takwimu na Sheria ya Makosa ya Mtandao, zote zikiwa zimepitishwa mwaka 2015. Sheria ya Takwimu inazuia taasisi yoyote, ikiwa ni pamoja na mashirika yasiyo ya serikali, kufanya utafiti wowote wa takwimu bila kupata

[17]. Agano la Kimataifa la Haki za Kiraia na za Kisiasa (ICCPR), Tume ya Umoja wa Mataifa wa Haki za Binadamu, Maelezo Na. 34 ibara 16: "Nchi wanachama wahakikishe kuwa vyombo vya matangazo vya umma vinafanya kazi katika mazingira huru. Hivyo basi, nchi wanachama zinapaswa kuvihakikishia uhuru wao na uhuru wa kiuhariri. Vyombo hivyo vipatiwe fedha kwa namna isiyoingilia uhuru wao"; Tamko la Kanuni za Uhuru wa Kujieleza Barani Afrika: Utangazaji kwa Umma, kifungu VI. :- "vyombo vya habari vya kitaifa au kiserikali vibadilishwe kuwa vyombo vya umma (…) viongozwe na bodi ambayo haitaingiliwa (…) vyombo vya habari vya umma vipatiwe fedha za kutosha kwa namna inayo vilinda kutokana na kuingiliwa kiholela bajeti zao… mamlaka na wajibu wa vyombo vya utangazaji vya umma yawekwe wazi na kuwe na jukumu la kuhakikisha kuwa umma unapata taarifa za kutosha za kisiasa zisizolenga upande wowote, hasa katika kipindi cha uchaguzi."

[18] Tamko la Kanuni za Uhuru wa Kujieleza Barani Afrika: Utangazaji kwa Umma, kifungu VII: "Mamlaka yoyote ya umma iliyo na uwezo katika maeneo ya usimamizi wa utangazaji au mawasiliano iwe huru ikiwa na ulinzi wa kutosha dhidi ya kuingiliwa, hususan kisiasa au kifedha (…) Mchakato wa uteuzi wa wajumbe wa mamlaka hizo uwe wazi, unaohusisha asasi za kiraia, na usitawaliwe na chama chochote cha siasa."

ridhaa ya mkurugenzi mkuu wa Shirika la Taifa la Takwimu na inafanya usambazaji wa "takwimu zisizo sahihi" kuwa kosa la jinai. Sheria ya Makosa ya Mtandao ina vipengele, kwa mfano kipengele 16, ambacho kinafanya utangazaji wa taarifa isiyo ya ukweli, iliyo ya uongo, ya kupotosha au isiyo sahihi kupitia kifaa cha elektroniki, kwa mfano kompyuta kuwa kosa la jinai na kosa hilo linaadhabu ya "faini isiyopungua Shilingi milioni tano au kufungwa kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu au vyote viwili", na sheria hiyo inatoa mamlaka makubwa mno kwa vyombo vya sheria katika kupekua na kunyang'anya taarifa au vyombo kabla ya kupata amri ya mahakama.

Mwanzoni mwa 2015, Bunge lilijadili, bila kupitisha, Miswada ya huduma ya Vyombo vya Habari na Upatikanaji wa Taarifa, iliyowasilishwa Bungeni pamoja na Sheria ya Makosa ya Mtamdao na Sheria ya Takwimu. Miswada hii miwili bado inasubiri kupitishwa. Wakati kuna haja ya kupitia upya sheria za vyombo vya habari, jambo ambalo vyombo vya habari na asasi za kiraia vimekuwa vikipigania kwa muda mrefu, hasa kuhusu kupatikana kwa sheria bora juu ya upatikanaji wa taarifa, miswada iliyowasilishwa Bungeni ina vipengele ambavyo vinabana uhuru wa vyombo vya habari na uhuru wa kujieleza na kubana na siyo kurahisisha upatikanaji wa taarifa. Wajadilianaji wa EU EOM walikua na maswali mazito juu ya miswada hii miwili.

Pamioja na uhuru wa kujieleza kuheshimiwa kwa kiasi kikubwa katika wiki kadhaa kabla ya uchaguzi na waandishi kuweza kufanya kazi katika mazingira ya uhuru, Sheria ya Makosa ya Mtandao ilionekana kwa maoni ya wajadilianaji wa jamii ya waandishi wa habari kuwa, kwa kiasi kikubwa, inaleta kujidhibiti katika uandishi kwenye mtandao. Muda mfupi baada ya uchaguzi, ilitumika pia dhidi ya Kituo cha Haki za Binadamu (LHRC) na pia dhidi ya CHADEMA kutokana na shughuli zao zinazoendana na kukusanya na kuchambua maoni ya uchaguzi na fomu za matokeo (ona Mazingira Baada ya Uchaguzi Tanzania Bara). Pia, Novemba 11, Tume ya Utangazaji ya Zanzibar ilisimamisha leseni ya utangazaji ya kituo cha redio kilichopo Visiwani humo cha Swahiba FM kwa miezi miwili kutokana na matangazo yake yaliyorushwa moja kwa moja tarehe 26 Oktoba ya mkutano wa mgombea urais wa CUF na waandishi wa habari ambako mgombea huyo alitangaza kushinda urais.

*B. Mfumo wa Kisheria*

Sheria ya Taifa ya Uchaguzi na Sheria ya Uchaguzi Zanzibar zinawapa wagombea haki kutumia vyombo vya habari vya taifa wakati wa kampeni. Pia, Sheria ya Gharama za Uchaguzi inavihitaji vyombo vya habari vya taifa (Bara na Zanzibar) kutoa taarifa za mchakato wa uchaguzi bila upendeleo na kuwa vyombo hivyo havitampendelea au kumbagua mgombea yeyote. Sheria ya Utangazaji inasema kuwa wakati wa kampeni kila kituo cha utangazaji kitatoa muda wakutosha na fursa sawa katika utangazaji kwa vyama vyote vinavyogombea.

Pamoja na mfumo wa sheria unaosimamia shughuli za vyombo vya habari wakati wa uchaguzi, ambao hupatikana katika sheria kadhaa, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ilianza matumizi, mwezi Julai 2015, ya Kanuni ya Huduma za Utangazaji (Maudhui) (Urushaji Matangazo ya Kiuchaguzi ya Vyama vya Siasa) *[Broadcasting Services (Content) (The Political Party Elections Broadcasts) Code]*, zikiwa ni taratibu zitakazoongoza vyombo vyote vya utangazaji, ikiwa ni pamoja na vyombo binafsi, ili kuwe na utangazaji unaolingana kwa wagombea wote na mijadala yote ya siasa. Kanuni pia inavipengele juu ya uandishi mtandaoni na unasimamia wa jinsi taarifa zinavyotolewa, kwa mfano kwenye taarifa za habari, kwenye vipindi mambo leo na kwenye mijadala. Wakati kanuni inalenga kuhakikisha usawa katika upatikanaji wa taarifa, baadhi ya vipengele vinabana mno na wengi wa wajadilianaji wa jamii ya waandishi wa habari waliviona kuingilia uhuru wa uhariri. Mifano ni pamoja na kuhitajika kuahirisha kipindi cha mjadala iwapo mmoja wa wajadilianaji hajatokea, na kipengele kinacho sema kuwa vituo vinatakiwa kuuliza maoni ya wanaopiga simu kabla ya kuwarusha hewani kwenye vipindi vinavyotangazwa moja kwa moja ili kupata uwiano wa maoni. Utekelezaji wa kanuni kutowekwa bayana, hususan kwenye vipindi vinavyo rushwa moja kwa moja, ilipelekea baadhi ya vituo binafsi kusita kujihusisha na vipindi vinavyojumuisha

watazamaji/wasikilizaji na hii ilichangia kuwa na vipindi vyenye urasimu mkubwa wakati wa uchaguzi.

Tume ya Utangazaji Zanzibar, taasisi inayosimamia vyombo vya utangazaji Zanzibar, ilianza matumizi ya kanuni kama hizi ikiwa na vipengele karibu sawa, isipokuwa vipengele vinavyozungumzia maudhui mtandaoni, kitu ambacho ZBC haisimamii. Hata hivyo, kanuni hazikutumika wakati wa kampeni za uchaguzi, na kituo cha taifa cha ZBC, ambao EU EOM walikutana nao, walikuwa hawana ufahamu kuhusu kanuni hizo.

Mwezi Septemba 2015, Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) ilitangaza Kanuni za Utendaji kwa Vyombo vya Habari zikielezea wajibu wa vyombo vya habari Zanzibar katika kipindi cha kampeni, ikiwa ni panoja na masharti ya uandishi usiofungamana na wajibu wa vyombo vya habari vya taifa kuhakikisha kuwa wagombea wote, na vyama vyote vinavyogombea uchaguzi Zanzibar, wanapata nafasi sawa. Kanuni za Utendaji zililazimisha kuwepo na muda wa kutolewa bure kwenye vyombo vya habari vya taifa kwa wagombea wakati wa kampeni, ratiba ikiwa imekubaliwa na vyama vya siasa na ZEC kabla ya kampeni kuanza. Vyama vya siasa vilivyokuwa vikigombea nafasi ya urais vilitakiwa kupata dakika 25 bure kwenye redio na televisheni kila wiki, na vyama vingine vilitakiwa kupata dakika 15 kila wiki. Kila chama kilichogombea kilipewa uwezo wa kutumia nusu ukurasa kwenye magazeti ya taifa kila wiki. Vyama havikuonyesha kutaka kutumia nafasi ya bure kwenye magazeti na vingine havikutumia haki yao ya muda wa bure kwenye redio na televisheni ya taifa. Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) lilikuwa, wakati mwingine, likitangaza ujumbe wa kampeni wa vyama nje ya ratiba iliyokubalika, bila kufuata ratiba ilivyopangwa kabla ya kuanza kwa kipindi cha kampeni. Chama cha CUF kilidai kuwa hili liliathiri uwezo wake kuwafikia watazamaji na wasikilizaji.

Kwa uchaguzi wa Jamhuri ya Muungano, Tume ya Uchaguzi ya Taifa (NEC) haikuwa na kanuni zozote za kuongoza shughuli za vyombo vya habari, kinyume na chaguzi zilizopita, na haikuhusika moja kwa moja katika mchakato wa kutoa muda wa bure kwa wagombea. Muda wa bure ulitolewa na Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC), ambalo pia lilirusha vipindi vifupi vya kuelezea hiistoria ya wagombea urais katika kipipndi cha wiki mbili kabla ya uchaguzi. Kwa mujibu wa TBC, vyama vya siasa vilivyokuwa na wagombea wa urais vilipatiwa masaa matatu bure mwanzo wa kipindi cha kampeni. Kinyume na matakwa ya sheria yanayotaka kutolewa muda sawa kwa wagombea wote, utangazaji wa TBC wa mikutano ya mwisho ya kampeni, ikitangaza mikutano ya CCM na CHADEMA tu, ilinufaisha CCM kwa sababu mkutano huo ulionyeshwa kwa kiasi kikubwa na muda uliyokuwa na watazamaji wengi, kulinganisha na utangazaji mdogo zaidi uliyotolewa kwa mkutano wa mwisho wa CHADEMA. Kwa ujumla, vipindi vilivyotolewa bure kwa vyama vya siasa vilikuwa vichache, hususan muda uliyotolewa kwa vyama vidogo ambavyo havikuwa na uwezo wa kununua muda kwenye vyombo vya habari.

### *C. Utangazaji wa Uchaguzi na Uangalizi wa Vyombo vya Habari wa EU EOM*

EU EOM ilianza shughuli za uangalizi wa vyombo vya habari tarehe 21 Septemba. Sampuli ya vyombo 16 vilivyoangaliwa ni pamoja na vituo vya televisheni vya taifa vya Shirika la Utangazaji wa Taifa (TBC1) na Televison Zanzibar, na mashirika binafsi ya Independent Televison (ITV), Channel 10, Star TV na TV Azam 2. Vituo vya taifa vya redio vilivyoangaliwa vilikuwa vya Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC Taifa) na Radio Zanzibar, na vituoa binafsi vya Radio Free Africa na Radio One. Magazeti yaliyokuemo kwenye sampuli hiyo yalikuwa magazeti ya taifa ya Daily News na Zanzibar Leo na magazeti binafsi ya kila siku Mwananchi na Nipashe pamoja na magazeti binafsi ya kila wiki ya Mwana Halisi na Raia Mwema.

Uchaguzi, haswa haswa uchaguzi wa urais, ulitawala matangazo na magazetini, taarifa za wahariri zikiwa zimelenga kampeni za wagombea wakuu. Wapiga kura waliweza kupata maoni mbali mbali kupitia vyombo vya habari, hasa kutokana na uwingi wa vyombo vya habari Tanzania Bara. Hata hivyo, kulikuwa na uandishi mchache wa kukosoa na kujadili sera za kisiasa, vyombo vingi vikiwa tu vinarudia jumbe za kampeni za vyama. Hali chanya ilikuwa kawaida kwenye taarifa nyingi za kampeni za wagombea, hususan kwenye taarifa za habari. Ratiba zilizobanana za vyama vikuu ilikuwa ni changamoto kwa vyombo vya habari. Ni

vituo vichache, kama vilikuwepo, ambavyo viliweza kuwapatia waandishi wake uwezo wa kuongozana na vyama kwenye kampeni. Waandishi mara nyingi hupewa usafiri na posho na vyama vya siasa, na hutegemewa kutoa taarifa njema. Hili linaelezea, kwa kiasi angalau, kuwa na taarifa njema na za kutokabiliana na vyama vya siasa kwenye vyombo vya habari. Mwishoni mwa mwezi Septemba, muandishi anayefanya kazi na Mwananchi aliondolewa kwenye kundi la waandishi waliokuwa wakiongozana na kampeni ya urais ya CCM baada ya kutoa taarifa ambayo CCM iliiona kuwa haiwafai.

Kwa upande wa muda na nafasi ya kulipiwa, CCM ilitawala kama ilivyoonekana kwenye uangalizi wa vyombo vya habari. Vyama vya UKAWA pia vilitumia fursa kuweka ujumbe wa kulipia kwenye vyombo vya habari, lakini kwa kiwango kidogo zaidi sana. Kwa kuwa vipindi havikuelezwa kuwa hivyo, ilikuwa vigumu kwa watazamaji kuelewa kama kipindi kiliandaliwa na waandishi wa kituo au kilikuwa ni kipindi cha kulipiwa cha chama cha siasa.

Matokeo ya uangalizi wa EU EOM wa vyombo vya habari ulionyesha kushindwa kwa vyombo vya habari vya taifa kutii masharti ya sheria juu ya usawa wa utoaji taarifa za kampeni, kwani walilenga zaidi utoaji taarifa za chama tawala. Televisheni na Redio ya Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC) zilitoa asilimia 63 kwenye televisheni na asilimia 53 kwenye redio za muda wake, katika wakati wa watazamaji na wasikilizaji wengi, kwa utangazaji wa vyama vya siasa na wanasiasa kwa CCM. Vivyo hivyo, televisheni na redio za Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) zilitoa asilimia 70 (televisheni) na asilimia 72 (redio) kwa taarifa zinazohusu CCM, wakati vyama vingine, kwa pamoja, vikipata asilimia 15 (televisheni) na asilimia 11 (redio). Muda uliyobaki kote TBC na ZBC ulitolewa kwa watendaji wa serikali - marais, makamu wa rais na viongozi wengine wa serikali zote mbili, baadhi yao wakiwa ni wagombea, - pamoja na shughuli zao za kikazi. TBC TV na redio zilitoa asilimia 18 (televisheni) na asilimia 29 (redio) na ZBC ilitoa asilimia 15 (televisheni) na asilimia 17 (redio) ya muda wa matangazo kwenye taarifa za habari kwa matukio haya. Kwenye vipindi vingine vilivyotangazwa na vyombo vya habari vya taifa, kiwango kilichotolewa kwa CCM kilikuwa kikubwa zaidi (Ona AnnexII: Matokeo ya Uangalizi wa Vyombo vya Habari).

Ya kutia moyo, baadhi ya vituo binafsi vilionyesha usawa zaidi katika utoaji taarifa za kampeni. Pamoja na kuwa nao pia walilenga zaidi wagombea wakuu, CCM na CHADEMA, mgawanyo wao wa muda ulikuwa wakulingana zaidi, na vyama kadhaa pia vilipewa muda hewani. TV Azam 2 ilitoa asilimia 37 ya muda wake kwa taarifa za CCM wakati CHADEMA ikipata asilimia 25, ACT ilipewa asilimia 8 na CHAUMMA ilipata asilimia 4. Kulingana na vyombo vingine, TV Azam 2 ilitoa muda mwingi zaidi kwenye vipindi maalum vya uchaguzi kwa wagombea, pamoja na waliyokuwa wakigombea nafasi za ubunge. Vyama vitatu; ACT, CCM na CHADEMA kila kimoja kilipewa takriban robo ya muda katika vipindi hivi. ITV na Radio One, vyote vikiwa ni vituo vya IPP Media, pia vilitoa utangazaji wa kulingana wa vyama vya siasa na wagombea. ITV iliipatia CCM asilimia 33 na CHADEMA asilimia 29 ya muda kwenye taarifa za habari, wakati Radio One ikitoa asilimia 27 kwa CCM na asilimia 20 kwa CHADEMA kwenye taarifa zake za habari. Vipindi vingine vilivyoandaliwa na ITV vilionesha ulingano kama huo, ingawa uchambuzi wa kina ulionyesha kuwa baadhi ya waandishi walikuwa wanaegemea CHADEMA.

Star TV na Radio Free Africa vilikuwa na utangazaji uliofanana na uliyotolewa na vyombo vya habari vya taifa. Vyote vililenga zaidi CCM, iliyopata asilimia 50 (Star TV) na asilimia 63 (Radio Free Africa) ya muda kwenye taarifa za habari, wakati CHADEMA ilipatia asilimia 10 ya muda kwenye habari kwenye vituo vyote viwili vya Sahara Media Group. Channel 10 pia ilitoa muda mkubwa kwa CCM, asilimia 42, wakati CHADEMA ilipata asilimia 23, na kiasi kikubwa cha muda uliyobaki ukionyesha shughuli za viongozi wa serikali. Vipindi vingine vilivyoandaliwa na Channel 10 vilikuwa na ulingano wa muda vikiwa vimetoa asilimia 38 ya muda kwa CCm na CHADEMA.

Gazeti la serikali, Zanzibar Leo, lilitoa kiasi kikubwa cha taarifa zake, asilimia 71, kwa CCM, wakati vyama vingine vya siasa kwa pamoja vilipata asilimia 10. Gazeti la serikali la Daily News pia lililenga zaidi CCM, ingawa taarifa zake za vyama vingine kwa pamoja ilikuwa ni kubwa zaidi, asilimia 27. Ukilinganisha, gazeti

binafsi la Nipashe lilitoa viwango vinavyo karibia kulingana zaidi kwa CCM na vyama vya upinzani, wakati gazeti binafsi la Mwananchi lilitoa nafasi kubwa kwa viama vingi zaidi. Gazeti binafsi la kila wiki la Raia Mwema pia lilitoa uwingi wa taarifa kwa wanasiasa na vyama vikuu, wakati gazeti binafsi la kila wiki la Mwana Halisi liliegemea kwa CHADEMA huku likiwa na taarifa za kukosoa CCM. Magazeti yote mawili ya kila wiki yalikuwa na taarifa za uchambuzi zaidi kulinganisha na vyombo vingine vya habari vilivyoangaliwa.

TCRA ilipokea malalamiko machache kuhusiana na shughuli za vyombo vya habari katika kipindi cha uchaguzi, lakini maelezo ya malalamiko hayo hayakutolewa kwa EU EOM. Wakati vyombo vya habari vilitakiwa kuitaarifu TCRA juu ya mipango yao ya matangazo ya uchaguzi, kwani TCRA ilikuwa ikifuatilia taarifa zilizokuwa zikitolewa na vyombo vya habari juu ya uchaguzi, TCRA haikuwa imeshughulika sana katika kipindi cha uchaguzi na ilishindwa kufuta upendeleo kwenye utoaji taarifa kwa vyombo vya habari vya taifa na baadhi ya vyombo binafsi.

## XI. Ushiriki wa Wanawake, Vikundi vya Wachache na Watu Wenye Ulemavu

### *A. Ushiriki wa Wanawake*

Wanawake ni asilimia 53 ya wapiga kura waliyoandikishwa nchini Tanzania. Mmoja kati ya wagombea urais wa Muungano alikuwa ni mwanamke, aliyependekzwa na chama cha ACT. Kwa mara ya kwanza, CCM ilimpendekeza mwanamke kwa nafasi ya makamu wa rais ambaye alikuja kuchaguliwa pamoja na mgombea wa urais wa CCM. Pamoja na kwamba Katiba inatoa nafasi kwa wanawake kuchaguliwa kwenye viti maalumu Bungeni, kwa sasa idadi ya viti isiyopungua asilimia 40 yaani viti 114[19], wanawake walikuwa na nafasi chache katika chaguzi za majimbo. Kulikuwa na wanawake 233 kati ya wagombea 1,218 waliyokuwa wakigombea viti vya majimbo 264 kwenye Bunge la Muungano na wanawake 679 kati ya wagombea 10,879 waliokuwa wakigombea nafasi katika manispaa na serikali za mitaa. Kwenye Bunge la Muungano, wagombea 26 kati ya wagombea wanawake 233 walichaguliwa: 18 wa CCM, 7 wa CHADEMA na mmoja wa CUF. Kiwango cha wanawake kimeongezeka kidogo tu kulingana na uchaguzi uliyopita; kutoka asilimia 18.4 kwenda asilimia 19.1.

Hakukuwa na mgombea urais mwanamke Zanzibar. Wanawake 29 kati ya wagombea 180, wakiwa asilimia 16, waligombea viti vya majimbo katika Baraza la Wawakilishi. Wanawake pia walichaguliwa kwenye viti maalumu kwenye Baraza la Wawakilishi. Alliance for Democratic Change (ADC) ilipendekeza 9, idadi kubwa zaidi ya wanawake, ikifuatiwa na CCM ikiwa na wagombea 7 na CUF ikiwa na wagombea 5. ACT ilipendekeza 3, Tanzania Democratic Alliance - TADEA na Demokrasia Makini walipendekeza wawili kila chama na CHAUMMA walipendekeza mmoja.

Viti maalum vinagawiwa kwa vyama vinavyopata angalau asilimia 5 ya kura zilizopigwa kwa wagombea ubunge na asilimia 10 ya kura zilizopigwa kwa Baraza la Wawakilishi. Kuendana na matokeo ya uchaguzi wa Bunge la Muungano, CCM ilipatiwa viti 64, CHADEMA 36 na CUF viti 10, wakati viti vitatu vilivyobaki viligawiwa baada ya uchaguzi kufanyika katika majimbo 8 ambako uchaguzi uliahirishwa. Mpaka ripoti hii inaandikwa, matokeo ya Zanzibar yalikuwa bado hayajulikani.

Waangalizi wa EU walieleza kuwepo kwa idadi kubwa ya wanawake kwenye mikutano ya kampeni, hususan ile ya CCM, lakini, kulikuwa na idadi ndogo ya wagombea wanawake na walyiozungumza kwenye mikutano hiyo. Katika vituo vya kupiga kura vilivyoangaliwa, asilimia 40 ya wakuu wa vituo na asilimia 51 ya wasaidizi walikuwa wanawake. CCM iliteua idadi kubwa kuliko wengine ya wanawake kuwa mawakala wake ikiwa ni asilimia 31, ikifuatiwa na CHADEMA yenye asilimia 16, ACT ikiwa na asilimia 12 na CUF iliyokuwa na asilimia 9.

[19] Tamko la SADC juu ya Maendeleo na Jinsia, 1997, kifungu (i): wanachama wa SADC [wameridhia] "kuhakikisha uwakilishwaji sawa wa wanawake na wanaume(…) na kufanikisha kufikiwa kwa lengo la kuwa na angalau wanawake asili mia 30 kwenye mifumo ya siasa na madaraka ifikapo mwaka 2005."

*B. Ushiriki wa Vikundi vya Wachache*

Jamii ya Wamasai inakumbana na changamoto kubwa kwenye swala la kuhusika katika mchakato wa uchaguzi na kufikia na kuwakilishwa katika vyombo vya utawala. Maisha yao ya kuhama hama, umbali wa makazi yao na uelewa wa lugha, kwani ni wachache wanaoongea Kiswahili, yaliwawazuia Wamasai wa vijijini kupata taarifa za kutosha kuhusu uchaguzi. Wamasai, na hasa wanawake wa kundi hili, wana uwakilishi duni katika tawala za kitaifa na kimkoa. Kulikuwa na wagombea 10 wa Kimasai, pamoja na mwanamke wa Kimasai mmoja, walyiogombea viti kwenye Bunge la Muungano.

*C. Watu wenye Ulemavu*

Tanzania imeridhia Mkataba wa Haki za Watu Wenye Ulemavu na kupitisha Sheria ya Watu Wenye Ulemavu mwaka 2010, ikihakikisha haki ya watu wenye ulemavu kupiga kura na kupigiwa kura. Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG), ikifuatilia mchakato wa uchaguzi, ilipokea malalamiko kutoka kwa watu wenye ulemavu juu ya uhaba wa elimu kwa wapiga kura, hususan kwa watu wasiyosikia. Hili pia lilikuwa ni tatizo wakati wa kujiandikisha kwani hakukuwa na wakalimani wa viziwi kwenye vituo vya uandikishaji. Karatasi za kupigia kura maalumu kwa wasiyoona zilikuwepo na pia sheria inaruhusu msaada waupigaji kura. Hakukuwa na uandikishaji maalum wala vituo maalum kwa watu ambao ulemavu wao unawazuia kuingia kwenye vituo vya uandikishaji au vya kupiga kura.

## XII. Utendaji wa Haki Kiuchaguzi

Kwa Katiba ya Tanzania ya serikali mbili, Jamuri ya Muungano na Zanzibar zina mahakama tofauti isipokuwa Mahakama ya Rufaa peke yake inayotumikia pande zote mbili. Mfumo wa sheria kwa kiasi kikubwa umerithi mfumo wa sheria ya Uingereza ikitoa nafasi kwa sheria za Kiislamu na za kimila.

Mahakama ya Rufaa, yenye majaji watano, ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inayoongozwa na Jaji Mkuu, inashughulikia rufaa kutoka Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano pamoja na kutoka Mahakama Kuu ya Zanzibar, isipokuwa kwa kesi zinazohusu Katiba ya Zanzibar na maswala ya sheria za Kiislamu zilizopo Zanzibar. Mahakama Kuu za Muungano na Zanzibar zina mamlaka juu ya maswala ya kikatiba na pia zinasikiliza kesi za uchaguzi za Muungano na Zanzibar kutoka mahakama za chini za pande zote mbili.

*A. Makosa ya Kiuchaguzi*

Makosa ya kiuchaguzi yameelezwa kwenye sura ya 6 ya Sheria ya Uchaguzi ya Taifa kwa chaguzi za Muungano na sura ya 7 ya Sheria ya Uhcaguzi na. 11 kwa chaguzi Zanzibar. Makosa ni pamoja na kujiandikisha mara mbili, kutoa taarifa za uongo juu ya sifa za kujiandikisha au kupendekezwa, utovu wa nidhamu kwa wasimamizi wa uchaguzi, kughushi daftari la wapiga kura au vitambulisho vya wapiga kura, kuwa na makaratasi ya kupigia kura kinyume cha sheria, kutotunza usiri wa kura, hongo, kujifanya mtu mwingine na kushinikiza wapiga kura, na mengine. Adhabu ni pamoja na kutozwa faini na/au kufungwa kwa kipindi cha hadi miaka mitano.

Kutokana na kuwa na asili ya makosa ya jinai, makosa ya kiuchaguzi yanashughulikiwa na mfumo wa kawaida wa kimahakama, mahakama za wilaya zikiwa sehemu ya kwanza kutoa hukumu ambazo zinaweza kukatiwa rufaa Mahakama Kuu. Zaidi ya kesi 40 za makosa ya kiuchaguzi zilifikishwa kwenye mahakama za wilaya za Muungano kabla na mara baada ya uchaguzi. Zilihusu zaidi lugha chafu, kukutwa na nyaraka/vifaa kinyume na sheria, kujiandikisha mara mbili na uharibifu wa vifaa vya kampeni uliyofanywa na wagombea na wafuasi wa CCM na CHADEMA.

Wakati ripoti hii ikiandikwa, kumekuwa na zaidi ya kesi 40 zinazopelelezwa na polisi juu ya matukio yaliyotokea kabla na baada ya uchaguzi, ambapo baadhi ya kesi zimepelekea kukamatwa kwa wafuasi wa vyama (zaidi wa CHADEMA) na wagombea wa CHADEMA, ambao inasemekana wameachiwa kwa dhamana.

Pamoja na kuwa katika kipindi cha uchaguzi vyama vingi vilipongeza jeshi la polisi kwa ufanisi wa kazi kwenye mikutano ya kampeni, kwenye baadhi ya maeneo, vyama vya upinzani vilieleza wasiwasi wao juu ya kukamatwa na kuwekwa kizuizini wagombea na wafuasi wao kwa tuhuma za kuleta vurugu.

Kabla ya siku ya uchaguzi, wagombea sita wa ubunge wa CHADEMA walikamatwa kwenye wilaya za Dodoma, Iringa, Morogoro, Katavi na Mara. Mgombea wa Dodoma Mjini, Benson Kigaila, alikamatwa tarehe 25 Septemba na kuachiwa kwa dhamana kwa tuhuma za kufanya maandamano kinyume na taratibu na kwa lugha chafu. Wafuasi kumi pia walishitakiwa kwa kuwa na nyaraka kinyume cha sheria na kwa shambulizi, wawili kati yao pia wakishitakiwa kwa shambulizi lililoleta madhara ya kimwili kwa afisa wa polisi. Mgombea ubunge wa Iringa Mjini, Mch. Peter Msigwa, alishitakiwa kwa uchochezi. Mgombea wa Mpanda Mjini, Jonas Kalinde, alishitakiwa kwa maandamano bila kibali. Mgombea huyo alikuja kushinda kiti cha ubunge. Mgombea wa Morogoro Mjini, Mascossy Albanie Mathew, alishitakiwa mwezi Septemba kwa kosa la kuanzisha kikosi cha mgambo ndani ya chama chake na kwa kuleta vurugu. Kesi hiyo iliyopangwa kusikilizwa tarehe 9 Oktoba, iliahirishwa. Wakati wakuandika ripoti hii, kesi hizi zote zilikuwa zikisubiri kusikilizwa. Mgombea wa ubunge wa Kilombero, Esther Bulaya, alikamatwa kwa tuhuma za shambulizi la kimwili na baadhi ya wafuasi wake pia walishitakiwa kwa kosa la wizi wa kutumia silaha. Aliachiwa baada ya siku tatu bila kufunguliwa mashitaka.

Sheria ya Muenendo wa Makosa ya Jinai inampa mkuu wa kituo cha polisi mamlaka ya kuamua muda wa kushikiliwa mtuhumiwa, hivyo kuleta uwezekano wa kutokea na watu kuwekwa kizuizini kwa muda mrefu kiholela. Zaidi, Sheria ya Tawala za Mikoa inawapa wakuu wa wilaya mamlaka ya kuamrisha kukamatwa mtu bila hati ya mahakama na kwa mtu huyo kuwekwa kizuizini kwa muda usiozidi masaa 48. Kwa hiyo basi, mfumo wa sheria unatoa mamlaka makubwa wa kukamata kwa polisi na watendaji walioteuliwa kisiasa.

*B. Kamati za Maadili*

Kamati za Maadili, zilizoelezewa kwenye Kanuni ya Maadili kwa Vyama vya Siasa na zenye uwezo wa kusimamia utekelezaji na heshima kwa maelekezo ya kanuni, zimeanzishwa katika ngazi ya kata, jimbo na taifa. Kamati ya Rufaa inawajibu wa kusikiliza rufaa kutoka Kamati ya Maadili ya Taifa. Wanakamati wanakuwa ni watumishi wa Tume ya Uchaguzi ya Taifa, wawakilishi kutoka serikalini na vyama vya siasa. Lalamiko linaweza kuwasilishwa katika ngazi yoyote na, kama mtu hajaridhika na matokeo, jambo linaweza kupelekwa mahakamani. Malalamiko matatu yaliwasilishwa kwenya Kamati ya Maadili ya Taifa juu ya tuhuma za uharibifu wa vifaa vya kampeni, uvunjaji wa ratiba ya kampeni na kuomba kura kwa msingi ya dini. Malalamiko matatu yote yalipatiwa suluhisho na maamuzi kukubalika na vyama vya siasa.

Waangalizi wa Uchaguzi wa EU waliripoti kuwa malalamiko takriban 25 yaliwasilishwa kwenye Kamati za Maadili nchini, zaidi kwenye maswala kama uharibifu wa vifaa vya uchaguzi, kupitiliza masaa ya kampeni na lugha chafu kutumika wakati wa mikutano ya kampeni. Mengi ya malalamiko yalisuluhishwa na yaliyobaki kupelekwa kwa vyombo husika, yaani Tume ya Uchaguzi ya Taifa, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na polisi.

Katika majimbo mengi, Baraza za Maadili zilianzishwa na kuonekana kwa vyama vya siasa kuwa ni chombo kinachofaa kutatua migogoro midogo midogo. Hata hivyo, uwezo wa kamati hizi kama chombo cha dharura cha usuluhishi ulihojiwa mara nyingi na, katika baadhi ya maeneo nchini, migogoro ya kampeni ilisuluhishwa ama baina ya wahusika na wasimamizi wa uchaguzi bila haja ya kuhusisha wala kuanzisha hizi kamati, au kwa usuluhishi wa mamlaka nyingine kama vile wakuu wa wilaya.

*C. Malalamiko na Rufaa*

Tume ya Uchaguzi ya Taifa na Tume ya Uchaguzi Zanzibar zina madaraka ya kutatua malalamiko na rufaa katika ngazi zote za utawala wa uchaguzi kwa kesi za madai. Pamoja na kuwa katiba zote mbili na sheria zake zinasema kuwa maamuzi ya tume hizo mbili ni ya mwisho, katiba hizo mbili pia zinatoa madaraka bila

mipaka kwa Mahakama Kuu na uwezekano wa kupitiwa upya kimahakama maamuzi yoyote yanayofikiwa na taasis za umma, ikiwemo taasisi za usimamizi wa uchaguzi. Lakini mchakato huu haujatumika kwa hiyo mahakama hazijaweza kutoa tafsiri ya kisheria ambazo zingetoa uhakika juu ya uwezekano wa kupinga maamuzi ya NEC na ZEC.

Kwa mujibu wa sheria, rufaa za maamuzi ya NEC na ZEC kuhusu upendekezaji wa wagombea wa Bunge zinaweza kupelekwa Mahakam Kuu baada ya kutangazwa matokea ya uchaguzi na si kabla. Kipengele hiki hakitoi fursa kwa mlalamikaji kupata suluhisho mapema la lalamiko lake. Mifumo ya kisheria ya Muungano na Zanzibar haina mchakato wa kukata rufaa kupinga maamuzi ya NEC na ZEC kukataa kupendekezwa mgombea wa urais.

Kwa kushughulikia malalamiko ya uchaguzi Zanzibar, ZEC haikuwa na utaratibu rasmi. CUF iliwasilisha malalamiko rasmi 12 kwa ZEC. Yalikuwa yanahusu kupata nakala ya daftari la wapiga kura Februari 2015; kutokuwa na uhakika wa mipaka mipya ya shehia na kata; na lalamiko dhidi ya afisa muandikishaji msaidizi wa wilaya ya Micheweni kwa sababu za kufungamana na upande mmoja. Malalamiko mengine yalikuwa juu ya kituo kimoja cha uandikishaji kilichotuhumiwa kuwepo kwenye kambi ya Kikosi cha Valantia Zanzibar (KVZ) na kingine ndani ya kambi la jeshi; tuhuma za makosa ya uandikishaji wapiga kura kwa kuandikisha watu wasiyo na sifa; pamoja na tuhuma ya wafuasi wa CCM kuvuruga mkutano wa CUF. Pia kulikuwa na wasi wasi ulioelezwa kwa ZEC juu ya ukusanyaji wa kadi za wapiga kura na kama maelezo ya kadi za wapiga kura ziliendana na mipaka mipya ya majimbo. Tarehe 17 Septemba, CUF iliwasilisha lalamiko rasmi kwa ZEC juu ya tuhuma ya usambazaji wa kadi za kupigia kura uliotuhumiwa kufanywa na masheha kabla ya kufunguliwa rasmi vituo vya ugawaji, wakituhumu mamlaka ya uchaguzi kuipendelea CCM. Vile vile, baada ya kumalizika kwa zoezi la siku tatu la usambazaji wa kadi za wapiga kura, CUF walilalamika kuwa wafuasi wake wengi Pemba hawakupata kadi zao pamoja na kuonyesha vitambulisho vyao vya Zanzibar na stakabadhi ya kulipia kadi ya mpiga kura. ZEC ilijibu baadhi ya haya malalamiko kwa maandishi; kesi nyingine zilishughulikiwa kwa mikutano ya pande husika au kwenye mkutano mmoja pekee wa Kamati ya Maadili uliyofanyika.

Malalamiko takriban 25 yaliwasilishwa NEC mengi yakiwa juu ya matatizo katika kupendekeza majina, makosa wakati wa uandikishaji wapiga kura na tuhuma ya upendeleo kwa wasimamizi wa uchaguzi. Siku ya uchaguzi, malalamiko machache sana yalitolewa kwenye vituo vya kupiga kura vilivyokuwa vinaangaliwa na EU EOM na malalamiko hayo yalishughulikiwa kufuatana na kanuni. Malalamiko mawili pia yalitolewa baada ya uchaguzi kuhusiana na kuorodhesha takwimu: lalamiko moja lilitolewa na mgombea wa CCM kwa tuhuma za kuchezea matokeo ya Banda Mjini, ikiwa na ombi la kutotangaza matokeo kabla ya kuhesabiwa upya kura - kesi ilifunguliwa kupinga matokea haya; na nyingine ya mgombea wa CHADEMA, wakala wa TADEA na wakala wa AFP wakituhumu makosa wakati wa kukusanya na kuorodhesha takwimu Musoma Mjini.

Kesi iliwasilishwa Mahakama Kuu tarehe 16 Oktoba na mgombea wa CHADEMA akidai kuwa agizo lililotanganzwa la NEC kuwa haruhusiwi mtu yeyote kuwa katika eneo la mita 200 ya kituo cha kupiga kura ni kinyume na Katiba. Mgombea huyo alikuwa anataka tafsiri ya vipengele vya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi iliyotajwa na NEC, na alidai kuwa NEC ilikuwa inakiuka haki ya watu kufuatilia mchakato wa uchaguzi na kuwepo wakati matokeo yanapotangazwa. Mahakama ilitoa maamuzi tarehe 23 Oktoba, maamuzi ambayo yalithibitisha kuwa tangazo la NEC lilikuwa linaendana na Katiba.

*D. Malalamiko ya Kichaguzi*

Mifumo ya kisheria ya Muungano na Zanzibar haitoi fursa kupinga matokeo ya uchaguzi wa rais, kinyume na misingi ya kidemokrasia ya kimataifa iliyoko kwenye Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Uraia na Siasa. [20] Vinavyoweza kupingwa ni uhalali wa uchaguzi wa Bunge la Muungano na Baraza la Wawakilishi tu kupitia Mahakama Kuu ya Muungano au ya Zanzibar, na kwa kesi zinazohusu chaguzi za madiwani kupitia mahakama za hakimu mkazi. Kesi za kupinga matokeo ya uchaguzi wa Bunge la Muungano na Baraza la Wawakilishi lazima ziwasilizhwe katika kipindi sha siku 30 kwa kesi za Bunge na siku 14 kwa kesi za Baraza la Wawakilishi baada ya kutangazwa matokeo. Mahakama Kuu lazima zitoe maamuzi katika kipindi cha miezi 12 kwa matokeo ya Bunge la Muungano na miaka miwili kwa matokeo ya uchaguzi wa Baraza la Wawakilishi. Muda huo wa miaka miwili kwa Mahakama Kuu ya Zanzibar kutoa maamuzi juu ya pingamizi ya matokeo ya uchaguzi ni mrefu sana kulinganishwa na miezi 12 kwa kesi za Muungano.

Gharama za kufungua kesi ya kupinga matokeoa ya uchaguzi kwenye Mahakam Kuu ni TZS200,00 (Euro 86) na kwenye Mahakama ya Hakimu Mkazi ni TZS100,000 (Euro 43). Zaidi ya hayo, muombaji lazima awasilishe maombi kwa mahakama kuamua kiwango cha dhamana itakayokidhi gharama za uendeshaji kesi katika kipindi kisichozidi siku 14 baada ya kuwasilisha pingamizi yake mahakamani. Kiwango kitakachoamuliwa na mahakama kisizidi TZS milioni 5 (Euro 2,100). Maamuzi anayoweza kupata muombaji ni tamko la mahakama kubatilisha uchaguzi, tamko la kubatilisha jina la mgombea lililopendekezwa au kutangaza mshindi mwingine au uchunguzi.

Wakati wa kuandika ripoti hii, kesi 51 za kupinga matokeo ya uchaguzi wa Bunge zimewasilishwa Mahakama Kuu ya Jamhuri wa Muungano, zikiwemo za Iringa Mjini, Tanga Mjini, Jimbo la Buyungu mkoani Tabora, Longido iliyopo Arusha na Mbagala Dar es Salaam. Kesi zingine ziliwasilishwa baada ya kupita kwa kipindi cha siku 30. Mahakama iliiomba NEC kuthibitisha tarehe matokeo yalipotangazwa katika hayo majimbo ili kuweza kuendelea na taratibu zinazohitajika. Zaidi ya hayo, kuna kesi 155 zinazopinga matokeo ya chaguzi za madiwani ambazo zimewasilishwa kwenye mahakama za mahakimu wakazi za Muungano.

Mafunzo kwa mahakimu yaliandaliwa na UNDP kupitia Mradi wa Uwezeshaji wa Kidemokrasia (DEP). Jumla ya mahakimu 84 walipewa mafunzo juu ya kusikiliza kesi za uchaguzi ili kuongeza uwezo wa mahakama katika usuluhishi migororo na kuwezesha kesi kusikilizwa kwa viwango vikubwa na haraka zaidi. Mafunzo kwa mahakimu wakazi na maafisa usajili wa mahakama yalifanyika baada ya uchaguzi, kuanzia tarehe16 hadi 19 Novemba. Lengo likiwa kuweza kushughulikia kesi zote za uchaguzi katika kipindi cha miezi 6.

## XIII. Jamhuri ya Muungano Tanzania - Siku ya Upigaji Kura na Kipindi

*A. Upigaji Kura na Kufunga Vituo*

Tarehe 25 Oktoba, uchaguzi ulifanyika kuanzia saa 1 asubuhi hadi saa 10 jioni. NEC iliongeza idadi ya vituo vya kupigia kura kutoka 51,572 mwaka 2010 hadi 65,105 kutokana na idadi kubwa ya wapiga kura waliojiandikisha. Vituo vilivyotumika kwa zoezi la uandikishaji vilitumika kama vituo vya kupigia kura pamoja na sehemu zingine. Kila kituo cha kupigia kura kilipangiwa wapiga kura wasiozidi 450, na wasimamizi watatu, na nje ya kituo karani mmoja wa kuongoza wapiga kura na askari mmoja wa usalama. Vyama vya siasa viliruhusiwa kuteua wakala mmoja kwa kila kituo.

Siku ya uchaguzi, waangalizi wa EU walifuatilia taratibu za upigaji kura kwenye vituo 625 katika mikoa yote nchini. Muenendo wa upigaji kura ulionekana kuwa mzuri katika asilimia 96 ya vituo vya upigaji kura

[20] Ibara 2 ICCPR, Tume ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Binadamu, Maelezo ya Jumla Na. 25, ibara 20: “Kuwe na uangalizi huru wa mchakato wa upigaji kura na kuhesabu na uwezo wa kupata utatuzi wa kimahakama au mchakato unaolingana nao ili wapiga kura wawe na imani juu ya usalama wa kura na kuhesabu,” na Tamko la Umoha wa Afrika Kuhusu Kanuni Zinazosimamia Chaguzi za Kidemokrasia Afrika, kifungu IV.7, kisemacho kuwa “Watu au vyama vya siasa watakuwa na haki ya kukata rufaa na kupata fursa ya kusikilizwa kwa wakati dhidi ya hitilafu zote za kiuchaguzi zilizothibitishwa, kupitia mamlaka zenye uwezo za kimahakama kulingana na sheria za kiuchaguzi za nchi”.

vilivyoangaliwa na EU EOM. Vituo vyote vilivyoangaliwa vilifunguliwa kwa wakati. Upigaji kura uliendeshwa katika mazingira yenye mpangilio na utulivu pamoja na kuwa na foleni ndefu zilizoripotiwa siku nzima. Taratibu za upigaji kura zilionekana kuwa na msimamo wa kulingana, na kuwawezesha wapiga kura kupiga kura kwa haraka na kwa mpangilio. Pamoja na kwamba mpangilio unaofaa wa vituo ulitumika kwa kiasi kikubwa, waangalizi wa EU waliripoti kutokuwa na kiwango cha kutosha sha kulinda usiri kwenye asilimia 21 ya vituo vilivyotembelewa, kutokana na mpangilio duni, usiyokuwa umekusudiwa, wa vituo hivyo. Wawakilishi wa vyama vya siasa walikuepo katika karibu vituo vyote vilivyoangaliwa wakati angalau muangalizi mmoja wa kitaifa alikuwepo kwenye asilimia 22 ya vituo hivyo. Waangalizi wa EU waliripoti matukio machache ya wawakilishi wa vyama vya siasa wakivuka mipaka ya mamlaka yao, pamoja na matukio ya karatasi za upigaji kura kutokuwepo kwa idadi ya kutosha kwenye vituo 11 na maelekezo ya taratibu kutokuwepo kwenye vituo 13.

Kwa jumla, taratibu za upigaji kura zilifuatwa kwenye vituo vya kupigia kura vilivyotembelewa na waangalizi wa EU, hii ikitoa uhakika wa kutosha wa uaminifu wa kura na uwazi wa mchakato wa upigaji kura. Ulinzi na kinga za upigaji kura na taratibu zilizowekwa kulinda usiri na uadilifu wa kura ilikuwa ni pamoja na kuwekwa picha kwenye orodha ya wapiga kura, kutmika wino usiyofutika kuweka alama kwenye vidole vya wapiga kura na masanduku ya kura yenye kuonyesha kilichomo ndani. Kinga za ziada zilikuwa ni kuweka kumbukumbu ya namba ya uandikishwaji ya mpiga kura kwenye vipande vya karatasi vilivyobaki kwenye kitabu baada ya kutoa karatasi za kupigia kura na karatasi za kupigia kura kupigwa mhuri pande mbili. Ufanisi wa wasimamizi wa upigaji kura kwa kiasi kikubwa ulioanekana kuwa mzuri sana.

Hata hivyo, kulikuwa na baadhi ya vituo ambako upigaji kura ilibidi uaihirishwe. NEC ilitangaza kurudiwa upigaji kura tarehe 26 Oktoba kwa uchaguzi wa urais na ubunge kufanyika kwenye vituo 35 Kinondoni mjini Dar es Salaam na kwenye vituo 15 Sumbawanga mkoani Rukwa. Kinondoni wasimamizi wa upigaji kura waliharibu karatasi za kura kutokana na mgogoro na NEC juu ya malipo yao kwa kazi zao siku ya kupiga kura. Kwenye kata ya Mitepa, Sumbawanga, wananchi walichoma moto karatasi za kura kutokana na tuhuma ya kuwepo kwa karatasi za kura zisizo halali. Zanzibar uchaguzi ilibidi usitishwe kwenye majimbo mawili ya uchaguzi kwa Baraza la Wawakilishi (Pangawe na Kijito Upele) kutokana na uhaba wa karatasi za kupigia kura. Uhaba wa karatasi za kupigia kura pia uliripotiwa kwenye majimbo ya Chukwani na Mombasa.

Pia upigaji kura kwa wabunge uliahirishwa awali kwenye majimbo 6 - Lushoto, Ulanga Mashariki, Arusha Mjini, Masasi, Ludewa na Handeni - na kwenye kata kadhaa kutokana na vifo vya wagombea. Sheria ya upigaji kura inasema kuwa msimamizi wa uchaguzi anatakiwa kuahirisha uchaguzi kwa jimbo hilo na NEC wanatakiwa kupanga tarehe nyingine, katika kipindi kisichozidi siku 30 tangu kuahirishwa kwa uchaguzi, kwa chama husika kupendekeza mgombea mwingine. Wagombea wengine hawahitajiki kuwasilisha upya majina yao. Pia, kwenye majimbo mawili, Lulindi na mji wa Masasi mkoani Mtwara, chaguzi za ubunge wa Muungano ziliahirishwa kutokana na ukosefu wa karatasi za kupigia kura na karatasi za kupigia kura kuwa na makosa ya uchapishaji.

*B. Kuhesabu na Kujumlisha Matokeo*

Zoezi la kuhesabu kura lilianza mara moja baada ya kufungwa kwa vituo kwenye asilimia 86 ya vituo vilivyotembelewa na zoezi lilifanyika wakiwepo mawakala wa vyama vya siasa na waangalizi. Uadilifu wa mchakato wa kuhesabu kura ulihakikishwa kwa kiwango cha kutosha. Nakala za fomu za matokeo zilionyeshwa wazi na kupewa kwa mawakala wa vyama vya siasa. Tathmini kwa jumla ya mchakato wa ufungaji na kuhesabu kura ilikuwa nzuri au nzuri sana kwenye asilimia 83 ya vituo vilivyoangaliwa na EU EOM, na tathmini ya uwazi wa mchakato kuwa ni nzuri au nzuri sana kwenye asilimia 88 ya vituo vilivyoangaliwa. Baadhi ya maeneo ya vituo havikuwa na umeme, jambo ambalo lilileta changamoto katika kuhesabu kura, hata kama kulikuwepo na taa zisizotumia umeme.

Kiwango cha uwazi na kuaminika kilikuwa kidogo zaidi kwenye kujumlisha kulinganisha na mchakato wa upigaji kura. NEC ilishindwa kuhakikisha kuwepo kwa taratibu zinazofanana za ukusanyaji na kujumlisha kura

kwenye mikoa yote. Miongozo iliyo wazi ya jinsi ya kuendesha zoezi la ukusanyaji na uhesabu wa kura na jinsi ya kushughulikia tofauti za kimahesabu haikutolewa na NEC kwa wasimamizi wa uchaguzi wala kwa wawakilishi wa vyama vya siasa. Wawakilishi walitumia mamlaka waliyopewa kufuatana na busara zao na uwezo na utaalamu wao ulipishana kwa kiasi kikubwa, jambo lililoathiri vibaya mpangilio na usimamizi wa mchakato. Viwango tofauti vya kufuatilia mchakato pia vilitolewa kwa wawakilishi wa vyama vya siasa pamoja na waangalizi kwenye vituo vya ujumlishaji.

Tathmini ya Waangalizi wa EU ya mchakato wa kuhesabu kura kwa ujumla ilikuwa nzuri sana au nzuri kwenye asilimia 64 tu ya vituo vilivyoangaliwa. Waangalizi wa kitaifa walikuwepo kwenye asilimia 41 tu ya vituo vilivyotembelewa. Kwenye baadhi ya vituo kulionekana kuwepo na wanachama wa vyama vya siasa na polisi ambao hawakustahili kuwepo. Kwenye nusu ya vituo vilivyotembelewa, mpangilio wa kazi ulitathminiwa kuwa mzuri au mzuri sana, wakati asilimia 15 ya ufanisi wa maafisa kwa ujumla ulitathminiwa kuwa m'baya. Mawakala wa CCM na CHADEMA walikuwepo kwenye asilimia 80 ya vituo vilivyoangaliwa na mara nyingi waliweza kuhakiki takwimu kwenye fomu kabla kazijaingizwa kwenye kompyuta. Kwenye vituo vingi, matokeo yalionyeshwa kwenye televisheni hapo kituoni mara baada ya takwimu kuingizwa kwenye kompyuta. Hata hivyo, kulikuwa na taarifa za matukio ya matatizo na mfumo wa NEC wa usimamizi wa matokeo (RMS). Pale ambapo kulikuwa na hitilafu ya mfumo, takwimu ziliingizwa kwenye Excel kama mfumo mbadala.

Matokea ya uchaguzi wa rais na ubunge hayakuwa yakipelekwa wakati wote moja kwa moja kwenye kituo kikuu cha jimbo kwa kujumlishwa, ila kwanza yalikuwa yanapelekwa kwenye kituo cha kata pamoja na matokeo ya uchaguzi wa madiwani, jambo ambalo lilisababisha ucheleweshaji wa kuwasilisha fomu za matokeo. Mpangilio wa upokeaji wa nyaraka ulitofautiana. Maeneo mengi mchakato wa upokeaji haukuwa na matatizo na ulisimamiwa vizuri. Hata hivyo, kwenye asilimia 34 ya upokeaji wa fomu na nyaraka ulioangaliwa, alama zilizotumika kuhakikisha kutofunguliwa vifaa kutoka vituoni hazikuwa zimetimia. Kwenye baadhi ya maeneo, mchakato wa kuwasilisha na kupokea vifaa haukuwa na mpangilio, kama ilivyoonekana kwenye majimbo ya Songea, Nyamagana, Musoma Mjini na Tanga. Songea baadhi ya maboksi yalifika yakiwa hayajawekewa chapa ya kuonyesha kufungwa ipasavyo.

Kulionekana kuwa na kutofautiana kwenye jinsi ya kuanza kuhesabu kura. Dodoma, Morogoro Vijijini, Dar es Salaam, Songea na Iringa Mjini, vituo vilikuwa na utaratibu wa kufanya zoezi la kupokea vifaa kwanza kisha la kuhesabu kura kufanyika. Fomu za matokeo na karatasi za kupigia kura zilikusanywa, kutunzwa na kuwekwa kando mpaka fomu na makaratasi yote yalipokuwa yamewasilishwa na ndipo zoezi la kuingiza takwimu kwenye kompyuta lilipoanza. Tofauti na hiyo, zoezi la upokeaji wa matokeo lilifanyika sambamba na la kuhesabu kura kwenye majimbo ya Morogoro Mjini, Morogoro Kusini Mashariki na Kawe. Kwenye vituo vya kuhesabia kura vya Morogoro Mjini, Dar es Salaam na Ukonga, takwimu za uchaguzi wa rais na ubunge zilijumlishwa kwa wakati mmoja, bila kufuata maelekezo ya NEC ya kutoa kipaumbele kwa kura za rais. Mchakato huu wa kujirudia ulionekana kuwa na hitilafu.

Matukio ya makosa ya kiutaratibu au ya kuruka au kukosea kuhesabu yalionekana. Tofauti kati ya fomu za matokeo ya vituo vya kupiga kura na takwimu zilizoingizwa kwenye mahesabu zilionekana kwenye asilimia 17 ya matukio yaliyoangaliwa. Mwanza kulikuwa na hitilafu kwenye kujaza fomu ambazo hazikurekebishwa na msimamizi mkuu. Makosa ya mahesabu kwenye fomu za matokeo hayakuhakikiwa wakati wa kupokea fomu, na wakati wa ujumlishaji makosa haya hayakurekebishwa. Lalamiko moja liliwakilishwa. Ilemela, matokeo ya baadhi ya vituo hayakuingizwa kwa usahihi kwenye takwimu za Excel za jimbo. Kwenye matukio kadhaa, kura chache (5 hadi 7) ziliongezwa kwenye kura za mgombea wa CCM na kwenye matukio mengine kadhaa kura za CHADEMA zilipunguzwa. Wakala wa CHADEMA hakuwepo kwenye hatua hii ya kujumlisha kura na baadae alikataa kutia saini fomu ya matokeo ya jimbo ya uhcaguzi wa mbunge. Lalamiko la kupinga matokeo haya liliwasilishwa.

Dodoma Mjini, msimamizi mkuu alitangaza matokeo ya uchaguzi wa ubunge ikiwa matokeo ya vituo 122 tu

kati ya 737 yalikuwa yameingizwa kwenye kompyuta. Msimamizi mkuu kwa makusudi hakuwataarifu mawakala wa vyama vya siasa kuhusu tangazo hilo.

Uchelweshaji katika mchakato wa kujumlisha kura kwenye ngazi ya jimbo ulileta wasiwasi kwenye baadhi ya vituo kwa wafuasi wa vyama waliokuwepo kufuatilia utangazaji wa matokeo. Baadhi ya maeneo, polisi waliingilia na kutumia mabomu ya machozi kutawanya makundi ya watu. Kwa kiasi kikubwa, wafuasi wa vyama walielezea wasiwasi juu ya ucheleweshaji wa kutangazwa matokeo ya uchaguzi wa ubunge. Kulikuwa na matukio ya vurugu Mbozi mkoani Mbeya, ambako makundi ya watu walichoma moto mahakama ya mwanzo ya Mlowo na ofisi ya wilaya ya CCM, wakidai kutangazwa matokeo mara moja. Matukio ya polisi kutawanya makundi ya watu nje ya vituo vya kujumlisha kura kwa kutumia mabomu ya machozi pia yaliripotiwa na waangalizi wa EU Tukuyu mkoani Mbeya, Songea mkoani Ruvuma, Bukoba Mjini mkoani Kagera, Mtwara, Tabora Mjini na Igunga mkoani Tabora, Bariadi Magharibi mkoani Simiyu, Longido mkoani Arusha, Ukonga mkoani Dar es Salaam, Manyoni mkoani Singida na Tanga.

*C. Matangazo ya Matokeo ya Uchaguzi wa Muungano*

Sheria haijaweka muda maalum kwa NEC kutangaza matokeo ya uchaguzi wa rais wa Muungano. Katiba inazungumzia tu muda usiozidi siku 7 kwa mshindi kutwaa madaraka baada ya kutangazwa kuwa mshindi, na muda mwingine tena usizidi siku 7 kwa rais kuitisha Bunge jipya baada ya kutangazwa matokeo ya uchaguzi wa ubunge.

NEC ilianza kutangaza baadhi ya matokeo ya uchaguzi wa urais tarehe 26 Oktoba. Zoezi la kujumlisha takwimu za uchaguzi wa urais lilifanyika tarehe 29 Oktoba kwenye kikao kilichokuwa wazi, baada ya fomu za matokeo kutoka majimbo mengi kuwa zimepokelewa. NEC walitangaza rasmi matokeo ya uchaguzi wa rais tarehe 30 Oktoba. Magufuli wa CCM alitangazwa kushinda kwa asilimia 58 ya kura (kura 8,882,935); Lowassa wa CHADEMA/UKAWA alipata asilimia 40 (6,072,848). Idadi hii ilikuwa kubwa kuliko yoyote yaliyopatikana na mgombea wa upinzani tangu Tanzania ianze mfumo wa vyama vingi. Wagombea 6 wa urais waliobaki kwa pamoja walipata chini ya asilimia 1.55 ya kura. Taarifa rasmi ya waliyojitokeza kupiga kura ilikuwa asilimia 67.31, ikiwa ni idadi kubwa sana kuzidi waliyojitokeza mwaka 2010 ambayo ilikuwa asilimia 43.

Rais mpya aliapishwa tarehe 5 Novemba. Kiwango cha uangalizi ulioelekezwa kwenye hiyo sherehe pamoja na ushiriki wa hali ya juu wa kimataifa ulipelekea swala la Zanzibar kupewa uangalizi mdogo zaidi.

***Matokeo ya uchaguzi wa rais***

| | | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Wapiga kura walioandikishwa | 23,161,440 | |
| Waliopiga kura | 15,589,639 | 67.31% |
| Kura halali | 15,193,862 | 97.46% |
| Kura zilizoharibika | 402,248 | 2.58% |

| | **Jina la Mgombea** | **Jinsi** | **Chama** | **Kura** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | ANNA ELISHA MGHWIRA | MKE | ACT | 98,763 | 0.65% |
| 2 | CHIEF LUTALOSA YEMBA | MME | ADC | 66,049 | 0.43% |
| 3 | DKT. MAGUFULI JOHN POMBE JOSEPH | MME | CCM | 8,882,935 | 58.46% |
| 4 | LOWASSA EDWARD NGOYAI | MME | CHADEMA | 6,072,848 | 39.97% |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 5 | HASHIM RUNGWE SPUNDA | MME | CHAUMMA | 49,256 | 0.32% |
| 6 | KASAMBALA JANKEN MALIK | MME | NRA | 8,028 | 0.05% |
| 7 | LYIMO M. ELIFATIO | MME | TLP | 8,198 | 0.05% |
| 8 | DOVUTWA FAHMI NASORO | MME | UPDP | 7,785 | 0.05% |

Pamoja na kwamba Magufuli na Lowassa wote wawili walifanya kampeni kitaifa, kulikuwa na mgawanyiko dhahiri kimkoa kwenye matokeo ya uchaguzi, Lowassa akiwa ameshinda mikoa ya kaskazini kama Arusha na Kilimanjaro na kufanya vizuri kwenye maeneo ya mijini ikiwemo mji mkuu kibiashara wa Dar es Salaam, wakati Magufuli alishinda katika karibu maeneo mengine yote, pamoja na maeneo yote ya vijijini, na kwenye eneo muhimu la Mwanza lililopo kaskazini magharibi mwa nchi. Kutokana na ukweli wa kuwa idadi kubwa ya wananchi wa Tanzania bado wako vijijini, na wafuasi wa CHADEMA walioko mijini kutokuwa wengi kutosha kuweza kupiku hazina hii ya CCM, CCM ilibaki kwenye nafasi nzuri zaidi. Tuhuma za hila zilizotolewa na CHADEMA, ikiwa ni pamoja na madai kuwa idadi halisi ya kura ilizopata ilifichwa kwenye maeneo iliyokuwa na uwezo mkubwa, hazikuweza kuhakikiwa kwa ushahidi uliyotolewa hadharani.

Idadi ya waliojitokeza kupiga kura ilipanda kutoka kiwango cha chini kabisa kutokea cha asilimia 43 mwaka 2010 na, ikifika karibu asilimia 67, kulingana na idadi iliyo kawaida kwa Tanzania kihistoria. Hata hivyo, pamoja na idadi kubwa ya wapiga kura kuandikishwa, idadi ya waliyojitokeza maeneo ya mijini haikuwa kubwa kutosha kuweza kupiku uwingi uliyojitokeza kwenye majimbo ya vijijini.

Pamoja na kuwepo na makubaliano ya ushirikiano kwenye uchaguzi kwa baadhi ya vyama, kugawana kura kati ya CUF na CHADEMA kwenye baadhi ya majimbo, hususan Dar es Salaam, kulivigharimu vyama hivyo na ilisaidia CCM kushinda au kubaki na viti ambavyo vinginevyo vingekuwa hatarini kuchukuliwa na upinzani.

Vyama vya UKAWA vilishinda idadi kubwa kuliko vilivyowahi kushinda ya viti vya majimbo na viti maalum. Kulinganisha na viti 89 ambavyo vyama vya UKAWA vilikuwa navyo wakati wakuvunjwa Bunge lililopita, umoja huo sasa una viti 113. TLP na UDP vyote vilipoteza kiti kimoja kimoja ambavyo kila chama kilikuwa nacho Bungeni, wakati NCCR-M kilipungukiwa kufikia kuwa na kiti kimoja tu. Chama kipya cha ACT kilishinda kiti kimoja. Pamoja na kuwa CCM ina uwingi kwenye Bunge la Muungano, ikiwa na viti 254, zaidi ya mara mbili ya wabunge wa upinzani (kabla ya kuongeza viti vya chaguzi zilizoahirishwa na viti maalum ambavyo rais anateua), kutakuwa na idadi kubwa zaidi ya kuleta changamoto kwa CCM.

*D. Hali Baada ya Uchaguzi*

Hali baada ya uchaguzi ilihusisha watu kadhaa kukamatwa kwa makosa chini ya Sheria ya Makosa ya Mtandao na kufunguliwa kwa kesi nne, polisi kukataza kuwa na mikusanyiko au maandamano yoyote, na kuwepo kwa idadi kubwa ya polisi na wanajeshi mitaani.

UKAWA, ikiongozwa na CHADEMA, ilikataa matokeo ya uchaguzi wa Muungano ya rais na ubunge, na kusisitiza kuwa mgombea wao alishinda. Chama kilijaribu kufanya maandamano Dar es Salaam tarehe 2 na 3 Novemba, lakini walikataliwa idhini ya polisi. CHADEMA walidai kuwa na ushahidi wa kughushi matokeo, na kuwa kulikuwa na tofauti kubwa kati ya matokeo kwenye vituo na takwimu zilizotangazwa na NEC. Juhudi za CHADEMA kujumlisha takwimu ziliingiliwa tarehe 25 Oktoba, wakati polisi walipovamia na kunyang'anya takwimu, kompyuta na vifaa vingine kwenye vituo vya mawasiliano vya CHADEMA, na wafanyakazi wake 191 walikamatwa na kufikishwa mahakamani na wanane waliwekwa kizuizini hadi tarehe 30 Oktoba. Wafanyakazi wa vituo vya mawasiliano vya CHADEMA walituhumiwa, chini ya kifungu cha 16 cha Sheria ya Makosa ya Mtandao, kwa kosa la kutangaza taarifa zisizo za kweli, za udanganyifu na zisizo na uhakika bila uhakiki wa NEC. Kesi hii ilikuwa ianze kusikilizwa tarehe 22 Desemba 2015.

Zaidi ya polisi kuvamia ofisi za CHADEMA, kituo cha takwimu cha Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), ambapo kikundi cha waangalizi wa kitaifa walikuwa wakikusanya na kuchambua taarifa kutoka kwa

waangalizi wake, pia kilivamiwa na polisi, tarehe 29 Oktoba. Wafanyakazi walishikiliwa na kompyuta na simu kunyang'anywa, pia chini ya kifungu cha 16 cha Sheria ya Makosa ya Mtandao. Polisi walidai kuwa walikuwa wanakusanya na kusambaza matokeo kupitia mtandao, kinyume na mamlaka waliyokuwa nayo ya uangalizi wa uchaguzi.

Kifungu cha 16 cha Sheria ya Makosa ya Mtandao kiltumika kwenye matukio mengine mawili ambapo watu walikamatwa. Kesi nyingine ya tatu ilimhusu mfuasi wa CHADEMA, Yericko Yohanesty Nuyerere, aliyekamatwa tarehe 24 Oktoba na baadae kuachiwa kwa dhamana, aliyeshitakiwa kwa kosa la kusambaza taarifa za uongo kupitia mitandao ya kijamii kati ya tarehe 25 Oktoba na tarehe 3 Novemba. Kesi ya nne na ya mwisho ilihusisha watu wanne ambao wanapelelezwa, wakishukiwa kusambaza taarifa za uongo tarehe 6 Novemba. Watu hao wanne walikuwa kizuizini bila dhamana. Kesi zote zilikuwa zinasubiri kusikilizwa wakati wa kuandika ripoti hii.

Sheria ya Makosa ya Mtandao ya 2015 ilikosolewa sana na vyama vya siasa na asasi za kiraia kwa kutoendana na misingi ya kimataifa juu ya uhuru wa kujieleza, na pia imeleta wasiwasi mkubwa juu ya utekelezaji wake, hususan kuzingatia uzito mkubwa wa adhabu na mamlaka makubwa yanayotolewa kwa polisi kupekua na kunyang'anya. Pamoja na kwamba kulikuwa na uwezekano wa kunyimwa uhuru wa kujieleza kutokana na kupitishwa kwake, uhuru wa kujieleza kwa jumla uliheshimika katika kipindi chote kabla ya uchaguzi, na vyombo vya habari viliweza kufanya kazi katika mazingira ya uhuru. Hata hivyo, mara baada ya siku ya uchaguzi, tendo la polisi kuvamia ofisi za CHADEMA na kikundi cha waangalizi wa kitaifa (TACCEO)/ Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, ambako uchambuzi wa takwimu za uchaguzi ulikuwa ukifanyika, na kukamatwa kwa wafanyakazi na kunyang'anywa vifaa na nyaraka, chini ya kifungu 16 cha sheria hiyo, kulileta wasiwasi juu ya utekelezaji wa sharia hiyo.

Kifungu cha 16 cha sheria kinachohusu usambazaji wa taarifa zisizo za ukweli kinasema *"Mtu yeyote anayetangaza au kusambaza taarifa, takwimu au maelezo yoyote katika mfumo wa picha, maandisi, ishara au mfumo mwingine wowote kwenye vifaa vya kompyuta <u>ambapo taarifa, takwimu au maelezo hayo si ya kweli, ni danganyifu, ya kupotosha au siyo kamili anakuwa ametenda kosa</u>, na akikutwa na hatia ataadhibiwa faini isiyopungua TZS milioni 3 au kifungo cha muda usiopungua miezi sita au vyote"*

Septemba 2015, Muungano wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) uliwasilisha lalamiko la kupinga uhalali kikatiba wa baadhi ya vipengele vya Sheria ya Makosa ya Mtandao, ikiwa ni pamoja na vipengele vinavyozuia haki ya kutafuta, kupokea au kusambaza taarifa; mamlaka kwa vyombo vya sheria kupekua na kunyang'anya vifaa vya kompyuta, takwimu na taarifa bila kuwa na hati ya mahakama; kubana uwezo wa mshitakiwa kufika mahakamani kujitetea mbele ya Mahakama (kifungu 38 kinatoa fursa kwa kesi kusikilizwa ikiwa upande mmoja tu upo mahakamani). Kesi ilitegemewa kusikilizwa tarehe 10 Februari 2016. Lalamiko, hata hivyo, halijazungumzia moja kwa moja kifungu 16 cha sheria.

Mabalozi wa Umoja wa Ulaya, Uswisi, Canada, Norway na Marekani waliyopo nchini walitoa tamko la pamoja tarehe 9 Novemba wakielezea wasiwasi juu ya matumizi ya Sheria ya Makosa ya Mtandao kwa namna inavyobana upana wa shughuli zinazoweza kufanyika na asasi za kiraia na waangalizi wa kitaifa.

## XIV. Zanzibar - Siku ya Kupiga Kura na Kipindi Baada

### *A. Upigaji Kura na Kufunga Vituo*

Huko Zanzibar Ujumbe wa Waangalizi wa Umoja wa Ulaya walifuatilia mchakato kwenye vituo 71 vya kupigia kura. Karibu vituo vyote vilivyoangaliwa vilifunguliwa kwa wakati na taratibu za kufungua zilifuatwa, kasoro kwenye kituo kimoja tu. Upigaji kura ulitathminiwa kuwa ni mzuri kwenye asilimia 96 ya vituo vya kupigia kura vilivyoangaliwa na EU EOM. Upigaji kura ulifanyika kwa mpangilio na katika mazingira ya utulivu pamoja na kuwepo kwa foleni ndefu zilizoripotiwa asubuhi hiyo. Kulikuwa na matukio machache ambapo

shughuli za kampeni zilionekana kufanyika karibu na maeneo ya vituo vya kupigia kura. Kwenye kituo cha Sharifumusa (jimbo la Mtoni) mgombea na wapiga kura walijihisi kutishiwa kwa uwepo wa kikosi maalum cha jeshi, kilichokuwa na silaha, kwenye geti la kuingilia. Waanagalizi wa EU walieleza kuwa kwenye kituo kimoja cha kupigia kura wawakilishi wa vyama vya siasa walivuka mipaka ya mamlaka yao na kuwa karatasi za kupigia kura hazikutosha kwenye vituo viwili vya kupigia kura. Taratibu za upigaji kura kwa ujumla zilifuatwa kwenye vituo vya kupigia kura vilivyotembelewa na waangalizi wa EU jambo ambalo lilihakikisha kuwa mchakato wa upigaji kura unaendeshwa kama ilivyokusudiwa. Waangalizi wa EU walieleza kutokuwa na ulinzi wa kutosha wa usiri wa kura kwenye asilimia 8 ya vituo vilivyotembelewa, zaidi hii ilitokana na mpangilio duni wa mazingira ya kituo. Ufanisi wa wasimamizi wa ZEC kwa ujumla ulitathminiwa kuwa ni mzuri au mzuri sana.

*B. Kuhesabu na Kujumlisha Kura*

Nakala za fomu za matokeo zilibandikwa nje ya vituo vya kupigia kura na pia kupewa kwa mawakala wa vyama vya siasa. Fomu za matokeo ya uchaguzi wa rais na wawakilishi wa Baraza la Wawakilishi zilipelekwa kwa wasimamizi wakuu wa uchaguzi wa majimbo 54.

Kwenye vituo vya kuhesabia kura vilivyoangaliwa na wawakilishi wa EU EOM Pemba, wasimamizi wa uchaguzi, baada ya kupokea vifaa, walihakikisha kuwa fomu zilijazwa kwa usahihi na kikamilifu. Wasimamizi wakuu walikuwepo wakati wa kushughulikia fomu za matokeo za vituo vya kupigia kura. Mawakala wa CCM, CUF, CHADEMA na ADC walikuwepo wakati wa kujumlisha matokeo. Waangalizi wa kitaifa hawakuwepo. Wakati wa kujumlisha matokeo, ilikuwa vigumu kwa waangalizi kufuatilia mchakato kwa kuwa ZEC haikuwa na karatasi ya majumlisho, na takwimu zilisomwa kwa sauti, zikaandikwa ubaoni na kufutwa haraka. Hata hivyo, jumla ya kura zilizotangazwa kwa kila mgombea na msimamizi mkuu zilioana na jumla zilizohesabika na wawakilishi na waangalizi. Wawakilishi wa vyama waliokuwepo walisaini fomu za matokeo kwenye vituo vilivyoangaliwa na hakukuonekana kuwa na makosa kiutaratibu au ya kutotimizwa lolote.

Wasimamizi wa uchaguzi waliorodhesha matokeo ya uchaguzi wa rais na wa Baraza la Wawakilishi na kuwatangaza washindi wa Baraza la Wawakilishi katika kila jimbo. Wasimamizi wa majimbo 54 ya Zanzibar walitoa vyeti vya ushindi kwa wagombea waliochaguliwa kwa Baraza la Wawakilishi, mara baada ya kutangazwa matokeo ya uchaguzi usiku wa tarehe 25 Oktoba na tarehe 26 Oktoba.

Kwenye zoezi la kuhesabu matokeo ya kura ya uchaguzi wa rais Zanzibar, wawakilishi wa ZEC na mwakilishi wa kila chama kilichogombea walikuwepo kwenye kituo cha kuhesabia kura cha Bwawani. Tofauti na ilivyokuwa kwenye kuhesabu kura za uchaguzi wa rais wa Muungano, ambapo waangalizi hawakuruhusiwa kuwepo, waangalizi wa EU, UNDP, Marekani na Ubalozi wa Uingereza waliruhusiwa kuangalia mchakato. Zoezi la kuorodhesha matokeo kwenye kituo kikuu cha ZEC lilikuwa kwa ujumla la uwazi kwa siku mbili za kwanza (tarehe 26 na 27 Oktoba) baada ya hapo waangalizi hawakuruhusiwa tena kuwepo hadi hapo uamuzi wa kubatilisha uchaguzi ulipofikiwa.

Mara baada ya kupokea fomu za matokeo kutoka kwenye jimbo, ZEC ilifanya zoezi la kuzihakiki na kujumlisha matokeo wakati mawakala wa vyama vya siasa wakifuatilia kwa karibu. Matokeo yaliwekwa kwenye kompyuta kwa kutumia Excel na kuonyeshwa ukutani. Zoezi la kuhakiki matokeo awali lilianzishwa kwenye ngazi ya vituo vya kupigia kura na kubadilishwa kwenda ngazi ya kituo cha jimbo, na kurudishwa tena kwenye ngazi ya kituo kufuatia ombi la mawakala wa CCM. Matokeo ya uchaguzi yaliyohakikiwa na ZEC yalikuwa yakitangazwa kwenye kituo cha kuhasabu kura kadiri yalivyokuwa yakipatikana. Idadi kubwa ya fomu za matokeo zilizokuwa na ZEC zililingana na zile walizopewa mawakala wa vyama. Palipokuwa na tofauti, ZEC ilimuomba wakala atoe nakala yake aliyopewa kutoka kwenye kituo cha kupigia kura. Waangalizi wa EU waliripoti kuwa, kadiri mchakato wa uhakiki ulivyokuwa ukiendelea kwenye ngazi ya jimbo, mchakato ulipata kuingiliwa na kucheleweshwa mara kwa mara. ZEC iliongeza maombi yake kwa mawakala wa vyama kuwasilisha nakala zao za fomu za matokeo ya vituoni kwa sababu mawakala wa CCM mara kwa mara

walikuwa hawakukubaliana na takwimu za matokeo kutoka kwenye vituo kadhaa. Maombi haya ya mara kwa mara yalipunguza kasi ya zoezi la kujumlisha kura na waangalizi wa kimataifa walikuwa wanazidi kunyimwa fursa ya kuangalia mchakato wa kujumlisha kura kwenye chumba kilichotengwa maalumu kwa uhakiki wa matokeo.

Mchana wa tarehe 27 Oktoba, askari wa Jesi la Wananchi Tanzania, kwa pamoja na Idara za Usalama Zanzibar, walizuia kuingia na kutoka kwenye kituo kikuu cha kuhesabia kura, hivyo kuwanyima waangalizi wa EU na taasisi zingine za kimataifa kuingia. Ruhusa ilitolewa baada ya masaa 5, bila kutolewa maelezo yoyote na ZEC wala na maafisa usalama. Kufika jioni ya tarehe 27 Oktoba, ZEC ilikuwa imeshatangaza matokeo ya uchaguzi wa rais kwa majimbo 31 kati ya 54. Kati ya hayo, hakukuwa na lolote kutoka Pemba.

ZEC ilikutana tarehe 28 Oktoba, baada ya kuahirishwa na kutangaza matokeo mengine ya uchaguzi. Mwenyekiti wa ZEC alipoondokoa kituo cha kujumlisha kura, makamu mwenyekiti wa ZEC alijaribu kuendeleza zoezi la ujumlishaji, lakini alizuiwa kufanya hivyo na kutolewa nje ya kituo na maafisa wa usalama. Baada ya hapo mwenyekiti wa ZEC alitangaza, kupitia ZBC, taarifa ya kubatilisha matokeo ya uchaguzi Zanzibar na akataja sababu za ubatilishaji huo. Sababu zilizotolewa na mwenyekiti wa ZEC kwa ubatilishaji zilikuwa ni pamoja na mivutano kati ya makamishna wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar; makamishna wa ZEC kushindwa kutekeleza wajibu wao kama makamishna na badala yake kuwa kama mawakala wa vyama; kutokuwepo kwa uwakilishi kwa baadhi ya vyama kwenye kituo cha ZEC; kuzidi idadi ya wapiga kura kwenye baadhi ya vituo, hasa Pemba, kuliko idadiya walioandikishwa; masanduku ya kura Pemba kuhamishwa na kuhesabiwa nje ya vituo vya kupigia kura; mawakala wa vyama, hasa wa TADEA, kutolewa kwenye vituo vya kupigia kura na kupigwa; kuvamiwa vituo vya kupigia kura na vijana na watu kunyimwa kufika kwenye vituo vya kupigia kura; vyama vya siasa kuingilia kazi za ZEC, ikiwa ni pamoja na kujitangazia ushindi; malalamiko mengi yaliyotolewa na vyama vya siasa kuelezea kutoridhishwa kwao na matokeo ya uchaguzi mkuu; na kuvurugwa takwimu kwenye fomu za matokeo kwenye baadhi ya vituo vya kupigia kura, hasa Pemba.

*C. Kubatilishwa Uchaguzi na Matkmio Baada*

Kufuatia tangazo la mwenyekiti wa ZEC tarehe 28 Oktoba kuwa matokeo ya uchaguzi Zanzibar yamebatilishwa, na kwamba uchaguzi utarudiwa, kulikuwa na taarifa ya matukio kadhaa ya kiusalama, ikiwa ni pamoja na vurugu kutendwa na vyombo vya usalama vya taifa dhidi ya wafuasi wa CUF kisiwani Tumbatu, karibu na Unguja. Vifaa viwili vya kulipuka viligundulika Stonetown, Unguja. Polisi walikilipua kimoja, na kingine kililipuka chenyewe. Hakuna majeruhi walioripotiwa. Pamoja na matukio haya, hali kisiasa Zanzibar kwa ujumla ilendelea kuwa ya utulivu, kwa kiasi kikubwa kwa sababu CUF mara kadhaa iliwasihi wafuasi wake hadharani kutulia.

Tarehe 29 Oktoba, EU EOM na jumbe za waangalizi wa kimataifa za Umoja wa Afrika, SADC na Jumuia ya Nchi za Madola zilitoa tamko la pamoja kuhusu Zanzibar. Jumbe hizo zilielezea wasiwasi wao mkubwa juu ya uamuzi wa mwenyekiti wa ZEC kubatilisha uchaguzi wa Zanzibar na, walisisitiza msimamo wao kuwa tathmini ya upigaji kura na mchakato wa kuhesabu kura kwenye vituo vya kupigia kura, kwa ujumla, ilikuwa kwamba haya yalifanyika kwa utulivu na mpangilio, kufuatana na taratibu zilizoelezwa kwenye sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na sheria za Zanzibar. Tume ziliiomba ZEC kubainisha vituo ambavyo vilikuwa na matatizo, na kuisihi ZEC kufanya kazi kwa uwazi kamilifu juu ya uamuzi wake wa kubatilisha uchaguzi.

Muda wa masaa 48 uliopangwa na CUF kutaka hali ishughulikiwa ulipita bila lolote kufanyika, na mawasiliano kati ya CUF na CCM yaliendelea kuwa finyu. CCM, kwenye kauli zake kwa jamii, ilisisitiza msimamo wake wa kuunga mkono uamuzi wa ZEC kuitisha uchaguzi mpya, wakati CUF walikataa mapendekezo ya kufanyika uchaguzi upya na kudai kuendelea na zoezi la kuhesabu kura na, baadaye, kutangaza matokeo ya uchaguzi wa rais na walikua na msimamo kuwa ubatilishaji wa uchaguzi ulikuwa ni

kinyume cha sheria.

Mara baada ya tangazo la mwenyekiti wa ZEC la kubatilisha uchaguzi, majadiliano yalianza katika asasi za kiraia na miongoni mwa wanasheria kuhusu uhalali wa uamuzi huu kwa mujibu wa taratibu na uthabiti wake. Awali, mwenyekiti wa ZEC alitangaza kuwa ilikuwa ni uamuzi wake kubatilisha uchaguzi, jambo lililozua wasiwasi kuhusu ZEC kuheshimu taratibu zake za maamuzi. Kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar, maamuzi yoyote ya ZEC lazima yapate akidi ya angalau wanatume watano (mwenyekiti au makamu mwenyekiti na makamishna wanne) na, ili maamuzi yapitishwe, lazima kura ipigwe na ipate wingi (yaani si chini ya kura tatu kuzingatia kuna wanatume watano). Kwa hiyo, maamuzi ya mwenyekiti wa ZEc peke yake hayawezi kuchukuliwa kuwa halali.

Hata hivyo, tarehe 1 Novemba, ZEC ilifanya mkutano wake wa kwanza tangu kubatulishwa matokeo, makamishna wote wakihudhuria. ZEC ikaamua kuidhinisha ubatilishaji wa uchaguzi, lakini kulikuwa na mgawanyiko kufuatana na vyama vya siasa, wateule wa CCM na mmoja mwingine wakikubaliana na mwenyekiti na kuidhinisha uamuzi huo kwa wingi wa kura nne, wakati wawakilishi wa CUF na makamu mwenyekiti walipiga kura kupinga uamuzi huo. Huo ulikuwa ndiyo mkutano wa mwisho kufanywa na ZEC hadi kuondoka kwa waangalizi wa EU EOM tarehe 8 Desemba. Uamuzi wa ZEC kubatilisha uchaguzi ulitangazwa kwenye Gazeti la serikali tarehe 11 Novemba ikitangazwa kuwa uamuzi ulifanyika tarehe 6 Novemba. Tangazo kwenye gazeti lilisema kuwa mwenyekiti wa ZEC, kwa niaba ya ZEC, amebatilisha uchaguzi uliofanyika tarehe 25 Oktoba na kutaja vipengele viwili vya sheria ambavyo vilitumika kufikia maamuzi: kifungu 119(10) cha Katiba kinachozungumzia akidi inayohitajika na idhini ya maamuzi yoyote ya tume; na vifungu 3(1) na 5(a) zinazosema kuwa kanuni zote, maelekezo na taarifa ambazo ZEC ina mamlaka kufanya yatachukuliwa kuwa yamefanyika kihalali chini ya sahihi ya mwenyekiti au mkurugenzi wa uchaguzi; na kwamba ZEC inawajibika kwa usimamizi kwa ujumla wa mpangilio wa uchaguzi mkuu. Taarifa hiyo haikubainisha misingi ya ubatilishaji wala mamlaka iliyopewa ZEC kubatilisha uchaguzi kwa sababu yoyote ile. Pia ilitamka kuwa tarehe nyingine ya kupiga kura itapangwa, bila kutoa maelezo zaidi.

Bila kujali kama utaratibu ulifuatwa katika uamuzi huu - kutokana na kupatikana idadi inayohitajika ya makamishna na kutangazwa kwenye gazeti la serikali - kuliendelea kuwepo na mvutano juu ya mamlaka ya kubatilisha matokeo ya uchaguzi au mchakato mzima wa uchaguzi, kwani hakuna kipengele maalumu kinachogusia hili kwenye sheria. Wajadialaji wote wa sheria pamoja na mahakama, isipokuwa Mwanasheria Mkuu aliyopo sasa, ambao waangalizi EU EOM walikutana nao, waliafikiana kuwa sheria haina kipengele cha kubatilisha mchakato mzima wa uchaguzi, ikiwa ni pamoja na awamu mbali mbali za uchaguzi pamoja na chaguzi zote tatu kwa pamoja, au uchaguzi mmoja tu (yaani wa urais, Baraza la Wawakilishi au udiwani). Kwa mujibu wa sheria, ZEC inaweza, kwa sababu yoyote ile, kuomba kuhesabiwa upya kura kwenye majimbo au kwenye jimbo tajwa. Zaidi, sheria inasema kuwa matokeo ya uchaguzi wa rais yanatakiwa kutangazwa katika kipindi kisichozidi siku tatu baada ya siku ya kupiga kura, isipokuwa pale ambapo kumetokea matatizo kwenye vituo vya kupigia kura, ambapo basi matokeo yatangazwe katika kipindi cha siku tatu baada ya kutatua matatizo hayo. Zaid ya hapo, ubatilishaji wa matokeo ya uchaguzi wa Baraza la Wawakilishi na madiwani umeendelea kuwa na mabishano kwa kuwa matokeo ya chaguzi hizo yalishatangazwa rasmi na wasimamizi wakuu wa uchaguzi, tarehe 25 na 26 Oktoba, kama inavyotakiwa kwa mujibu wa sheria na matokeo hayo yanaweza kupingwa tu kwa malalamiko kuwasilishwa Mahakama Kuu. Wasimamizi wakuu walishatoa vyeti vya ushindi kwa wagombea wa viti kwenye Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa sheria. Matokeo ya uchaguzi yaliyotangazwa na wasimamizi wakuu wa majimbo 54 kwa uchaguzi wa Baraza la Wawakilishi yalivipa CCM na CUF viti 27 kila chama.

Ingawa kuna uwezekano kuwa uamuzi wa mwenyekiti wa ZEC ungeweza kukatiwa rufaa Mahakam Kuu, wazungumzaji wengi, pamoja na vyama vya siasa, hawana imani na Mahakama ya Zanzibar kwenye swala la uwazi na kutokuwa na upendeleo. EU EOM waliambiwa kuwa kuna uwezekano mkubwa kwa majaji kushinikizwa kukubali uamuzi wa kubatilisha uchaguzi. Mtazamo huu wa shinikizo kwa majaji ulipewa uzito kwa jinsi ambavyo makamu mwenyekiti wa ZEC, ambaye mwenyewe ni Jaji wa Mahakama Kuu,

alivyosindikizwa na maafisa wa usalama kutoka kwenye kituo cha kuhesabu kura na kutoruhusiwa kuendeleza zoezi la kuhesabu. Katika mazingira haya, na kwa kuwa na wasiwasi kwamba kesi mahakamani ingeendelezwa bila uamuzi kwa muda mrefu, walalamikaji hawakufikiria hata kidogo kuchukua hatua za kimahakama.

Tarehe 9 Novemba, CCM na CUF walianza mazungumzo, kwenye mkutano wa kwanza kati ya mikutano 9[21] kati ya wagombea urais waliokuwa wakiongoza, Ali Mohamed Shein wa CCM (Rais wa Zanzibar) na Seif Sharif Hamad wa CUF (Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar). Mikutano hiyo ilihudhuriwa pia na Rais Mstaafu wa Zanzibar, Amani Abeid Karume, Rais Mstaafu wa Tanzania (na Zanzibar) Ali Hassan Mwinyi, na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Seif Ali Iddi. Mazungumzo haya ya ana kwa ana kati ya wagombea wakuu yalifuata mkutano uliofanyika tarehe 4 Novemba kati ya Rais Kikwete na Seif Sharif Hamad.

Kutangazwa kwa uamuzi wa mwenyekiti wa ZEC kwenye gazeti la serikali tarehe 11 Novemba, wakati mkutano wa pili ukiendelea, kulibadilisha sura ya mazungumzo kati ya pande hizo mbili. Wakati CUF wakitegemea makubaliano juu ya kendelea kwa zoezi la kuhesabu kura, tangazo hilo kwenye gazeti la serikali lilibadilisha mazingira kisheria kwani uamuzi wa ZEC ukawa umeshapitishwa kuanzia tarehe ya kutangazwa kama usingepingwa mahakamani. CUF walichukulia hii kuwa CCM hawakuwa na nia ya kufikia muafaka kwenye mazungumzo hayo. Mazungumzo yakaendelea kuhusu uhalali wa uamuzi uliochukuliwa na ZEC kwenye swala la mamlaka kisheria ya ZEC kubatilisha matokeo ya uchaguzi. Ombi la CUF kuwa mwenyekiti wa ZEC afikishwe kwenye mikutano hiyo lilikataliwa na CCM kwa madai kuwa hawakuwa na mamlaka ya kumuita mwenyekiti huyo.

Kwenye mkutano wa nne, tarehe 24 Novemba, CUF ilileta mapendekezo mawili ili kuleta usuluhisho la hali iliyokuwepo Zanzibar: i) kama kutafanyika upigaji kura upya kwa chaguzi zote tatu za Zanzibar, CUF itashiriki tu ikiwa chaguzi hizo zitaendeshwa na tume huru inayoongozwa na Umoja wa Mataifa; ii) kuwe na upigaji kura upya kwa uchaguzi wa rais kwenye majimbo 14 tu kisiwani Pemba ambapo kulikuwa na tuhuma za utata. Kwenye majimbo tisa yaliyobaki ambako matokeo ya uchaguzi wa rais yalihakikiwa, lakini hayakutangazwa na ZEC, haikuweza kueleweka kama matokeo hayo ni halali au la, uamuzi ukibaki kwa CCM. Hata hivyo, maamuzi yote yaliyotangazwa na ZEC kwa uchaguzi wa Baraza la Wawakilishi na madiwani yachukuliwe kuwa halali kwani yalishatangazwa rasmi na wasimamizi wakuu, vivyo hivyo matokeo ya uchaguzi wa rais kwenye majimbo 31 (kati ya 54) ambayo yalishahakikiwa na kutangazwa na ZEC. Kwenye mkutano wa tano, mapendekezo yote mawili yalikataliwa na CCM, la kwanza kwa sababu ya kutokuwepo na vifungu vya sheria vinavyoruhusu kuwa na tume huru inayoongozwa na Umoja wa Mataifa, na la pili wala CCM hawakulitafakari.

Baada ya mikutano kadhaa, CUF waliamini kuwa hakukuwa na sababu kuendelea na mikutano ya pande hizo mbili wakidai kuwa CCM hawakuwa na nia thabiti ya kujadili muafaka. CCM ilishikilia msimamo wa kurudiwa zoezi la upigaji kura, kwani mwenyekiti wa ZEC alibatilisha hatua za upigaji na kuhesabu na kujumlisha kura tu.

Sababu kuu za wasiwasi juu ya kurudia upigaji kura zilikuwa ni juu ya uhalali na imani kwa ZEC kama ilivyokuwa kuendesha upya upigaji kura; wasiwasi kuwa matokeo yanaweza kubatilishwa tena; na uhaba wa rasilimali fedha kuwezesha upigaji kura upya. Jumla ya gharama ya uchaguzi mkuu wa tarehe 25 Oktoba Zanzibar ilikuwa € (Euro) milioni tatu. Ingawa hakukuwa na imani kwa Tume ya Uchaguzi Zanzibar kama ilivyokuwa wakati huo, kutokana na taratibu za uteuzi, kunge kuwa na uwezekano mdogo wa kuwabadilisha makamishna na wafanya kazi wa makao makuu kama upigaji kura ungerudiwa. Hata hivyo, CCM ilisistiza kuwa wafanyakazi wasiyo wa kudumu, ikiwa ni pamoja na maafisa wa vituo vya kupigia kura, lazima wabadilishwe kutokana na tuhuma zilizojitokeza za utata kwenye uchaguzi wa tarehe 25 Oktoba.

[21] Mikutano kati ya wagombea urais wawili hao ilifanyika tarehe 9 Novemba, 23 na 24 Novemba, 30 Novemba, 7 Desemba, 11 Januari na 14 Januari. Tarehe 22 Januari, 2016, ZEC ilitangaza zoezi la kurudiwa uchaguzi kufanyika tarehe 20 Machi.

Nafasi ya taasisi za kimataifa za upatanishi wa mgogoro huu ilikuwa ni ndogo sana pamoja na kuwepo kwa juhudi za balozi kadhaa kuwasiliana na wadau wote husika. Mazungumzo yalibaki kuwa swala la Kizanzibari tu, na CCM haikuonyesha utayari wa kukubali upatanishi kutoka nje. Zaidi, hakukuwa na hatua za kuonekana zilizochukuliwa na CCM Tanzania wala Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania za kutatua tatizo hili hadi kuondoka kwa waangalizi wa EU, hata baada ya Rais Mteule Magufuli kusema wakati wa kuzindua Bunge la Muungano tarehe 20 Novemba kuwa Makamu wa Rais atakuwa na nafasi kubwa katika usuluhishi wa mgogoro wa Zanzibar. Jitihada za CUF kukutana na Rais zilikuwa zimeshindikana hadi tarehe 8 Desemba. Rais Magufuli alikutana na Rais wa Zanzibar Ali Mohammed Shein (CCM) na Makamu wa Rais Seif Sharif Hamad (CUF), kila mmoja kwa wakati wake, mwishoni mwa mwezi Desemba.

EU EOM ilibaki nchini Tanzania hadi tarehe 8 Desemba, ikiwa Zanzibar mara kwa mara kufuatilia maendeleo ya mchakato wa uchaguzi visiwani humo. EU EOM ilikuwa na mikutano mara kwa mara na wadau wakuu Zanzibar, ikiwa ni pamoja na vyama vya siasa, mwanasheria mkuu wa wakati huo na mstaafu, wanasheria na majaji, asasi za kiraia na wasimamizi wa uchaguzi. EU EOM iliona kuwa matokeo ya mikutano kati ya CCM na CUF hayakutangazwa hadharani na kulikuwa na juhudi za makusudi kuzuia upatikanaji wa taarifa hizo. Mikutano kati ya vyama hivyo viwili ilichukuliwa kuwa ya siri na hakukua na habari zozote juu ya maudhui wala maendeleo zilizotangazwa, hivyo kuwaacha wananchi wakiwa hawana uhakika kuhusu yatakayojiri siku za baadaye kwa taasisi za kisiasa nchini Zanzibar. Hali hii ya kutokuwa na uhakika, pamoja na uwepo mkubwa uliyoonekana wa jeshi visiwani, ilijenga mazingira ambayo baadhi ya wananchi waliamini kuwa jeshi lilikuwa limetwaa shughuli za serikali mpaka muafaka upatikane.

Pamoja na kutoa maombi kadhaa, EU EOM haikuweza kukutana na mwenyekiti wa ZEC wala makamu mwenyekiti. Tangu wakati wa uamuzi wa kubatilisha uchaguzi, mwenyekiti wa ZEC hakuweza kupatikana na ZEC, kama taasisi iliyokuwa na mamlaka ya kuendesha na kusimamia mchakato wa uchaguzi, ikawa kama haionekani. Isipokuwa kwa mkurugenzi wa uchaguzi wa ZEC, makamishna wa ZEC hawakuwepo kwenye ofisi za tume ya uchaguzi. Hapakuwepo na matamko mengine kutoka ZEC kuwataarifu wapiga kura juu ya mchakato wa uchaguzi wala kutoa maelezo zaidi juu ya tuhuma zilizokuwepo za makosa yaliyotendeka ambayo yalipelekea uamuzi wa kubatilisha uchaguzi. Hili lilidhihirishwa zaidi kwa ukweli wa kuwa, pamoja na kuwa taasisi yenye mamlaka juu ya mchakato wa uchaguzi, ZEC haikuhusishwa kwenye mikutanio kati ya vyama hivi vikuu viwili, ambako suluhisho la mgogoro lilikuwa likijadiliwa.

EU EOM ilifikia mtazamo kwamba mpaka kufikia muda wakuondoka kwake tarehe 8 Desemba, ZEC haikuwa imefanya kazi kwa uwazi katika swala la uamuzi wa kubatilisha uchaguzi na haikuupatia ujumbe huo wala mdau mwingine yeyote wa uchaguzi ushahidi wa makosa yaliyopelekea ubatilishwaji wa uchaguzi.

Tarehe 8 Desemba, kabla ya kuhamia kwa muda barani Ulaya, EU EOM ilitoa taarifa kwa vyombo vya habari ikisisitiza haja ya sulhisho la haraka la kukamilisha mchakato wa uchaguzi Zanzibar, kuendana na misingi ya chaguzi shirikishi, za uwazi, za muda wa kupangwa na za kuaminika. Taarifa hiyo ilisema kuwa, pamoja na mchakato wa uchaguzi Zanzibar kutokamilika, EU ilikuwa bado ina msimamo wake kwa uchaguzi Zanzibar na kwamba ujumbe ungetumwa tena pale ambapo makubaliano yatakakuwa yamefikiwa juu ya kuendeleza mchakato wa uchaguzi kwa misingi ya uhirkishwaji, uwazi, muda na uaminifu.

Pamoja na kwamba mikutano kati ya uongozi wa CCM na CUF Zanzibar iliendelea hadi Januari 2016, hakukuwa na muafaka juu ya mvutano wa uchaguzi kwa kuwa vyama vyote vilishikilia misimamo yake. Tarehe 22 Januari, kabla maamuzi yoyote ya kusitisha rasmi mikutano ya pande hizo mbili, mwenyekiti wa ZEC, kwa niaba ya ZEC iliyokuwa imekutana tarehe 30 na 31 Desemba 2015, aliitangaza tarehe 20 Machi kuwa tarehe ya kurudiwa uchaguzi mkuu Zanzibar. Tarehe 28 Januari, baada ya mikutano yake yenyewe, CUF ilitoa tamko rasmi kuwa haitashiriki zoezi la kurudiwa uchaguzi wa Zanzibar. Kufuatia matukio haya, tarehe 29 Januari, mabalozi wa Ubelgiji, Canada, Denmark, Hispania, Sweden, Uswisi, Uingereza na Marekani walitoa tamko la pamoja. Kwenye tamko hili, mabalozi hao walisisitiza imani yao kuwa ingekuwa ni bora mgogoro wa kisiasa Zanzibar ungepatiwa suluhisho linalokubalika na pande zote kupitia

majadiliano. Mabalozi walielezea wasiwasi wao kuwa uamuzi wa taasisi au upande mmoja tu wa kurudia uchaguzi ungeweza kuchochea kuongezeka kwa vitisho na mvutano. Tamko lilivitaka vyama vyote na wafuasi wao kuendelea kushirikiana kupata suluhisho la amani na walimshauri rais Magufuli kuonyesha uongozi katika kipindi hicho cha mvutano wa kisiasa, ili kuhakikisha matokeo ya amani na uhalali wa mchakato wa uchaguzi. Mabalozi pia walisisitiza kuwa michakato ya kuaminika ya uchaguzi lazima iwe shirikishi na yenye kuonyesha sura halisi na kuwa, katika mazingira yaliyokuwepo wakati huo, ingekuwa vigumu kutoa uangalizi wa kimataifa.

Marudio ya uchaguzi Zanzibar yalifanyika tarehe 20 Machi. Uchaguzi ulisusiwa na vyama tisa kati ya 14 amabavyo vilishiriki kwenye uchaguzi uliopita wa mwezi Oktoba, ikiwa ni pamoja na CUF. Pamoja na vyama kuiandikia ZEC kuieleza nia yao ya kutoshiriki, ZEC haikuondoa majina ya wagombea waliosusa wala vyama vyao kutoka kwenye makaratasi ya kupigia kura, wakidai uamuzi wao huo unatokana na misingi ya kiutaratibu. Vyama vya siasa vilivyoshiriki marudio ya uchaguzi havikuruhusiwa kufanya kampeni kabla ya uchaguzi. EU EOM haikufanya uangalizi wa uchaguzi wa tarehe 20 Machi kwa sababu haikuaminika kuwa mazingira ambayo uchaguzi ulikuwa ukifanyikia ni yanayo jenga ushirikishwaji, wala uchaguzi halali na wa kuaminika.

## XV. MAPENDEKEZO

Uboreshaji wa maeneo mengi ya mchakato wa uchaguzi, pamoja na kupitiwa upya mifumo ya sheria ya Muungano na Zanzibar, unahitajika ili kutimiza kikamilifu haki za msingi za watu na makundi, kama ilivyoelezwa kwenye kanuni za kimataifa na za kikanda za chaguzi za kidemokrasia. Kwa hili, mapendekezo yafuatayo yanatolewa ili kutafakariwa na kuchukuliwa hatua na Serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Tume ya Uchaguzi Zanzibar, vyama vya siasa, asasi za kiraia na jumuiya ya kimataifa. Mengi kati ya mapendekezo haya yako kwenye ripoti kamili ya EU EOM ya mwaka 2010 na bado yanaendelea kustahili kutolewa. Mazungumzo ya utekelezaji wa mapendekezo makuu yafuatayo yapangwe mapema iwezekanavyo ili kushughulikia kwa wakati mapungufu yaliyoonekana kwenye mchakato wa uchaguzi wa mwaka 2015. Jedwali la maepdnekezo kwa undani zaidi linapatikana kwenye kiambatisho I cha ripoti hii.

### Mfumo wa Kisheria

1. Haki ya kugombea uchaguzi isiwekewe mipaka ya ulazima wa kupendekezwa tu na chama. Kwenye swala hili, uamuzi wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu lazima utekelezwe. Wagombea binafsi wanatakiwa kuwa na haki ya kugombea nafasi yoyote kwenye uchaguzi wa Muungano au wa Zanziabr kama ilivyoelezwa kwenye Agano la Kimataifa la Haki za Uraia na Siasa na Hati ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu. Utekelezaji wa haki za wagombea binafsi kugombea nafasi kwenye uchaguzi hauna athari kwa mfumo wa uchaguzi unaozingatia kupata wingi wa kura unaotumika kwenye chaguzi za Muungano na Zanzibar.
2. Haki ya vyama vya siasa kuunda na kuandikisha miungano na kusimamisha wagombea kwa pamoja lazima ielezwe kwenye sheria, hususan kwenye swala la uchaguzi wa rais wa Muungano ambapo wagombea wawili wanasimamishwa kwa pamoja kugombea nafasi ya rais na makamu wa rais.
3. Katiba zote mbili za Muungano na Zanzibar kwa sasa zinanyima haki ya kupinga matokeo ya uchaguzi wa rais. Haki ya kupinga matokeo ya uchaguzi wa rais lazima ibainishwe kisheria kulingana na misingi ya kimataifa ya uendeshaji wa chaguzi za kidemokrasia.
4. Orodha ya wagombea wa kike kwa viti maalumu inayotolewa na vyama vya siasa kwa NEC na ZEC kabla ya uchaguzi isichukuliwe kuwa ni siri. Vyama vya siasa vitakiwe kisheria kutoa orodha ya majina ya wanaopendekezwa viti maalum kwenye Bunge la Muungano na Baraza la Wawakilishi, na NEC na ZEC wazitangaze orodha hizo ili wapiga kura wajue watakaonufaika na kura zao.

5. Utekelezaji wa vifungu fulani vya Sheria ya Makosa ya Mtandao unaweza kubana uhuru wa kujieleza na kupelekea watu kukamatwa kiholela. Kanuni za utekelezaji zianzishwe ili kuwe na utekelezaji wa Sheria hii unaoendana na aina ya makosa na unaotabirika. Watu wanaofunguliwa mashtaka kwa mujibu wa Sheria hii wasinyimwe haki ya kujitetea mbele ya mahakama, kama kifungu 38 cha Sheria kinavyosema kuwa ombi kwa mahakama litafanyika kwa kusikiliza upande mmoja tu na kwa siri.

**Utendaji wa Uchaguzi**

6. Zoezi la kupitia upya mipaka ya majimbo lifanyike ili kuhakikisha kuwa majimbo yanaendana vizuri zaidi na hali halisi ya mabadiliko ya idadi ya watu, ili kuchangia usawa zaidi kwenye kura. Haki ya kupiga kura kwa wote ina maana kuwa kila kura ina uzito sawa. NEC na ZEC lazima zishughulike tofauti kubwa iliyopo ya idadi ya wapiga kura waliyoandikishwa kwenye kila jimbo kuhakikisha kuwa mipaka ya majimbo inaendana na wingi wa watu na hivyo kuleta uwiano wa kura kwenye uwakilishi Bungeni. Kanuni ziangaliwe kuleta ushirikiano wa karibu zaidi kati ya serikali, inayowajibika kupanga mipaka ya kata, na utawala wa tume za uchaguzi, zinazowajibika kwa mipaka ya majimbo.
7. . Jitihada za makusudi zifanyike ili kupunguza uhusika wa taasis za utawala za serikali kwenye maswala ya upangaji na utekelezaji wa mchakato wa uchaguzi. Zoezi la kujenga mfumo huru wa kudumu wa NEC kimkoa pia uangaliwe, pamoja na mfumo wa muda kwenye ngazi ya jimbo wakati wa uchaguzi, namfumo huu uachane na utegemezi wake wa sasa kwa vyombo vya utawala wa mkoa/wilaya. Uteuzi wa makamishna wa NEC upitiwe upya ili kuongeza imani ya uhuru wa NEC miongoni mwa wadau wote.
8. Ili kujenga uwazi, uwajibikaji na imani ya vyama vya siasa kwa mchakato wa uchaguzi, NEC na ZEC zianzishe sera za mijadala yenye tija, ushirikiano na kugawana taarifa na vyama vya siasa na ziboreshe ufanisi wa idara zake za maelezo kuboresha utoaji wa taarifa kwa wananchi. Taarifa kamili na za wakati zitangazwe na zifikishwe kwa wadau wote, pamoja na vifaa vyote vya kiufundi vya mchakato wa uchaguzi: orodha za vituo vya kupigia kura, madaftari ya wapiga kura na maelezo yoyote kuhusiana na uendeshaji wa uchaguzi. Maamuzi na kanuni zinazotolewa na tume za uchaguzi vyote vielezwe kwa wadau.

**Uandikishaji Wapiga Kura**

9. Muda mrefu zaidi wa kutangaza madaftari ya wapiga kura kwa Muungano na Zanzibar utaboresha kwa kiasi kikubwa viwango vya madaftari kwa chaguzi zijazo.
10. Kwa swala la uandikishaji wa wapiga kura Zanzibar, sharti la kuwa na kitambulisho cha Zanzibar na la ukazi wa angalau miezi 36, lipitiwe upya kutokana na tofauti iliyopo kati ya Watanzania walioandikishwa Bara na wanaoandikishwa Zanzibar. Swala la mamlaka zilizopewa *sheha* kuhusu ushahidi wa ukazi pia lazima liangaliwe upya ili kujenga imani na mchakato. Daftari la wapiga kura lazima lisiwe na ubaguzi na muda wa ukazi upunguzwe.
11. Vyama vya siasa viwe vinapewa taarifa za mara kwa mara na kwa wakati juu ya kuongezwa majina, marekebisho au kukatwa majina kwenye daftari za wapiga kura, na wapatiwe nakala ya daftari za wapiga kura kabla uchaguzi kufanyika.

**Elima kwa Wapiga Kura**

12. Ili kuweza kuwataarifu wananchi kwa wakati na kikamilifu juu ya mchakato wa upigaji kura na chaguo walizonazo kwenye uchaguzi, tume za uchaguzi ziangalie uwezekano wa kuchukua hatua za kuboresha mipango, bajeti na utekelezaji shughuli za kuelimisha wapiga kura. Shughuli hizi zilenge

kuhusisha wote, pamoja na maelezo yanayolenga makundi maalum kama vijana na wanaopiga kura wa mara ya kwanza, wanawake na watu wenye ulemavu.

**Siku ya Kupiga Kura**

13. Maelezo ya taratibu za hatua muhimu za ukusanyaji, usafirishaji na kutangazwa kwa matokeo yatolewe ili kuepukana na kutofautiana kwa tafsiri za wasimamizi wa uchaguzi. Mafunzo kwa wasimamizi wote wa uchaguzi ya kuhesabu na kujumlisha, yaani jinsi ya kujaza fomu mabali mbali hasa fomu za matokeo, yanaweza kuboreshwa. Maelekezo na vitabu vya miongozo vipatiwe kwa wasimamizi wa uchaguzi na wadu kabla ya siku ya uchaguzi.
14. Nafasi ya vyombo vya usalama siku ya uchaguzi iangaliwe upya. Mamlaka ya polisi kwenye uchaguzi lazima ielezwe kikamilifu kwenye sheria na wapiga kura wafahamishwe. Wingi na muonekano mkubwa wa jeshi, kama ilivyokuwa, hususan visiwani Zanzibar, inaongeza hatari ya vitisho, au angalau hisia za vitisho kipindi cha uchaguzi.
15. Vyombo vya habari vinavyotambulika viruhusiwe kuingia vituo vya kupigia kura siku ya uchaguzi na kwenye vituo vya kukusanya na kuhesabu kura ili kuongeza uwazi wa mchakato. Miongozo thabiti ya ruhusa kwa vyombo vya habari inaweza kuandaliwa na tume ya uchaguzi kwa ushirikiano na Baraza la Vyombo vya Habari Tanzania (MCT).

**Matokeo ya Uchaguzi**

16. Kuongeza imani juu ya mchakato wa uchaguzi, hatua thabiti za uwazi, kama vile ruhusa kwa wawakilishi wa vyama vya siasa na waangalizi kujionea hatua zote za mchakato wa kujumlisha matokeo, ziangaliwe. Maeneo yanayofaa yakiwa na mpangilio unaofaa yaandaliwe ili kuruhusu ufuatiliaji na uangalizi bora wa mchakato.

**Malamiko na Rufaa**

17. Mahakama zinapaswa kuwa na mamlaka ya uangalizi wa wazi juu ya utekelezaji na maamuzi ya tume za uchaguzi. Maamuzi ya NEC na ZEC yanapaswa kuweza kupingwa mahakamani mara baada ya kipindi cha kupendekeza majina ya wagombea, na kwa kipindi chote cha mchakato. Walalamikaji wasilazimike kusubiri mpaka baada ya kutangazwa matokeo kuweza kwenda mahakamani.
18. Gharama za kuwasilisha lalamiko zipunguzwe kwa kiasi kikubwa ili kuwapa walalamikaji haki kamili ya kupata haki na sulushisho la mahakama.
19. Muda wa kuwasilisha malalamiko na muda wa kuyashughulikia uoanishwe na muda uliopangwa kwenye mchakato wa Muungano. Kwa Zanzibar, lalamiko linaweza kuwasilishwa mahakamani katika kipindi kisichozidi siku 15 baada ya kutangazwa matokeo, wakati kwa Muungano lalamiko linaweza kuwasilishwa katika kipindi kisichozidi siku 30. Kwenye kushughulikia malalamiko, Zanzibar mahakama inaweza kutoa uamuzi katika kipindi kisichozidi miezi 24, wakati mahakama za Muungano zimepewa kipindi kisichozidi miezi 12 kutoa maamuzi juu ya lalamiko.
20. ZEC na NEC ziangalie uwezekano wa kuwa na taratibu za kueleweka, zenye msimamo na zilizo wazi za kushughulikia malalamiko, ili kuwa na msimamo kwenye hatua zinazochukuliwa kushughulikia malalamiko na kujenga imani juu ya uwazi kwa mchakato.

**Vyombo vya Habari**

21. Vyombo vya habari vya taifa, Shirika la Utangazaji la Tanzania (TBC) na shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC), vigeuzwe kuwa vyomba vya huduma kwa umma na kupewa uhuru kamili wa uhariri na kifedha visiwe tegemezi kwa serikali.
22. Uhuru wa Mamlaka ya Usimamizi wa Mawasiliano Tanzania (TCRA) uboreshwe kisheria ili kuwe na mfumo uliyo wazi wa uteuzi wa bodi na mkurugenzi, usiyoingiliwa na chama chochote cha siasa, na unaohusisha asasi za kiraia na vyama vya waandishi wa habari.
23. Vyombo vya habari vibainishe matangazo yaliyolipiwa na vyama vya siasa kwa namna inayoeleweka ili wapiga kura wajue aina ya kipindi kinachotangazwa.
24. Muda wa bure unaotolewa kwa matangazo ya wagombea ugawiwe kwa namna yenye usawa, kwa misingi ya vigezo vya uwazi na kutofungamana. Vifungu vya sheria vinavyozungumzia muda wa bure wa matangazo vinaweza kufafanuliwa zaidi.
25. Taasisi za usimamizi ziangalie uwezekano wa kurekebisha Kanuni ya Huduma za Utangazaji (Maudhui) (Urushaji Matangazo ya Kiuchaguzi ya Vyama vya Siasa) *[Broadcasting Services (Content) (The Political Party Elections Broadcasts) Code]* kupunguza masharti, hususan kwa vyombo binafsi. TCRA ipitie upya kanuni kwa namna shirikishi kwa kuzingatia maoni ya wadau wa vyombo vya habari ambao walipata fursa ya kuzijaribu kanuni hizo kwa mara ya kwanza kwenye uchaguzi huu.
26. Sheria zinazogusa maswala ya uhuru wa kujieleza, pamoja na Sheria ya Takwimu na Sheria ya Makosa ya Mtandao zilizopitishwa hivi karibuni zirekebishwe kuondoa adhabu kali kuliko uzito wa kosa.

*****

VIAMBATISHI

| Dhumuni na inapoptokea kwenye Ripoti | Pendekezo | Hatua zinazopendekezwa na muda, inapostahili | Taasisi inayolengwa na wadau wengine | Ahadi za Kimataifa/Kikanda za Msingi |
|---|---|---|---|---|
| **MFUMO WA KISHERIA** | | | | |
| Kuendeleza haki na kuboresha fursa kushiriki shughuli za jamii, hususan haki na fursa kugombea nafasi kwenye uchaguzi<br><br>*Kurasa 13 na 21 za **Ripoti*** | Haki ya kugombea kwenye uchaguzi isiwe tu kwa wagombea wanaopendekezwa na vyama. Wagombea binafsi wanatakiwa kuwa na haki ya kugombea uchaguzi wowote wa Muungano au Zanzibar. Utekelezaji wa haki za wagombea bainafsi kugombea uchaguzi hauna athari kwa mfumo wa uchaguzi wa 'wa-kwanza-kupita' unaotumika Tanzania Bara na Zanzibar | Marekebisho ya katiba za Muungano na Zanzibar pamoja na Sheria ya Uchaguzi ya Taifa na Sehria ya Uchaguzi ya Zanzibar na. 11 | Bunge la Muungano na Baraza la Wawakilishi | Vifungu 3 na 25 (a) za ICCPR; Maelezo na 25 ya ICCPR, ibara 15: "utekelezaji wa haki na fursa ya kugombea nafasi kwenye uchaguzi inahakikisha kuwa watu wenye haki ya kupiga kura wanakuwa na uhuru wa kuchagua wagombea" na ibara 17: "Haki ya mtu kugombea nafasi kwenye uchaguzi isinyimwe bila mantiki kwa kuwa na sharti la wagombea kuwa wanachama wa vyama vya siasa maalum"<br>Vifungu 2 na 25(a) ya ACHPR na Uamuzi wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu 009-011-2011, Mch. Christopher Mtikila v. Tanzania |
| Kuhakikisha kikamilifu haki ya kukusanyika/kujumuika<br>*Kurasa 13 na 21 za **Ripoti*** | Haki ya vyama vya kuunda na kusajili umoja na kupendekeza wagombea wa pamoja itajwe moja kwa moja kwenye sheria, hususan kwenye uchaguzi wa rais wa Muungano ambapo wagombea wawili wanapendekezwa kwenye tiketi moja ya rais na makamu wa rais. | Kurekebisha katiba za Muungano na Zanzibar pamoja na Sheria ya Vyama vya Siasa | Bunge la Muungano, Baraza la Wawakilishi | *Kifungu 22 cha ICCPR na Maelezo ya ICCPR na. 25 :" haki ya uhuru wa kujumuika, pamoja na haki ya kujiunga na kuunda mashirika yanayojihusisha na maswala ya siasa na shughuli za jamii, ni kipengele muhimu kwa haki zilizolindwa na kifungu 25."* |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kujenga imani kwa mchakato wa uchaguzi na kujenga haki ya kupata suluhishi kisheria. *Kurasa 13 na 34 za* ***Ripoti*** | Katiba zote mbili za Muungano na Zanzibar kwa sasa zinanyima haki ya kupinga matokeo ya uchaguzi wa rais. Haki ya kupinga matokeo ya uchaguzi wa rais iwekwe kisheria kuendana na misingi ya kimataifa ya uendeshaji wa chaguzi za kidemokrasia. | Marekebisho ya katiba za Muungano na Zanzibar, Sheria ya Uchaguzi ya Taifa na Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar na. 11 | Bunge la Taifa, Baraza la Wawakilishi | *Kifungu. 2(3) cha ICCPR: "a) mtu yeyote ambaye uhuru wake .. unaingiliwa atakuwa na suluhisho stahili;"* ICCPR Maelezo ya Jumla 25: *"Kuwe na uchunguzi huru wa mchakato wa upigaji kura na kuhesabu pamoja na kuweza kutafuata suluhishi kumahakama au njia nyingine stahili ili wapiga kura wawe na imani wa usalama wa kura na zoezi la kuhesabu."* |

| Dhumuni na inapoptokea kwenye Ripoti | Pendekezo | Hatua zinazopendekezwa na muda, inapostahili | Taasisi inayolengwa na wadau wengine | Ahadi za Kimataifa/Kikanda za Msingi |
|---|---|---|---|---|
| **MFUMO WAKISHERIA** | | | | |
| Kujenga haki ya kuwakilishwa kisiasa na haki ya upatikanaji taarifa *Kurasa 14 ya* ***Ripoti*** | Orodha ya wagombea wanawake wa viti maalumu iliyowasilishwa na vyama vya siasa kwa NEC kabla ya uchaguzi isichukuliwe kuwa ni siri. Vyama vya siasa vitakiwe kisheria kutoa orodha ya wagombea wote wa viti maalumu vya Bunge la Muungano na Baraza la Wawakilishi. NEC na ZEC zinatakiwa kutangaza orodha hizo kuwezesha wapiga kura kufahamu wagombea watakaonufaika na kura zao. | Marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi ya Taifa na Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar na. 11 | Bunge la Muungano, Baraza la Wawakilishi | ICCPR Maelezo ya Jumla 25, aya 26: *"Ili kuhakikisha upatikanaji kamilifu wa haki zilizowekwa kwenye kifungu 25, ni lazima kuwe na upatikanaji huru wa taarifa na maoni juu ya maswala ya kijamii na kisiasa baina ya wananchi, wagombea na watendaji waliochaguliwa";* Kifungu 19(2) cha ICCPR: *"Haki ya kupata taarifa zilizo mikononi mwa taasisi za umma"* |
| Kulinda uhuru wa kujieleza na haki ya kujitetea mahakamani *Kurasa 27,28 na 38 za* ***Ripoti*** | Utekelezaji wa baadhi ya vifungu vya Sheria ya Makosa ya Mtandao yana uwezekano wa kubana uhuru wa kujieleza na kupelekeaa watu kukamatwa kiholela. Kanuni za utekelezaji zitengenezwe na kutumika kuleta utekelezaji wa sheria unaotabirika na unaoendana na uzito wa makosa. Watu wanaoshtakiwa kwa mujibu wa sheria hii wasinyimwe haki ya kujitetea mahakamani kama sheria invyosema kwa taratibu za kusikiliza maombi kukiwa na upande mmoja tu mahakamani na kwa siri. | Marekebisho ya vifungu kadhaa vya Sheria ya Makosa ya Mtandao kuondoa tafsiri binafsi za sheria, hususan kifungu 16 na maneno "kutangaza/kusambaza taarifa" na kifungu 38 kinachozuia kuwepo kwa mtu anyetuhumiwa mahakamani kujitetea. | Bunge la Muungano | Kifungu 14 cha ICCPR na Maelezo ya Jumla ya ICCPR 32, ibara 31: *"pale kesi inaposikilizwa bila upande mmoja kuwepo, kifungu 14, ibara 3(a) kinasema, bila kujali kutokuwepo kwa mshitakiwa, hatua zote stahiki zimechukuliwa kumuarifu mshtakiwa kuhusu tuhuma na kumuarifu kuhusu kusikilizwa kesi."* |

| Dhumuni na inapoptokea kwenye Ripoti | Pendekezo | Hatua zinazopendekezwa na muda, inapostahili | Taasisi inayolengwa na wadau wengine | Ahadi za Kimataifa/Kikanda za Msingi |
|---|---|---|---|---|
| **UTENDAJII WA UCHAGUZI** | | | | |
| Kujenga haki ya kupiga kura kwa wote *Kurasa 16 na 17 ya **Ripoti*** | Mipaka ya majimbo ipitiwe upya kuhakikisha majimbo yanaendana na mabadiliko ya idadi na makazi ya watu, hivyo kuchangia usawa zaidi wa kura. Haki sawa kwa wote ya kupiga kura ina maana kila kura ina uzito sawa. Hatua ziangaliwe kuhusu ushirikiano wa karibu kati ya serikali, inayowajibika kwa mipaka ya kata, na tume yauchaguzi, inayowajibika kwa mipaka y majimbo. | Shughulikia tofauti kubwa iliyopo ya idadi za wapiga kura walioandikishwa katika kila jimbo kuhakikisha kuwa mipaka inaendana na uwingi wa watu na hivyo kuongeza usawa katika uwakilishi Bungeni. | NEC na ZEC na mamlaka husika za Muungano na Zanzibar | Kifungu 25(b) na Maelezo ya Jumla ya ICCPR 25, ibara 21: *"katika mifumo ya uchaguzi ya kila nchi, kura ya mpiga kura mmoja itakuwa na uzito sawa nay a mwingine. Uchoraji wa mipaka ya maeneo ya uchaguzi na mfumo wa kutoa kura usiende kinyume na mgawanyo wa makazi wa wapiga kura na usibague kundi lolote wala usi nyime mwananchi yoyote haki ya kuchagua mwakilishi wake kwa uhuru"* ; Kifungu 21.3 cha UDHR |
| Kujenga uhuru na imani kwa utendaji wa uchaguzi *Ukurasa 14 ya Ripoti* | Hatua thabit zichukuliwe kupunguza uhusika wa vyombo vya utawala vya serikali na utegemeaji wa mifumo ya tawala za mitaa kwa mipango na utekelezaji wa mchakato wa uchaguzi. Uteuzi wa makamishna wa NEC upitiwe upya kujenga imani juu ya uhuru wa NEC | Kuanzishwa kwa mfumo huru wa kudumu wa NEC katika ngazi za mkoa, na wakati wa uchaguzi, mfumo wa muda katika ngazi za ya majimbo. | NEC na serikali ya Muungano | Maelezo ya Jumla ya ICCPR 25 ibara 20: *"mamlaka huru ya uchaguzi ianzishwe kusimamia mchakato wa uchaguzi na kuhakikisha kuwa unaendeshwa kwa usawa na biala upendeleo…";* Tamko la Umoja wa Afrika juu ya Kanuni zinazoongoza Chaguzi za Kidemokrasia barani Afrika la 2002, kifungu II.4€; kanuni na Miongozo ya SADC zinazoongoza Chaguzi za Kidemokrasia ya 2004, sehemu ya 7, kifungu 7.3 |
| Kuboresha uwazi, uwajibikaji na imani ya vyama vya siasa kwa mchakato wa uchaguzi *Kurasa 15 na 16 za **Ripoti*** | NEC na ZEC zianzishe sera za kujenga mawasiliano na kupeana taarifa na vyama vya siasa na kuboresha ufanisi wa idara zake za maelezo kuboresha upatikanaji wa taarifa kwa jamii. Maamuzi na kanuni za Tume za Uchaguzi zielezwe kikamilifu kwa wadau. | Taarifa kamili na za wakati zitangazwe na kusambazwa mapema, ikiwa ni pamoja na orodha za vituo vya kupigia kura, madaftari ya wapiga kura na maelezo mengine ya uendeshaji wa uchaguzi. | NEC na ZEC | Maelezo ya Jumla 25, ibara 26: *"ili kuhakikisha haki zilizotajwa kwenye kifungu 25, mawasiliano huru ya taarifa na maoni juu ya maswala ya kijamii na kisiasa kati ya wananchi, wagombea na wawakilishi waliochaguliwa ni lazima"*; Maelezo ya Jumla ya ICCPR 34 ibara 18 na kifungu 19(2) cha ICCPR: *"haki ya upatikananji maelezo yaliyopo mikononi mwa taasisi za umma".* |

| Dhumuni na inapoptokea kwenye Ripoti | Pendekezo | Hatua zinazopendekezwa na muda, inapostahili | Taasisi inayolengwa na wadau wengine | Ahadi za Kimataifa/Kikanda za Msingi |
|---|---|---|---|---|
| **UANDIKISHAJI WAPIGA KURA** | | | | |
| Kuhakikisha orodha ya wapiga kura iliyo kamili, isiyotenga au kubagua na inayoaminika<br>*Kurasa 19 na 20 za **Ripoti*** | Muda mrefu zaidi wa kuonyeshwa madaftari ya wapiga kura ya Muungano na Zanzibar utaboresha kwa kiasi kikubwa ubora wa madaftari hayo kwa chaguzi zijazo. | | NEC na ZEC | Maelezo ya Jumla ya ICCPR 25: *"Nchi zichukue hatua thabiti kuhakikisha kuwa wote wenye haki ya kupiga kura wanaweza kutumia haki kiyo."* |
| Kuhakikisha orodha ya wapiga kura isiyotenga au kubagua<br>*Kurasa 19 na 20 za **Ripoti*** | Kwenye swala la uandikishaji wapiga kura wa Zanzibar, sharti la kuwa na kitambulisho cha Zanzibar, pamoja na kuwa ukazi wa kipindi si chini ya miezi 36, lifanyiwe marekebisho kuzingatia tofauti iliyopo jinsi raia wa Tanzania wanavyoandikishwa Bara na Zanzibar. Mamlaka waliyopewa *masheh*a ya kutoa ushahidi wa makazi pia yapitiwe upya ili kujenga imani juu ya mchakato. Daftari la wapiga kura lisiwe na ubaguzi na muda unaohitajika wa ukazi upunguzwe. | Urefu wa muda wa ukaaji kwenye sharti la ukazi upunguzwe na mamlaka ya *masheha* yapunguzwe. | ZEC na taasisi za serikali ya Zanzibar | Maelezo ya Jumla ya ICCPR 25 uk. 11: *"Nchi zichukue ahtua thabiti kuhakikisha wote wenye haki ya kupiga kura wanaweza kutumia haki hiyo. Pale uandikishaji wa wapiga kura unapohitajika, uandikishaji huo urahisishwe na kusiwekwe vizingiti. Kama kuna sharti la makazi kwa uandikishaji, masharti hayo yaw yakueleweka/ yasiwe magumu mno."*; uk.12: *"hatua zichukuliwe kuondoa vizingiti vya uhuru wa kutembea/kuhama ambao unawanyima watu wenye haki ya kupiga kura kutumia haki yao ipasavyo."* |
| Kuongeza haki ya upatikanaji wa maelezo na kuhakikisha uwazi ili kujenga imani kwa madaftari ya wapiga kura.<br>*Ukurasa 20 wa **Ripoti*** | Vyama vya siasa vipatiwe taarifa za mara kwa mara na kwa wakati juu ya maongezeko, marekebisho na kufutwa majina kwenye daftari la wapiga kura mapema kutosha kabla ya uchaguzi kufanyika. | | NEC na ZEC | Maelezo ya Jumla ya ICCPR 34 uk. 18 na kifungu 19(2) cha ICCPR: *"haki ya upatikanaji wa taarifa zilizo mikononi mwa taasisi za umma"* |

| Dhumuni na inapoptokea kwenye Ripoti | Pendekezo | Hatua zinazopendekezwa na muda, inapostahili | Taasisi inayolengwa na wadau wengine | Ahadi za Kimataifa/Kikanda za Msingi |
|---|---|---|---|---|
| **ELIMU KWA WAPIGA KURA** | | | | |
| *Kuhakikisha haki kamili za kisiasa na haki ya kufanya chaguo baada ya maelezo.*<br>*Ukurasa 18 ya **Ripoti*** | Ili kuwapa wananchi taarifa mapema na kikamilifu juu ya mchakato wa kupiga kura na chaguo walizokuwa nazo, tume za uchaguzi ziangalie uwezekano wa kuchukua hatua kuboresha mipango, bajeti na utekelezaji wa shughuli za elimu kwa wapiga kura, shughuli zilenge makundi maalum kama vile vijana na wapiga kura wa mara ya kwanza, wanawake na watu wenye ulemavu | | NEC na ZEC | Maelezo ya Jumla ya ICCPR 25 uk. 11*: "Elimu ya wapiga kura na kampeni za uandikishaji wapiga kura ni muhimu kuhakikisha haki zilizotajwa kwenye kifungu 25 za jamii iliyo na maelezo kamili"*; uk. 12*: "Hatua thabit zichukuliwe kuondokana na matatizo… yanayonyima watu wenye haki ya kupiga kura kutumia haki yao hiyo kikamilifu. Mbinu maalum… zianzishwe kuhakikisha wapiga kura wasioweza kusoma na kuandika manapata maelezo ya kutosha ili kufanya maamuzi yao."* |
| **SIKU YA KUPIGA KURA** | | | | |
| *Kuhakikisha uwazi zaidi na kutabirika kwa taratibu za siku ya kupiga kura*<br>*Ukurasa 36 na 37 za **Ripoti*** | Maelekezo ya taratibu za hatua muhimu za ukusanyaji, usafirishaji na utangazaji matokeo yatolewe kuondoa tafsiri binafsi za wasimamizi wa uchaguzi. Mafunzo kwa maafisa wote wa uchaguzi ya kuhesabu na kujumlisha kura, hususan kujaza fomu mbali mbali, yanaweza kuboreshwa. Maelekezo na vitabu vya taratibu vitolewe kwa wingi kwa wasimamizi wa uchaguzi na wadau kabla ya siku ya kupiga kura. | Mafunzo bora kwa waafisa wa uchaguzi na wasimamizi wa vituo vya kupigia kura juu ya taratibu. | NEC na ZEC | |
| *Kuhakikisha kueleweka kwa nafasi ya vyombo vya usalama wakati wa uchaguzi*<br>*Ukurasa 44 wa **Ripoti*** | Nafasi ya vyombo vya usalama siku ya kupiga kura ipitiwe upya. mamlaka ya polisi na jeshi wakati wa uchaguzi yatajwe kikamilifu kwenye sheria na wapiga kura kuelezwa. | | Bunge la Muungano, Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Serikali zote, NEC na ZEC. | |

| Dhumuni na inapoptokea kwenye Ripoti | Pendekezo | Hatua zinazopendekezwa na muda, inapostahili | Taasisi inayolengwa na wadau wengine | Ahadi za Kimataifa/Kikanda za Msingi |
|---|---|---|---|---|
| **SIKU YA KUPIGA KURA** | | | | |
| Kuboresha uwazi wa mchakato<br>*Ukurasa 36 wa **Ripoti*** | Vyombo vya habari vinavyotambulika vipewe ruhusa kuingia kwenye vituo vya kupigia kura siku ya kupiga kura. Kanuni maalumu za vyombo vya habari ziandaliwe na tume za uchaguzi kwa kushirikiana na Baraza la Vyombo vya Habari Tanzania (MCT) | | NEC na ZEC | |
| **MATOKEO YA UCHAGUZI** | | | | |
| Kujenga imani ya mchakato wa uchaguzi<br>*Ukurasa 36 wa **Ripoti*** | Hatua mahsusi za uwazi, kama vile uwezo wa kuwafikia wawakilishi wa vyama vya siasa na waangalizi usiyo na vizuizi kwenye hatua zote za mchakatao wa ujumlishaji, zifikiriwe. Nyenzo stahili zenye mpangilio unaofaa ziwekwe kuruhusu usimamizi na uangalizi wa uafanisi wa mchakato. | | NEC na ZEC | |
| **MALAMIKO NA RUFAA** | | | | |
| Kuhakikisha haki ya suluhisho la kukidhi na la wakati<br>*Kurasa 22 na 33 za **Ripoti*** | Mahakama iwe na nafasi ya kueleweka ya uangalizi juu ya ufanisi na maamuzi ya tume za chaguzi. Maamuzi ya NEC na ZEC lazima yaweze kupitiwa mahakamani mara baada ya mchakato wa kupendekeza majina ya wagombea na wakati wote wa mchakato mzima. Walalamikaji wasilazimike kusubiri hadi kutangazwa matokeo kabla hawajaweza kusaka haki mahakamani. | | NEC, ZEC, Bunge la Muungano, Baraza la Wawakilishi na mahakama | Kifungu 2(3) cha ICCPR: *"a) mtu yeyote ambaye haki au uhuru wake… unakiukwa atapatiwa suluhisho la kukidhi haja yake.; (b) mtu yeyote anaye dai suluhisho kama hili haki yake kufanya hivyo itatathminiwa na mamlaka husika ya mahakama, kitawala au kisheria… na kuweka mazingira ya kuweza kupatikana kwa suluhiso la kisheria."* |

| Dhumuni na inapoptokea kwenye Ripoti | Pendekezo | Hatua zinazopendekezwa na muda, inapostahili | Taasisi inayolengwa na wadau wengine | Ahadi za Kimataifa/Kikanda za Msingi |
|---|---|---|---|---|
| **MALALAMIKO NA RUFAA** | | | | |
| *Hakikisha haki ya kupata suluhisho za kimahakama na kisheria*<br>*Ukurasa 34 wa **Ripoti*** | Gharama za kuwasilisha maombi zipunguzwe kwa kiasi kikubwa ili kuwapatia walalamikaji haki kamili ya kupata suluhisho la kisheria | Marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi ya Taifa na Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar na. 11 | Bunge la Muungano na Baraza la Wawakilishi | Kifungu 26 cha ICCPR*: "watu wote ni sawa mbele ya sheria na wana haki, bila ubaguzi, ya kulindwa sawa na sheria. Kwa swala hili, sheria… inwahakikishia watu wote kulindwa sawa dhidi ya ubaguzi kwa sababu yoyote…"* |
| Kuhakikisha haki ya kupata suluhisho kamili na kwa wakati<br>*Ukurasa 34 wa **Ripoti*** | Muda unaotajwa wa kuwasilisha na kushughulikia malalamiko Zanzibar uendane na muda uliotolewa na Muungano. Zanzibar, lalamiko linaweza kuwasilishwa mahakamani katika kipindi kisichozidi siku 15 baada ya kutangazwa matokeo wakati kwa Muungano lalamiko linaweza kuwasilishwa katika kipindi kisichozidi siku 30. Kwa kushughulikia malalamiko, Zanzibar mahakama inaweza kutoa uamuzi katika kipindi kisichozidi miezi 24 wakati kwa Muungano mahakama zimepewa muda usiozidi miezi 12 kutoa uamuzi. | Marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi ya Taifa na Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar na.11 | Bunge la Muungano na Baraza la Wawakilishi | |
| Kuhakikisha kuwa maamuzi yana misingi ya kisheria na yanatangazwa na kujenga imani juu ya uwazi wa mcakato.<br>*Ukurasa 33 wa **Ripoti*** | ZEC na NEC ziangalie uwezekano wa kuandaa na kutumia taratibu zinazotabirika na zilizo wazi kushughulikia malalamiko ya uchaguzi ili kuwa na uwiano wa jinsi zinavyoyashughulikia malalamiko. | | NEC na ZEC | Maelezo ya Jumla ya ICCPR 13 uk. 6: *"uwazi wa usikilizaji kesi ni sehemu muhimu ya kulinda maslahi ya mtu na jamii kwa ujumla… Kamati inaona kuwa… hata kwa kesi ambazo jamii hairuhusiwi kuwepo, uamuzi lazima, isipokuwa kwa sababu maalumu zilizoelezwa, utangazwe kwa jamii."* |

| Dhumuni na inapoptokea kwenye Ripoti | Pendekezo | Hatua zinazopendekezwa na muda, inapostahili | Taasisi inayolengwa na wadau wengine | Ahadi za Kimataifa/Kikanda za Msingi |
|---|---|---|---|---|
| **VYOMBO VYA HABARI NA UCHAGUZI** | | | | |
| Kuhakikisha uhuru wa vyombo vya habari vya taifa<br><br>*Ukurasa 27 wa **Ripoti*** | Vyombo vya utangazaji vya Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) na Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) vibadilishwe kuwa mashirika ya kuhudumia umma na kuwa huru kikamilifu kutokana na kuingiliwa kiuhariri na kifedha na serikali. | Kamilisha zoezi la kurekebisha mashirika hayo kama ilivyotajwa kwenye Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi wa Mawasiliano ya Tanzania ya 2003. | TCRA, Wizara ya Habari, Vijana Utamaduni na Michezo (Tanzania Bara); Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo (Zanzibar) | Maelezo ya jumla ya ICCPR34 ibara ya 16*: "Nchi lazima zihakikishe kuwa vyombo vya utangazaji vya umma vinafanya kazi kwa uhuru. Kwa hili, nchi lazima zivihakikishie uwezo wa kujitegemea na uhuru wa kiuhariri. Nchi zivipatie vyombo fedha kwa namna isiyoingilia uhuru wa vyombo hivyo.";* Tamko la Misingi ya Uhuru wa Kujieleza Afrika: Matangazo ya Jamii, kifungu VI: *"vyombo vya utangazaji vya umma na vya taifa vibadilishwe kuwa vyombo vya huduma kwa umma… kuendana na misngi ifuatayo: viongozwe na bodi zilizo huru na kuingiliwa, uhuru wa kiuhariri wa vyombo vya huduma ya utangazaji vya umma uhakikishwe, vyombo vya utangazaji vya umma vipatiwe fedha za kutosha kwa namna inayovihakikishia kutpoingiliwa bajeti zao kiholela, wajibu wa huduma ya utuangazaji wa vyombo vya utangazaji vya umma uelezwe kikamilifu na wajibu wa kuhakikisha kuwa jamii inapata taarifa za kutosha na zenye usawa kisiasa, hususan katika kipindi cha uchaguzi".* |
| Kuhakikisha uhuru wa TCRA na mchakato wa kuteua wawakilishi wake kutoka serikalini<br><br>*Ukurasa 30 wa **Ripoti*** | Uhuru wa TCRA uboreshwe kisheria ili kuwa na mfumo uliyo wazi wa kuteua wanabodi na mkurugenzi, usioingiliwa na chama chochote cha siasa, unaohusisha asasi za kiraia na wataalamu wa uandishi wa habari. | Rekebisha Sheria ya Usimamizi wa Mawasiliano ya 2003 | Bunge la Muungano | Tamko la Misingi ya Uhuru wa Kujieleza Afrika: Utangazaji wa Umma, kifungu VII: *"taasisi yoyote ya kitaifa yenye mamlaka kwenye maeneo ya utangazaji au mawasiliano lazima iwe huru na ilindwe vya kutosha dhidi ya kuingiliwa, haswa kisiasa au kifedha… mchakato wa uteuzi wa wanabodi wa taasisi ya usimamizi lazima uwe wazi, ushirikishe asasi za kiraia na usisimamiwe na chama chochote cha siasa."* |

| Dhumuni na inapoptokea kwenye Ripoti | Pendekezo | Hatua zinazopendekezwa na muda, inapostahili | Taasisi inayolengwa na wadau wengine | Ahadi za Kimataifa/Kikanda za Msingi |
|---|---|---|---|---|
| **VYOMBO VYA HABARI NA UCHAGUZI** | | | | |
| Kuboresha utofautishaji wa muda wa matangazo wa kampeni uliolipiwa na muda wa kutoa habari za kampeni wa kituo chenyewe. | Vyombo vya habari vieleze vipindi vilivyolipiwa au matangazo yaliyodhaminiwa na chama cha siasa kwa namna iliyo dhahiri ili wapiga kura waelewe aina ya kipindi. | | Vyombo vya habari | |
| *Kutoa muda wa matangazo unaolingana kwa wagombea*<br><br>*Ukurasa 29 wa **Ripoti*** | Muda wa bure unaotolewa kwa matangazo ya wagombea utolewe kwa njia iliyo na usawa, kwa misingi ya uwazi na kutofungamana. Taratibu za utoaji muda wa bure zielezwe kikamilifu. | Kupitia upya Sheria ya Uchaguzi; Sheria ya Huduma za Utangazaji | Vyombo vya habari vya taifa | *Misingi na Miongozo ya SADC inayoongoza Chaguzi za Kidemokrasia za 2004, kifungu 2.1.5: wanachama wa SADC [watatoa] "fursa sawa kwa vyama vyote vya siasa kupata muda kwenye vyombo vya habari vya taifa."* |
| *Sehemu za kanuni zinabana mno na zinaonekana kuingilia uhuru wa uhariri.*<br><br>*Kurasa 28 ya **Ripoti*** | Taasisi zinazosimamia vyombo vya habari ziangalie uwezekano wa kurekebisha Kanuni za Utangazaji wa Umma (Maudhui) (Matangazo ya Vyama Vya Siasa) ili kuwa na masharti yasiyo bana mno, hususan kwa vyombo binafsi. TCRA ipitie upya kanuni kwa namna shirikishi ikizingatia maoni ya wadau wa vyombo ya habari ambao walipatia kwa mara ya kwanza fursa ya kuzitumia kwenye uchaguzi huu. | Kurekebisha Kanuni za Utangazaji wa Umma (Maudhui) (Matangazo ya Vyama Vya Siasa) | TCRA | Maelezo ya Jumla ya ICCPR 25, ibara ya 26*: "utoaji huru wa maelezo na maoni juu ya maswala ya kijamii na kisiasa baina ya wananchi ni lazima. Hii ina maana vyombo vya habari huru na vyombo vingine viweze kuzungumzia maswala ya jamii bila kudhibitiwa na hivyo kutoa taarifa kuwezesha jamii kuwa na maoni. Inahitaji heshima kamili kwa… uhuru wa kujihusisha na shughuli za kisiasa kama mtu binafsi au kupitia vyama vya siasa au taasisi nyingine, uhuru wa kujadili maswala ya kijamii,… kukosoa na kupinga, kutangaza habari za kisiasa, kufanya kampeni za uchaguzi na kutangaza maoni ya kisiasa."* |
| Kuhakikisha uhuru wa kujieleza na adhabu zinazoendana na uzito wa makosa | Sheria zinazohusiana na uhuru wa kujieleza ikiwa ni pamoja na sheria mpya za Takwimu na Makosa ya Mtandao zirekebiswhe kuondoa adhabu | Rekebisha sheria zinazohusu uhuru wa | Bunge la Muungano | Maelezo ya Jumla ya ICCPR 25, ibara ya 26: *" utoaji huru wa maelezo na maoni juu ya maswala ya kijamii na kisiasa baina… ni lazima. Hii ina maana vyombo vya habari huru na vyombo vingine vinaweza kutoa maoni juu* |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| *Ukurasa 27 na 28 za* ***Ripoti*** | zisizoendana na uzito wa makosa. | kujieleza. | | *ya maswala ya kijamii bila kudhibitiwa wala kubanwa ili kuwezesha jamii kujenga maoni."* |

**ANNEX II: EU EOM MEDIA MONITORING RESULTS**

European Union Election Observation Mission
Tanzania 2015

# Media Monitoring Results

## For the period between
## 21 September and 24 October 2015

# European Union Election Observation Mission Tanzania 2015

The EU EOM conducted media monitoring of broadcast and print media outlets from 21 September till 24 October 2015, using quantitative and qualitative analyses, assessing the amount of time/space allocated to contestants (and other political actors) as well as the tone of their coverage. The media which were monitored are as follows:

The monitored media were:

The state-owned nation-wide TV channel Tanzania Broadcasting Corporation (TBC1); and Television Zanzibar (ZBC TV), available in Zanzibar and partially also on mainland Tanzania.

The private Independent Television (ITV), Channel 10, Star TV, and TV Azam 2 (all nation-wide except of Azam TV)

The monitored TV channels were recoded daily, during the evening prime time from 17:00 till 23:00

The state-owned nation-wide radio station Tanzania Broadcasting Corporation (TBC Taifa) and Radio Zanzibar, that is accessible only on the territory of Zanzibar (Radio Zanzibar was monitored from 29 September till 24 October)

Private Radio Free Africa and Radio One, both with nation-wide coverage


All stations were monitored daily from 6am till 8am and from 4pm till 21:30pm


The state-owned daily newspapers *Daily News* and *Zanzibar Leo* and the private dailies *Mwananchi* and *Nipashe*, as well as private weeklies *Mwana Halisi* and *Raia Mwema.*

Explanation of the charts: The pie charts show the percentage of airtime/space allocated to contestants and other subjects. The bar charts show how much airtime/space contestants and other subjects received, and the tone of their coverage - positive (green), neutral (white) and negative (red).


# European Union Election Observation Mission
# Tanzania 2015

## TBC TV news programmes





## TBC TV other editorial programmes






## TBC TV paid programmes




# European Union Election Observation Mission
# Tanzania 2015

## ZBC TV news programmes





## ZBC TV other editorial programmes (incl. free airtime)






## ZBC TV paid programmes




# European Union Election Observation Mission
# Tanzania 2015

## TV AZAM 2 news programmes





## TV AZAM 2 other editorial programmes






## TV AZAM 2 paid programmes




# European Union Election Observation Mission
# Tanzania 2015

## ITV news programmes





## ITV other editorial programmes






## ITV paid programmes




# European Union Election Observation Mission
# Tanzania 2015

## Star TV news programmes





## Star TV other editorial programmes






## Star TV paid programmes




# European Union Election Observation Mission
# Tanzania 2015

## Channel 10 TV news programmes





## Channel 10 TV other editorial programmes






## Channel 10 TV paid programmes




# European Union Election Observation Mission Tanzania 2015


## TBC Radio news programmes





## ZBC Radio news programmes





# European Union Election Observation Mission
# Tanzania 2015


## Radio One news programmes





## Radio Free Africa news programmes





# European Union Election Observation Mission
# Tanzania 2015


## Daily News





## Zanzibar Leo





# European Union Election Observation Mission
# Tanzania 2015


## Mwananchi





## Nipashe





# European Union Election Observation Mission
# Tanzania 2015


## Raia Mwema




## Mwana Halisi



# European Union Election Observation Mission
# Tanzania 2015

| | | | |
|---|---|---|---|
| Alliance for Change and Transparency | ACT | National  Reconstruction Alliance | NRA |
| Alliance for Democratic Change | ADC | Progressive Party of Tanzania | PPT |
| Allaince for Tanzania Farmers Party | AFP | Sauti ya Umma | SAU |
| Chama Cha Kijamii | CCK | Tanzania Democratic Alliance | TADEA |
| Chama Cha Mapinduzi | CCM | Tanzania Labour Party | TLP |
| Chama Cha Demokrasia na Maendeleo | CHADEMA | President of United Republic of Tanzania | TZPRES |
| Chama Cha Ukombozi wa Umma | CHAUMMA | Vice-president of United Republic of Tanzania | TZVP |
| Chama Cha Haki na Ustawi | CHAUSTA | United Democratic Party | UDP |
| Civic United Front | CUF | Umoja wa Katiba ya Wananchi | UKAWA |
| Demokrasia Makini | DM | Union for Multiparty Democracy | UMD |
| Democratic Party | DP | United People's Democratic Party | UPDP |
| Government | GOV | President of Zanzibar | ZPRES |
| National Convention for Constitution and Reform | NCCR | 1st Vice-president of Zanzibar | ZVP1 |
| National League for Democracy | NLD | 2nd Vice-president of Zanzibar | ZVP2 |

